Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Sita - Tarehe 20 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 73

**Ujenzi wa Soko - Ruaha na Mifereji ya Maji ya Mvua**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kulikuwa na ahadi ya kujenga soko katika Mji Mdogo wa Ruaha kwenye kata ya kidodi Wilayani Kilosa katika kipindi cha 2004/2005:-

(a) Je, ni lini sasa ujenzi huo utaanza?

(b) Kwa kuwa, Mji huo unahitaji pia kuchimba mifereji ya kupitisha maji ya mvua wakati wa mvua nyingi, Je, ni lini upimaji na uchimbaji mifereji utaanza ili kuuokoa Mji huo?

(c)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (K.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher S. Wegga, Mbunge wa Mikumi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli soko la Ruaha lililopo Kata ya Kidodi Wilayani Kilosa linahitaji kujengwa upya ili liweze kukidhi matakwa ya watumiaji. Ili kufanikisha azma hiyo mnamo mwaka 1999 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ikisaidiana na wananchi ilijenga mabanda ya biashara kuzunguka eneo la soko hilo. Mpango uliopo sasa ni kujenga soko la kisasa ambalo linakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 30.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imeshafanya mikutano na wadau wa soko la Ruaha wakiwemo wafanyabiashara na tayari wamekubaliana kurekebisha mchoro wa soko hilo ili liweze kuchukua wafanyabiashara wengi zaidi. Baada ya kukamilisha kazi ya awali ya kitaalam na ushirikishwaji wa wadau, Halmashauri ya Kilosa imeweka kipaumbele cha kujenga soko hilo katika bajeti yake ya 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli lipo tatizo la maji ya mvua kutiririka na kujaa katika Mji wa Ruaha. Kujaa kwa maji katika Mji huo kunatokana na sababu za umbile la ardhi kwani Mji huu unaojengwa chini ya milima ya Vidunda. Aidha, mbali na sababu za kimaumbile, Mji wa Ruaha ulijengwa kiholela ukiwa ni msongamano mkubwa wa nyumba za makazi na biashara kwa sababu eneo hili lilijengwa bila kupimwa. Hivyo ili kufanikisha zoezi la kupitisha mifereji, lazima mji huo upimwe na kuvunja baadhi ya majengo, hivyo shughuli hii inahitaji gharama kubwa za fidia kwa mali za wananchi zitakazoharibiwa. Kwa sasa Serikali haina uwezo huo, hivyo itaupa kipaumbele na kuutekeleza mradi huo baadaye pale itakapopata uwezo wa kifedha.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Lakini pia nimshukuru Naibu Waziri kwa jibu hasa hasa kukubali kwamba wameweka kwenye bajeti ijayo milioni 30 kujenga soko. Je, sasa Wizara itahakikisha inasimamia vizuri suala hili kwa sababu wilaya imechukua muda mrefu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO (k.n.y. WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuwasaidia wananchi na hasa katika hatua hii ambayo imefikiwa ya kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya kukubaliana kutenga fedha na hatimaye kulijenga hilo, Serikali itakuwa tayari kusimamia na kuwasaidia.

Na. 74

**Soko kwa Ajili ya Mtama**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, inasemekana kwamba nchi ya Italia inataka kununua mtama mwingi sana mweupe kutoka Tanzania kwa ajili ya matumizi yao:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo na kwamba kama ni kweli wananchi wameshajulishwa ili waweze kuuza mtama huo na kuondokana na umaskini?

(b) Je, tunayo mbegu ya kutosha kuwagawia wananchi wote hasa wale wa mikoa kama ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Musoma (Mara) na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inazo habari kuhusu Chama cha Wafanyabiashara wa Kiitaliano wanaofanya biashara na nchi za kiafrika kiitwacho *Convivium 2000,* na kwamba wanahitaji kununua jumla ya tani 300,000 za matama mweupe kutoka Tanzania kwa mwaka. Hali ya uzalishaji wa zao la mtama kwa ujumla ilikuwa ni wastani wa tani 244,300 mwaka 2001/2002 na tani 186,100 mwaka 2002/2003. Kama sehemu ya kujiandaa na changamoto hii ya kupatikana kwa soko hilo la mtama, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitoa taarifa kwa mikoa yote Tanzania Bara juu ya upatikanaji wa soko hilo pamoja na viwango vya bei. Taarifa ya bei iliyopatikana kutoka kampuni hiyo ni Dola za Marekani 115 hadi 120 kwa tani ya mtama *CIF* Bandari ya Ravena, Italia sawa na shilingi 121,848/= hadi 127,146/= kwa tani. Pamoja na taarifa hizo kwa Mikoa hiyo hadi kufikia Januari 2005, ni mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Rukwa, Lindi, Dar es Salaam, Singida, Mwanza, Tabora, Kagera, Mbeya, Morogoro na Ruvuma tu ndiyo iliyoonyesha nia ya kuzifanyia kazi taarifa hizo ili kuweza kushiriki katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendeleza mawasiliano na Kampuni hiyo kwa lengo la kuifahamu kwa kina kampuni yenyewe pamoja na kushauriana nayo juu ya mpango endelevu wa kuzalisha kiasi kinachohitajika katika muda utanaokubaliwa ili kuhakikisha biashara hii inawanufaisha wazalishaji wetu, na kuwaondolea umaskini. Napenda kupitia Bunge lako Tukufu kutoa mwito kwa wakulima wote katika maeneo hayo wazingatie uzalishaji wa zao hilo kwa viwango vya ubora vinavyotakiwa ili kukidhi mahitaji ya soko na hatimae kujiongezea kipato na kuwawezesha kuondokana na umaskini.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya upatikanaji wa mbegu za mtama, taarifa zinaonyesha kuwa hadi Januari, 2005 kulikuwapo na jumla ya takriban tani 10,098 za mbegu za mazao mbalimbali ya nafaka, kati ya hizo tani 331 zilikuwa mbegu za mtama. Mbegu hizo zipo za kutosha na zinapatikana kibiashara katika mashamba ya Serikali, makampuni yanayofanya biashara ya mbegu kutoka kwa wakulima wanaozalisha mbegu chini ya utaratibu wa uzalishaji wa mbegu kwa kuwatumia wakulima.

(c) Mheshimiwa Spika, mazao mengine yanayotakiwa na kampuni hiyo ya Italia na yanayoweza kuzalishwa katika mikoa iliyotajwa ni mahindi na soya. Kiasi cha mazao hayo kinachohitajika katika Soko hilo ni mahindi tani 400,000 kwa mwaka kwa bei ya dola za Marekani 120 hadi 130 kwa tani, ambapo Soya zinahitaji tani 150,000 kwa mwaka kwa bei ya dola za Marekani 210 hadi 215 kwa tani.

Serikali inaendelea kutoa mwito kwa wadau wengine katika sekta binafsi, kupitia vyama vyao kama vile *TCCIA* na Taasisi na Wakala wa Serikali. Kushiriki katika

biashara hii kwa kuweka mikakati ya pamoja na madhubuti itakayowawezesha wakulima wetu kufaidika na fursa hii iliyojitokeza.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mtama mweupe uko aina nyingi.

(a) Je, Waziri atakuwa tayari kutuambia mtama mweupe ni upi kwa jina la Kiswahili, kiingereza na *Scientific name?*

(b) Kwa kuwa wananchi wa Iramba Mashariki ni wakulima wazuri sana wa matama na kwa kuwa Serikali sasa hivi lengo lake ni kuwasaidia wananchi waondokane na umaskini. Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa Iramba Mashariki ili waweza kulima mtama mwingi na kuuza huko Italia na umaskini waondokane nao?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu mtama mweupe ni wa aina ipi, nilisema hapa niliopokuwa najibu swali la msingi nimesema kwamba Serikali inaendeleza mawasiliano na kampuni hii. Ili kuweza kujua kwa uhakika pamoja na hili la kujua mtama mweupe ni wa kiasi gani na viwango, na namna hata ya hufanyaji wa biashara. Kwa hiyo, tunaendeleza mawasiliano hayo, tukishapata hizo *specification* alizosema Mheshimiwa Mbunge tutakuwa tayari kutoa taarifa kama ambavyo tulitoa wakati kampuni hii ilipokuja kujitangaza. Lakini kuhusu ni namna gani Serikali itawasaidia wakulima wa Iramba kuweza kulima mazao ya kuwaondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme kwamba Serikali imeendelea kusaidia wakulima katika njia mbalimbali. Moja ya njia zinazotumika ni kama hivi nasema kwamba mbegu zipo za kutosha ambapo wakulima wanaweza wakajipatia kuweza kupanda, lakini hata hivyo wenzetu wa Wizara ya kilimo na chakula wanatoa utaalam kwa kupitia maafisa ugani walioko kule mikoani kuweza kuwasaidia wakulima wazalishe hivi viwango vinavyotakiwa na hatimaye kujiondolea umaskini.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo. Kwa kuwa wananchi wa Singida na hasa Singida Kusini wameupokea mpango huu kwa moyo mkunjufu na kwa matumaini kwamba utawaondolea au utawapunguzia sana umaskini. Je, ni lini mpango huu unatarajiwa kuaanza na ni taratibu gani ambazo Serikali imeweka au itaweka ili kuwawezesha wananchi hawa kuweza kupata kuchukua mazao yao ya mtama na kufikisha huko kwenye soko linakohitajika. Ahsante sana

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nilipokuwa najibu swali la msingi hapa nilieleza jinsi Serikali ilivyoupokea mpango huu na kutoa taarifa kwa mikoa mbalimbali, na vilevile nimesisitiza na kutoa mwito hapa kwamba wananchi katika mikoa inayohusika na ulimaji wa zao hili la mtama pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuliopo hapa kwamba tupokee changamoto hiyo kwa kuhimiza uzalishaji wa mazao haya.

Kwa hiyo kimsingi utaratibu huu umeanza na kama nilivyosema kwamba mawasiliano yanaendelea na kampuni hii, na vilevile nimetoa mwito kwamba makampuni mengine sasa ya wafanyabiashara binafsi, vilevile wajiingize katika suala hili tuweze tukapanga mikakati ya pamoja na hatimaye tuweze tukanufaika na fursa hii.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge ningependa kutambulisha wageni waliotoka Ujerumani ambao wako katika *Gallery* ya Spika asubuhi hii.

**WABUNGE FULANI:** Papa.

**SPIKA:** Siyo, ni mkuu wa Shirika la *Fredrish Eberty Foundation,* kutoka Berlin na *Resident Director* wake hapa Dar es Salaam. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 75

**Bei ya Pamba**

**MHE. LUCAS L. SELELII (k.n.y. DR. RAPHAEL M. CHEGENI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wa pamba hapa nchini mwaka jana walipata hasara kubwa sana kutokana na kushuka kwa ghafla kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia na hivyo kuwafanya wakulima wa zao hilo hapa nchini kuwa maskini mwaka hadi mwaka kutokana na kushindwa kwa Bodi ya Pamba kuwawekea wakulima mazingira yanayofaa kwa kilimo bora/ cha kisasa kitakachowapatia mavuno mengi kwa gharama nafuu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuwasaidia wakulima kupata Bima ya Kinga ya Mazao ili kuepuka tatizo la kushuka kwa bei ya mazao kiholela kwenye soko husika na kuwawezesha pia kupata uhakika wa kilimo badala ya utaratibu uliopo sasa wa kuwapatia bei ambayo haiwasidii?

(b) Kwa kuwa mwaka jana Serikali ilitambua umuhimu wa kuwapatia wakulima bei itakayofidia gharama za uzalishaji kwa kufuta baadhi ya kodi zinazotozwa katika soko hilo. Je, hadi sasa ni wakulima wangapi wamelipwa fidia ya bei ya shs. 275/= kama ilivyotangazwa na Serikali na ni kutoka Wilaya zipi, wangapi hawajalipwa, kutoka katika wilaya zipi na kwa nini?

(c) Je, Serikali inatoa matumaini gani kwa wakulima wa pamba mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Raphael Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na kinga ya mabadiliko ya bei ili kumlinda mkulima dhidi ya anguko la bei kwa mazao yake. Hivi sasa Serikali inakamilisha maandalizi ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ambayo itaelekeza mikakati ya kukabiliana na tatizo la kuanguka kwa bei za mazao, ukiwemo mkakati wa kutumia kinga ya Bima. Aidha Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeandaa mafunzo ya jinsi ya kujikinga na mabadiliko ya bei ya mara kwa mara. Mafunzo haya yataanza kutolewa kati ya mwezi Mei na Juni 2005. Bodi ya Pamba itaratibu mafunzo yatakayohusu zao la pamba. Wakulima na wafanyabiashara wa pamba na Waheshimiwa Wabunge wanaowakilisha majimbo yanayolima pamba wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika mafunzo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu Swali Na. 30 la Mheshimiwa James Musalika, katika mkutano huu wa 19 wa Bunge lako Tukufu, kati ya makampuni 34 yaliyoshiriki katika ununuzi wa pamba msimu wa 2004/2005, makampuni tisa yamelipa mapunjo ya bei ya jumla ya shilingi 51,950,936/= katika wilaya 11 za Magu, Kwimba, Misungwi, Sengerema, Ilemela, Nyamagana, Geita, Bariadi, Maswa, Bukombe na Biharamulo. Wilaya za Igunga, Iramba, Bunda, Musoma, Kahama, Shinyanga, Meatu, Kishapu na Serengeti bado hazijaonyesha takwimu za idadi ya wakulima ambao bado hawajalipwa mapunjo yao.

(c) Mheshimiwa spika, kwa mujibu wa makubaliano ya kikao cha pamoja baina ya Viongozi wa Wilaya, Wanunuzi wa pamba na Bodi ya Pamba kilichofanyika tarehe 17 Februari, 2005 Jijini Mwanza, wanunuzi ambao hawatakuwa wamewalipa wakulima mapunjo ya bei hadi tarehe 31 Machi, 2005 hawatashiriki katika biashara ya pamba msimu ujao wa 2005/2006.

Aidha, wafanyabiashara hao watachukuliwa hatua za kisheria ili kuhakikisha wakulima wanalipwa haki zao. Kwa sasa Serikali inafuatilia kwa viongozi wa wilaya juu ya utekelezaji wa makubaliano ya kikao hicho. Hivyo wakulima wa pamba wawe na matumaini kuwa Serikali inasimamia na kufuatilia upatikanaji wa haki zao.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, kwa kuwa wakulima wa Jimbo la Busega, Igunga, Iramba walikatwa fedha zao za fidia ya mazao kwa mfuko wa bembejeo kwa kutumia *pass book,* na kwa kuwa mpaka sasa hivi bado hawajalipwa na wanadai,

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa suala hili la madeni kwa wakulima?

La pili kwa kuwa gharama za kilimo, kilimo cha pamba kiko juu sana kuliko bei ambayo mkulima anapewa. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuweka bima ya bei ya mazao hasa kwa zao hili la pamba?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zilizokatwa kupitia *pass book* za wakulima na madeni ya wakulima kwa ujumla. Kama ambavyo tulisema wakati tunawasilisha Muswada ambao tuliumaliza jana hapa kwamba madeni mbalimbali ambayo wakulima wanadaiyana na Vyama vya Ushirika

ama Taasisi nyingine kwa ujumla wake yanafuatiliwa na Serikali, na tukasema kwamba zoezi hilo litakapokuwa limekamilika basi tutaainisha madeni ya kweli, yale ambayo yametokana na sababu ambazo ni za msingi, Serikali iweze kuangalia na kutoa msimamo wa namna ya kuyashughulikika.

Kwa hiyo ningependa kusema tu kwamba madeni ya wakulima kwa ujumla yote yanashughulikiwa na Serikali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuhusu gharama kubwa ya kuwekewa Bima nadhani ndio swali la msingi lilivyokuwa linaelekeza kwamba tutaandaje utaratibu wa kuweka kinga juu anguko la bei.

Lakini pamoja na hayo kuangalia gharama kubwa ya ukilinganisha na ile bei inayopatikana, nimesema kwamba utaratibu unaandaliwa ambapo tumetoa mwito tu hapa kwamba Serikali kwa kushirikiana na benki ya dunia wataandaa mafunzo ama semina ambazo zitatoa maelekezo ya kuandaa utaratibu huo, na tukaalika kwamba Waheshimiwa Wabunge wanatoka kwa maeneo husika nao waweze kuhudhuria.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda niulize kama ifuatavyo;

Kwa kuwa wakati anajibu swali langu la tarehe 13 mwezi huu kuhusu wanunuzi ambao hawajalipwa mapunje ya wakulima alisema kwamba ni makampuni tisa yameshalipa na katika hela zilizolipwa ni pamoja na Geita na kwa kuwa kuanzia siku hiyo hadi leo asubuhi baadhi ya wakulima wamekuwa wakinipigia simu nao wanasikiliza sasa hivi kusema kwamba hawajalipwa hata mmoja. Serikali inatamko gani nao wanasikiliza huko wasikilize? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nilisema kweli kwamba ni makampuni tisa tu ambayo yamewalipa wakulima kati ya makampuni 34. Sasa makampuni haya tisa yamegusa wilaya mbalimbali ambazo yalikuwa yamenunua.

Lakini makampuni mengine yaliyobakia bado hayajalipa ina maana kwamba katika makampuni yale yaliyobakia baadhi ya wakulima lazima watakuwa wako zile wilaya zingine ambazo zimeshalipwa na makampuni yale tisa.

Na. 76

**Ustawi wa Wazee Wastaafu Tanzania**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na sera nzuri inayoandaliwa na Serikali kuhusu Wazee pamoja na Wastaafu nchini kote:-

(a) Je, isingekuwa wakati muafaka kwa nchi yetu kuandaa utaratibu wa jinsi ya kuwapatia Wazee maslahi angalau ya kujikimu wakati wanaposhindwa kuendelea na kazi?

(b) Je, Serikali itakapoandaa utaratibu w ajinsi ya kuwasaidia wazee wastaafu wa kazi za umma, kwa nini wasifanye hivyo hivyo kwa wengine kwa kutumia mifuko mingine ya pensheni nchini?

(c) Je, maamuzi ya Serikali kutaka kuwahudumia wazee wastaafu wa Serikali yatagharimu kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, mwezi, Septemba, 2002 Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Wazee. Madhumuni ya jumla ya Sera kuhakikisha kwamba wazee wanatambuliwa, na kupewa huduma muhimu kwa ajili ya kuboresha maisha yao. Sera hii inawahusu wazee wote waliopo mijini na vijijini, waliokuwa kwenye ajira rasmi na isiyo rasmi. Sera inalenga katika kuboresha maisha ya wazee katika nyanja mbalimbali. Hatua za Serikali za kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaafu na msamaha wa uchangiaji gharama za matibabu Hospitalini zinalenga katika kuboresha maisha ya wazee wetu. Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Wazee Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha maisha ya wazee wastaafu na wale ambao hawakuwa na ajira rasmi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kimiti kwa ushauri wake wa Serikali itatilia maanani wakati wote wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee.

(b) Mheshimwa Spika, Serikali haijawa na utaratibu wa kuwapatia wazee maslahi ya kujikimu wanaposhindwa kuendelea na kazi nje ya pensheni. Mifuko ya Pensheni nchini kama vile *NSSF, PPF* na *LAPF* itaendelea kutoa pensheni kwa wastaafu waliochangia Mifuko hiyo. Utaratibu wa kuwaingiza katika mpango wa pensheni wazee wasio katika sekta rasmi unafanyiwa utafiti kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gharama ya wastaafu wa Serikali hubadilika badilika kutokana na idadi yao kuongezeka kila mwaka, tumelipeleka suala hili Wizara ya Fedha ili lifanyiwe uchambuzi wa kutosha.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Waziri atakubaliana nami, ya kwamba kwa kipindi kirefu pamoja na Sera nzuri tulizoziandaa kwa kuwa hakuna kitengo maalum cha kushughulikia wazee, atakubaliana nami ya kwamba wakati umefika kuwe na kamisheni maalum ya wazee, na kama haiwezekani, kwa nini asiniruhusu ni kaja na hoja na binafsi ili Wabunge waniunge mkono tuwe na kitengo hicho?

(b) Waziri atakubaliana nami ya kwamba kutokana na utaratibu ambao wazee hawana kitengo maalum cha kuwasaidia. Matatizo makubwa yaliyojitokeza hasa kuhusiana na wazee wetu wa Afrika Mashariki wafanyakazi, wamekuwa wakisumbuka, wamekuwa kila wakati wakiandamana bila kupata msaada wowote. *(Makofi)*

Je, Waziri anasema nini kuhusiana na mafao yao, kwa sababu Waziri alituambia ya kwamba anangoja kibali cha Bunge, hivi miaka 27 unangoja kibali cha Bunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Lakini ukitaka kuleta hoja binafsi, huhitaji ruksa ya Waziri unahitaji ruksa ya Spika.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu rai yake ya kutaka Wizara itenge kitengo maalum cha kushughulikia wazee. Sisi kama Wizara tunapokea ushauri wake, lakini kwa sababu yeye alikuwa Waziri wa Wizara hii nina amini kwamba anafahamu si jambo linaloweza kutolewa jibu papo kwa papo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, inafurahisha sana tunapoona utamaduni mpya wa aina hii, lakini ningependa nirudie ili kwa faida yao waweze kuelewa. Nasema nimekubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Waziri kwa kuzingatia kwamba alikuwa ni Waziri katika Waziri katika Wizara hii.

**WABUNGE FULANI:** Aaa.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA MICHEZO:** bila ya shaka anafahamu kwamba utaratibu wa kutengwa kitengo katika Wizara hauwezi ukatolewa papokwa papo, maana kuna taratibu za kutengeneza vitengo katika Wizara mbalimbali.

(b) Kuhusu mafao ya wafanyakazi wa Afrika Mashariki, kuunganishwa na kitengo maalum cha wazee ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, bila ya shaka ni jambo halifanani sana, lakini Wizara inayoshughulikia na masuala haya ya Wizara ya Fedha, bila shaka imemsikia Mheshimiwa Kimiti na mimi sioni kama kuna uhusiano wa moja kwa moja wa kitengo cha wazee Wizara ya Kazi na malipo ya wastaafu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Wizara hii inaitwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ukiwemo na mpira wa miguu na kama unavyofahamu juzi juzi ilikuwepo mechi kali kati ya Simba na Yanga zote za Dar es Salaam. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jibu la nyongeza, ningependa kuongezea kidogo juu ya jibu zuri ambalo ametoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu jinsi tunavyowahudumia wazee, Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba Sera ya wazee imekwisha kamilika na imekwisha tolewa.

Ndani ya Sera ya wazee jinsi ambavyo wazee hawa watakavyosaidiwa namna ya kukabiliana na hali ngumu ya maisha. Ikiwemo hata utaratibu wa kutengeneza mfuko maalum.

Bado kinachoangaliwa ni mikikakati ya utekelezaji wake, lakini vile vile si sahihi kusema kwamba wazee hawa tu ndio hawaangaliwi kwa sababu suala sio kitengo tunayo kamisheni nzima ya ustawi wa jamii na majukumu yake makubwa katika ustawi wa jamii ni kuangalia walemavu, kuangalia wazee na kuangalia watoto yatima na kuangalia watoto walio katika mazingira magumu.

Kwa hiyo, ni kweli hapa Serikali kwa dhati kabisa inachukulia suala la wazee kwa nguvu zake zote.

**SPIKA:** Na kuhusu malipo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi waliokuwa wafanyakazi wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitoa tamko kwamba yuko tayari kuzungumza nao kuhusu mafao yao, endapo wataondoa kesi yao mahakamani.

Walifanya hivyo na walizungumza na Wizara ya Fedha, na tarehe 25 kikao cha pamoja cha hao wastaafu pamoja na Wizara ya Fedha walitoa ripoti yao juu ya fedha zao, juu ya mafao yao, na hiyo inafanyiwa kazi.

**WABUNGE FULANI:** wapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Tarehe 25 Januari wahusika ni wafanyakazi 28,000. Si rahisi kuweza kupitia yote ukatoa mafao yao na kwa wakati mmoja. Lakini sasa hivi Serikali inaendelea na suala hili.

Na. 77

**Bei Maalum kwa Mazao ya Wakulima**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingine duniani huwa na bei maalum ya mazao kwa wakulima hasa kwa akiba *(SGR)* na mazao mengine ya ziada humwachia mkulima ayauze kwenye soko huria:

(a) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu huo utamfanya kila mkulima afahamu kwa hakika mchango wake ni nini kwa Taifa?

(b) Je, mchango wa *'SGR'* si ungekuwa ndio msingi wa kuanza kuwa na utaratibu wa kuwawekea bima wakulima baada ya kuishiwa nguvu za uzalishaji na kuziwezesha katika maisha ya uzeeni kama watumishi wengine?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa hiyo ndiyo njia pekee ya wakulima wadogo wadogo itakayowawezesha kujiwekea akiba kwa maslahi yao ya baadaye?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edson Mbeyale Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Idara ya Usalama wa Chakula yameorodheshwa chini ya kifungu cha nane cha Sheria ya Usalama wa Chakula Na. 4 ya mwaka 1991. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, majukumu ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(The Strategic Grain Reserve)* ni kununua mazao kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa, kutunza chakula hicho na kuandaa na kutekeleza utaratibu wa kukizungusha *(recycling/rotation)* chakula hicho na kukisambaza kama itakavyoelekezwa. Hifadhi ya Chakula ya Taifa haikukusudiwa kutumia kama madhumuni anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge na kama kuna haja ya kutekeleza majukumu haya, itabidi kutunga sheria nyingine maalum kwa ajili hiyo. Mheshimiwa Mbunge anaweza kuleta Muswada binafsi Bungeni kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Katika kuendesha Hifadhi ya Taifa ya Chakula, Wizara imeweka utaratibu wenye malengo ya kumsaidia mkulima kama ifuatavyo:-

(a) Inatarajiwa kwamba mkulima atauza mazao yake kwenye soko huru. Iwapo mkulima atakosa soko kwa mazao yake au iwapo bei atakayokuta kwenye soko itakuwa

ndogo, anaweza kuyauza kwa *SGR* kwa bei itakayokuwa imewekwa. Kwa maneno mengine, Hifadhi ni kimbilio la mwisho yaani *buyer of last resort* na haikusudiwi kushindana na wanunuzi binafsi kwenye soko.

(b) Mara nyingi, Hifadhi imetumiwa kumhakikishia mkulima bei nzuri, hususan pale wafanyabiashara wanapompa bei ndogo mno.

(c) Kuna nyakati ambapo chakula kilichohifadhiwa katika *SGR* kimesambazwa kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula ili kuwawezesha wananchi kupata chakula kwa bei nafuu au kushusha bei za chakula katika soko.

Wizara ingependa Hifadhi ya Chakula ya Taifa iendelee kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Sheria na tunakusudia kuleta Bungeni marekebisho ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1991 yatakayotenganisha Hifadhi ya Chakula ya Taifa na Idara ya Usalama wa Chakula na kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kuendesha na kusimamia Hifadhi hiyo.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri ambayo kwa kweli hayasaidii sana katika mlolongo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara haoni ni aibu maeneo ya nchi hii mengine yana njaa na mengine chakula kipo kinasazwa, bila kukisambaza kwa utaratibu unaoeleweka na kuacha hali ya chakula iwe huria kama anavyoeleza?

La pili tunasema ukulima ni kazi na watumishi wana akiba yao pensheni baada ya maisha yao kuwa ya utu uzima. Je, hivi mkulima huyu anafaidika nini katika Dunia hii kuzalisha, kunyonywa, kupuuzwa anakufa na sanda ya kununuliwa tu, bila kufikiri bima yake kwa kumfanyia akiba ya mazao haya *SGR* si ingefanya kazi hiyo kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edson Halinga kama ifuatavyo:-

Kwa kweli Wizara ya Kilimo inajitahidi sana. Kwa mfano kwa mwaka huu imehakikisha imenunua mazao kwa wingi na tumepata kwa mara ya kwanza kuwa na akiba inayozidi tani 125,000. Tumejitahidi na tunastahili sifa angalau kwa hilo na kama kuna uhakika yako mahindi yamebaki mahali leo tuonane nikitoka hapa tutayafuatilia, tutanunua yote. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Wapi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** La pili, ni kweli ukulima ni kazi na kweli anavyosema mkulima hana pensheni. Lakini tumeshaambiwa kuwa masuala ya wazee na wengine yanashughulikiwa na Wizara ya Kazi hapa hapa kabla yangu tumepata jibu hilo. Lakini vile vile kwa sasa vipo *provision* mbalimbali za kuziwekea akiba, iko bima ukienda kwenye Ofisi ya Bima hapa hapa Dodoma unaweza

hawaulizi unafanya kazi gani, unaweza ukajiwekea. Lakini vilevile tumesema kama unaona kuna njia au umuhimu wa kufanya suala hili zaidi ya haya tunayofanya, tafadhali leta hoja binafsi. *(Makofi)*

Na. 78

**Matrekta**

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2003/2004 Serikali iliahidi kuwakopesha wananchi matrekta mapya na wananchi kupewa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kuyafanyia ukarabati matrekta waliyonayo:-

(a) Je, Serikali imewakopesha wananchi wangapi katika Wilaya ya Kahama?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kila kijiji nchini kipatiwe angalau matrekta mawili yamilikiwe na kijiji kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kwa gharama nafuu/kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wananchi walioomba mikopo ya matrekta kutoka Wilaya ya Kahama ni 42. Maombi mawili kati ya hayo ni ya kununua matrekta mapya na 40 ni ya kukarabati matrekta machakavu. Baada ya Mfuko wa Pembejeo kufanya uchambuzi wa maombi hayo, ilibainika kuwa maombi manne tu ndiyo yalikuwa yametimiza masharti ya mikopo na hivyo kupitishwa na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko. Waombaji ambao maombi yao yalipitishwa na Bodi ya Mfuko waliandikiwa barua zilizowataka kuwasilisha kadi halisi za matrekta yatakayokarabatiwa, ankara vifani za vipuri vinavyotakiwa na dhamana za mikopo ili waweze kupewa mikopo yao. Hadi sasa hakuna mwombaji aliyejitokeza kuchukua mkopo wake. Uongozi wa Mfuko unawasiliana na Halmashauri za Wilaya husika ili kujua sababu za waombaji hao kutochukua mikopo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la kuwepo kwa matrekta kwenye vijiji ni zuri sana na Serikali imekuwa ikihimiza wananchi kununua matrekta kwa wingi ili kuongeza kiwango cha matumizi ya matrekta nchini. Suala la nani atamiliki matrekta kwenye vijiji linahitaji kuangaliwa kwa uangalifu.

Kwa maoni ya Wizara yangu, ni busara watu binafsi wahamasishwe na ikiwezekana, wasaidiwe ili wanunue matrekta na kuyaweka vijijini na kuyakodisha kwa wakulima kibiashara. Uzoefu tuliopata kutokana na vijiji kumiliki malori na matrekta,

hautupi matumaini kwamba vijiji vitaweza kumiliki na kuendesha matrekta kwa ufanisi na kwa manufaa yanayotarajiwa.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa inaonekana kwamba maombi yalikuwa ni mengi, na yaliyokidhi mahitaji ya sifa ni manne tu.

Je, Serikali haioni kwamba inawezekana kwamba masharti yaliyopo ni magumu mno kiasi kwamba hayatekelezeki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Kipole kama kifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, masharti si magumu sana tunasema hivi, kama unataka kukopa kukarabati trekta ni lazima ulete kwanza ile karatasi ya kuonyesha trekta hili ni la aina gani, lipo wapi? na kadha wa kadha. Mengine katika masuala ya kukopa kwa kuwa hizi ni fedha za umma lazima sharti yazingatiwe. Hatuwezi kuchukua hela za umma kwa kupeana bila kufuata taratibu za fedha zilizopitishwa na Bunge. Kwa hivi tunaomba kwa usalama na uhai wa mfuko huu tufuate masharti hayo, tafadhali.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Moja ya swali nililotaka kuuliza ni hilo mwenzangu aliyeuliza. Lakini bado nasema kwa kuwa Serikali inajua kilimo ni uti wa mgongo, na kwa kuwa Serikali hiyo hiyo masharti iliyoweka ni magumu ninaomba kama ikiwezekana kwa nini isiyapitie upya ili iweze kuona urahisi wa watu wanaohitaji kilimo wakaweza kufanya hivyo? Ukizingatia haswa watu walioomba 40 na wakapewa wanne masharti magumu na mimi ni mmojawapo nayajua. Ahsante.

**SPIKA:** Sawa, sisitiza jibu lako Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Martha Wejja swali lake moja kwa kusisitiza niliyozungumzia huko nyuma.

Kwanza sisi tunayo masharti yaliyowekwa na Bunge namna ya kukopesha fedha za umma, haya tumefuata vinginevyo tutakuja kupata matatizo *queries* nyingi tu. Lakini lingine vile vile Mheshimiwa kama kweli una wazo zuri kiasi hicho tuonane mimi niko tayari kumchukua. *(Makofi)*

Na. 79

**Tatizo la Maji Nanyumbu**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ipo mito mingi jimboni Nanyumbu inayotiririsha maji mengi wakati wa kifuku na maji hayo hukauka wakati wa kiangazi; na kwa kuwa, jimbo hili hukabiliwa zaidi na uhaba wa maji majira ya kiangazi:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa ipo haja ya kuzuia maji hayo yanayopotea wakati wa kifuku ili yatumike wakati wa kiangazi?

(b) Je, Serikali ipo tayari sasa kupeleka teknolojia ya uhifadhi wa maji hayo na ufadhili jimboni Nanyumbu ili kumaliza tatizo sugu la uhaba wa maji katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ipo haja ya kuzuia maji yanayopotea wakati wa kifuku ili yatumike wakati wa kiangazi katika jimbo la Nanyumbu na hata maeneo mengine hapa nchini.

Hii ni teknolojia mbadala ya kupata maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo, kilimo na matumizi mengine badala ya vyanzo vya maji chini ya ardhi ambavyo vina gharama kubwa za uendeshaji.

Mbinu ya kuhifadhi maji ya mvua ni kwa kujenga mabwawa ya kukinga maji kwenye mito wakati wa msimu wa mvua. Aidha, ujenzi wa matanki ya kuvuna maji kutoka kwenye mapaa kwa ajili ya familia au jamii ndogo ndogo unaweza kutumika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishaanza kupeleka teknolojia ya uhifadhi wa maji ya mvua jimboni Nanyumbu kuanzia mwaka 1993, ambapo ilijenga matanki ya mfano ya kuvunia maji ya mvua kutoka katika mapaa ya nyumba. Matanki haya ya mfano yamejengwa katika kituo cha mafunzo cha Michiga, zahanati za Likokona na Mangaka, ofisi ya Kata Mangaka na shule ya msingi Mburusa. Aidha, ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua katika vijiji vya Manene na Nangoma unaendelea kufanyika kwa msaada wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, ili kuufanya mpango huu uwe endelevu, napenda kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iingize miradi ya uvunaji wa maji ya mvua katika Bajeti yake ya kila mwaka. Wananchi nao wahamasishwe kutumia teknolojia hii. Wizara yangu ipo tayari kusaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na wananchi wa jimbo la Nanyumbu katika kufanikisha matumizi ya teknolojia hiyo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mradi wa maji wa Ndwika Mangaka umekwama kumalizika kutokana na kuishiwa mabomba, na kwa kuwa miradi ya mabwawa ya Nangomba na Maneme nayo imesimama kutokana na kuishiwa fedha.

Je, Serikali itakuwa tayari kumalizia miradi hiyo ili kuwaondolea Wananchi wa maeneo hayo kero hii ya maji?

La pili, kwa kuwa kulikuwa miradi na mpango wa kujenga mabwawa katika vijiji vya Maratane, Masogo, Mpwahiya na Mpombe kwa ufadhili wa *TASAF,* na kwa kuwa survey ilikwishafanyika. Sasa ni lini mabwawa hayo yatajengwa na kumalizika ili kuwaondolea Wananchi wa maeneo hayo kero ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aridi Uledi, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Ni wajibu wa Serikali kutekeleza na kuona kwamba miradi inayoianzisha inakamilika. Kwa hiyo kwa jitihada hizo hizo ambazo Wananchi wa maeneo ambako mradi unaotekelezwa na *TASAF* wamefanya kwa kuchangia nguvu zao, pamoja na ushirikiano uliopo kati ya viongozi na uongozi wa wasimamizi wa mradi huo nina hakika kwamba mradi huo utakamilika mara fedha zitakapopatikana. Hivyo hivyo inaendana na miradi ambayo amesema bomba zimekwisha kwa sababu ya upungufu wa fedha, fedha zitakapopatikana ni hakika kwamba tungependa kuona kazi hiyo imekamilika kama ilivyopangwa. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Aridi Uledi awe na uvumilivu.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Wilaya ya Masasi ukitokea upande wa Nanyumbu ukapita Mikangaula, unaingia Jimbo la Masasi katika Kata za Masasi Magharibi na Majani na Namatutwe ambako kuna matatizo makubwa sana ya maji kama yale yaliyosemwa Nanyumbu. Ningependa kuomba Wizara

**SPIKA:** Uliza usiombe.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Niwape matumaini gani watu wa eneo hili katika kuhakikisha kwamba inasaidia kufufua mabwawa ya zamani kwa mfano kama Mpangala na kadhalika ili maji yapatikane bila wasiwasi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, eneo wanalolisema Mheshimiwa Mbunge nalifahamu na ninapenda nirudie kusema kwa vile ameuliza hapa Bungeni kwamba tutapenda tupate ushirikiano sana. Malambo au Mabwawa hayo mawili aliyoyasema yameharibika kutokana na kulimwa au shughuli za ukulima kando na hivyo yamejaa tope.

Ningependa kuwaomba sana Wananchi wote hapa nchini nikijumuisha wananchi wa Masasi, kwamba mabwawa au malambo yana masharti ya matumizi na siyo vizuri kulima kando kando au karibu sana na vyanzo vya maji yanayoingia kwenye hayo malambo. Kwa kufanya hivyo ndio sababu kubwa ambayo ilisababisha malambo mawili anayoyasema Mheshimiwa Raynald Mrope kujaa tope na hivyo kutokutumika.

Lakini ushauri wa pili ninapenda nitoe shukrani sana kwa uongozi wa Wilaya ya Misungwi. Malambo mengi sana haya madogo madogo au mabwawa madogo yanaweza kuchimbwa kwa mikono kwa kutumia Majembe, hivyo imefanyika Misungwi na wamefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo ningeomba wananchi wa Masasi pia wangeweza kufanya hivyo ili kutatua matatizo ambayo yanawapa sasa hivi ya kukosekana kwa maji. *(Makofi)*

Na. 80

**Ustawishaji Mifugo**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mifugo mingi katika Afrika, na kwa kuwa kwa muda mrefu wafugaji wa Kitanzania hawajafaidika kwa mazao yatokanayo na mifugo yao kutokana na huduma duni mfano malambo na majosho.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kustawisha mifugo yetu ili ipate soko la uhakika hasa nchi za nje?

(b) Je, kwa nini mifugo isiundiwe Bodi kama zilivyo Bodi za Mazao ya Kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na nchi yetu kuwa na ng’ombe takriban milioni 17.7, mbuzi milioni 12.5, kondoo milioni 2.5 na mifugo mingine mingi, bado wafugaji hajafaidika sana na uuzaji wa mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, ili nchi iweze kuuza mifugo na mazao yake katika masoko ya nje, ni sharti ikidhi viwango vya Kimataifa vya biashara hiyo. Tatizo kubwa linalofanya mifugo yetu isiweze kupata soko la uhakika la nje ni kuwepo kwa magonjwa ya mifugo yetu isiweze kupata soko la uhakika la nje ni kuwepo kwa magonjwa ya mifugo hususani ya milipuko yasiyo na mipaka *(Transboundary Animal Diseases).*

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine ni ukosefu wa mifugo na udhoofu wa mifugo unaosababishwa na uhaba wa maji na ukosefu wa malisho bora. Kutokuwepo kwa viwanda vya kutosha vya kusindika mazao hayo pia tatizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba panakuwepo ustawi wa kutosha kwa mifugo yetu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, imejenga na kukarabati malambo 299 na majosho 124 kuanzia mwaka 2001/2002 na 2004/2005. Katika kipindi hicho hicho Wizara imeimarisha miundombinu ya masoko, minada 56 na kukarabati mabehewa 60 ya kubeba mifugo.

Hali kadhalika Wizara imejenga machinjio ya kisasa na Chuo cha Ukataji Nyama hapa Dodoma ili kuongeza ubora wa nyama. Wizara yangu itaendelea kujenga miundombinu ya aina hiyo pamoja na mpango wa unenepeshaji wa mifugo ili kuongeza ubora wa mifugo katika maeneo kadhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Sekta binafsi kufuga kibiashara na kustawisha ufugaji, baadhi ya ranchi za *NARCO* zimegawanywa katika ranchi ndogo 49 na kumilikishwa kwa wawekezaji Watanzania Wazalendo. Wizara yangu inahimiza sana matumizi ya mbegu bora ili kuendeleza mifugo yetu.

Hivyo Kituo cha *NAIC* cha Arusha kimeimarishwa na kinaweza kuzalisha dozi 230,000 za mbegu bora kwa mwaka. Vilevile uzalishaji wa mitamba chotara unaendelea kufanyika katika mashamba ya Mabuki, *Sao Hill,* Ngerengere, Kitulo na Nangaramo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa magonjwa ya mifugo, Wizara yangu imeweza kutokomeza kabisa ugonjwa wa Sotoka na juhudi hizi zimetambuliwa rasmi na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE).*

Wizara yangu inaendeleleza juhudi kama hizo katika kutokomeza magonjwa mengine kwa mfano homa ya mapafu, kimeta, chambavu, ugonjwa wa Miguu na miundo, homa ya nguruwe, kideri na magonjwa mengine.

Kuhusu ugonjwa wa homa ya mapafu Serikali imenunua dozi milioni 13 za dawa ya chanjo zenye thamani ya shilingi milioni 910 kati ya mwaka 2003/2004 na 2004/2005 na tayari dawa hizo zimetumika huko Wilayani. Utokomezaji wa magonjwa haya utasaidia nchi yetu kuingia katika soko la kigeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakamilisha utayarishaji wa Sera ya Mifugo ambayo itazingatia maeneo yote ya kuistawisha Sekta ya Mifugo. Sera hii itatekelezwa vizuri na baadhi ya sheria tulizozipitisha hapa Bungeni hivi karibuni, yaani Sheria ya Magonjwa ya Mifugo (2003), Sheria ya Utabibu wa Mifugo (2003), Sheria ya Maziwa (2004). Sheria nyingine zinaendelea kurekebishwa kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi katika Sekta ya Mifugo.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mazao ya mifugo nayo yanastahili kuundiwa Bodi ili kusimamia na kudhibiti mazao hayo.

Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa maziwa inatarajia kuunda Bodi ya Maziwa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Maziwa (2004). Bodi za mazao mengine kwa mfano nyama na ngozi, nazo zitaundwa baada ya kupitishwa kwa Sheria zinazosimamia mazao hayo. Wizara yangu iko katika hatua mbalimbali za kurekebisha Sheria hizo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa mara nyingi Serikali husisitiza zaidi mazao ya mifugo kama maziwa na nyama peke yake bila kuzungumzia zao la mifugo kama ngozi na Mifupa.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa suala la ngozi na mifupa kwa sababu na lenyewe ni zao la mifugo?

Kwa kuwa kuna fedha ambazo zinatumika kwenye Wizara ya Mifugo lakini zinapitia Wizara ya Kilimo. Kwa nini Serikali inaona kigugumizi kuhamisha hizo fedha kutoka Wizara ya Kilimo ziende Wizara Mifugo kwa sababu Rais alishatenganisha kilimo na mifugo, mifugo ni Wizara ya peke yake. Kwa nini wanaona kigugumizi mpaka leo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucas Selelii, lenye sehemu mbili kama ifuatavyo:-

Tunaposisitiza unywaji wa maziwa au ulaji wanyama, hiyo misisitizo haiwezi kufanikiwa kama hakuna mahitajio. Kwa hiyo shughuli yote ya ufugaji, shughuli yote ya mazao ya mifugo inaongozwa na mahitajio na upatikanaji au *demand na supply.*

Kwa hiyo, kama kuna *demand* ya mifupa na kuna *demand* ya ngozi ambayo nina hakika ipo na biashahara hiyo imeshamili sana. Nina hakika kwamba mazao hayo pia yatapata wanunuzi na Wananchi watafaidika kutokana na mauzo ya mazao hayo.

Hili suala la pili ambalo ameliuliza Serikali inalifanyia kazi na mambo mengi sana tayari yameshahamishiwa Wizarani kwetu. Kwa hiyo, yamebaki maeneo madogo madogo ambayo pia tunayafanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara hizo mbili.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara hii kwa uhakika sasa wanao mwelekeo sahihi na mzuri wa ufugaji wa uendezaji wa ng’ombe, na kwa kuwa katika majibu ya Waziri mwenyewe amekiri na kuonyesha kwamba wanatambua matatizo yanayotufanya tusiingie katika soko la uuzaji wa nyama nchi za nje.

Je, kwa kuwa kutambua tatizo ni busara na ni jambo zuri Waziri anaweza akatusisitiziaje sasa kwamba kuna mpango gani ambao ungetuwezesha kuvuna ng’ombe waliopo hivi sasa kuliko hata kuangaika na kuboresha ng’ombe wengine?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kama ifuatavyo:-

Mpango mmojawapo tulionao wa Wizara ni mpango ambao Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya yeye mwenyewe anaufanya sasa hivi, baada ya kumpatia shamba lililokuwa mali ya Serikali.

Sasa hivi analitumia kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa mifugo na uchinjaji wa nyama ambayo nina hakika soko lake ameshalitafuta na itakuwa ni faida kubwa sana kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kupitia Bunge lako Tukufu ningependa Waheshimiwa Wabunge wengine.

Nina hakika wengi pia mnafahamu taarifa zao kwamba wameanza kuingia kwenye biashara hii. Itasaidia sana kuhamasisha uzalishaji wa mifugo na kuwezesha wakulima au wafugaji wetu kujipatia kipato. Kwa hiyo, napenda niseme kwamba Serikali inasisitiza kwamba biashara hii ina faida kwa wote ambao wanahusika na biashara hii au ufugaji wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, pili, matatizo kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi ya magonjwa, yanatokana pia na tabia yetu ya ufugaji wa kutozingatia masharti. Ndio maana nimeeleza kwamba kuna baadhi ya sheria itabidi tuzirekebishe ili wananchi ambao wanavunja masharti ya kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine washughulikiwe kwa sababu inasababisha nchi ipate magonjwa na hivyo kutupotezea soko la mazao ya mifugo yetu nchi za nje. Kwa hiyo, napenda nihimize kwamba tushirikiane kama tulivyoanza na nina hakika tutafikia kiwango ambacho Mheshimiwa Mzindakaya angependa tufikie.

Na. 81

**Umeme - Songwa**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika mji wa *Songwa Railway Station* ulioko katika Kata ya Songwa, Tarafa ya Mondo?

(b) Kwa kuwa, kijiji cha Mwigumbi kilichopo Kata ya Mondo kiko karibu na kijiji cha Songwa ambacho kina umeme. Je, isingekuwa vema kijiji hicho nacho kikapatiwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ng'wala Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

(a) Ili kukipatia umeme kijiji cha Songwa Stesheni, inahitajika ujenzi wa laini ya kilovoti 33 umbali wa kilomita 1.5 pamoja na kusimamisha au kujenga *transforma* moja yenye ukubwa wa *100kVA;* na ujenzi wa laini ndogo za usambazaji umeme umbali wa kilomita 3. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi 29 milioni.

Mheshimiwa Spika, kijiji hiki ni kati ya vijiji vya Mkoa wa Shinyanga ambavyo vimependekezwa kupatiwa umeme katika programu ya umeme vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, kijiji cha Mwigumbi kipo umbali wa kilomita kama 13 kutoka sehemu ulipo umeme kwa hivi sasa. Jumla ya shilingi 179 milioni zihitajika ili kukipatia umeme kijiji hiki.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huu kama ilivyoonyeshwa ni kubwa kidogo lakini tunaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa laini ya umeme inayotoka Maganzo kwenda Songwa *Health Center* na kutoka sehemu hiyo ni robo kilometa kufika katika eneo ambalo nimelitaja la *Songwa Railway Station.* Sasa je, Serikali inaona ugumu gani kumalizia sehemu ambayo ni kama robo kilometa tu kutoka ambako umeme umepita? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Makolo na wananchi wa sehemu yake kwamba Serikali haioni ugumu kutekeleza mradi huo kwa maana aliyoisema. Katika kusambaza umeme huwa kunakuwa na kazi ya awali ya kutathmini maeneo ya kupita umeme na kuzingatia mambo mbalimbali na ndio maana wakati najibu swali nilisema kwamba gharama ziko kama Sh.29 milioni na imewekwa katika programu ya utekelezaji. Kwa hiyo, ningependa nichukue nafasi hii kuwahakikishia wananchi wa eneo husika kwamba Mheshimiwa Mbunge amelifikisha suala hili na linafanyiwa kazi na limewekwa katika programu ya umeme vijijini.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa mahitaji ya umeme ni ya nchi nzima pamoja na Mkoa wa Singida na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba ingeweza kupeleka umeme Tarafa ya Ihanja kabla ya

Uchaguzi Mkuu kufika. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hili maana tarehe zinakwenda?

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya lakini Naibu Waziri kama unayo majibu unaweza kuyatoa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema mahitaji ya umeme ni ya nchi nzima na kwa kuzingatia umuhimu wa umeme ndio maana juzi tu hapa tumepitisha Sheria ya Wakala na Mfuko wa Umeme vijijini ili kuhimiza kazi hii muhimu na kazi hii kubwa inayohitajika nchi nzima.

Kuhusu umeme wa Ihanja, napenda nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Mbunge wa eneo hili, Mheshimiwa Missanga amelishughulikia sana suala hili na sisi tumemuahidi kwamba tutajitahidi kadri iwezekanavyo umeme huu ufike hasa kwenye Shule ya Sekondari ya Ihanja.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa mradi huu kama nilivyosema awali kwa kweli kunatokana na matatizo ya fedha tu na wala sio lingine.

Lakini napenda nisisitize kwamba ndio maana basi sasa tumekuja na programu nzuri na nzito hii ya kusambaza umeme vijijini na kama nilivyosema juzi wakati tunawasilisha Muswada kwamba umeme sasa unakuwa sekta mtambuka ambayo itakwenda kuhudumia maeneo mbalimbali ya afya, elimu, mawasiliano na kadhalika.

Na. 82

**Mita za Mafuta kwenye Vituo vya Mafuta**

**MHE. KHADIJA S. NGOZI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Ugavi wa Umeme *TANESCO* limejiwekea utaratibu wa kukata umeme kila linapotaka kufanya hivyo:-

(a) Je, ni sababu gani zinazotumiwa na Shirika hilo kukata umeme?

(b) Kwa kuwa watakaokatiwa huduma hiyo ni wateja na wanayo haki ya kupata taarifa ya kusitishwa kwa huduma hiyo kabla ya kufanya hivyo, je, wateja hao huarifiwaje kwa muda muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, kama ifuatavyo:-

(a) Sababu zinazofanya Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini *TANESCO* kuwakatia wateja wake umeme ni nyingi na nimeziorodhesha na kwa kuwa jibu ni refu sana tutampatia Mheshimiwa Mbunge ili kuokoa muda. Lakini kwa uchache tu ni pamoja na:-

1. Iwapo mteja hajalipia ankara *(bill)* yake ya umeme;

2. Iwapo mteja atagundulika anaiba umeme kwa njia yeyote ile;

3. Iwapo mteja atagundulika anawapatia umeme jirani zake bila mkataba wowote;

4. Iwapo mteja atagundulika hakuunganishiwa umeme kwa njia halali;

5. Iwapo mteja atajiunganishia umeme kwa sababu mojawapo ya hizo zilizotajwa hapo juu;

6. Iwapo wakati wa ukaguzi wa kawaida itagundulika kuwa mtandao wa umeme wa ndani ya nyumba au kiwanda cha mteja sio salama;

7. Iwapo mteja atafunga kifaa chochote kwenye nguzo ya Shirika au katika laini za umeme za Shirika bila makubaliano yoyote na Shirika;

8. Iwapo mteja atadanganya shirika na kuwekwa pamoja na kulipishwa umeme ataotumia katika kiwango *(tariff cat egory)* ambayo hustahili *(wrong tariff);*

9. Iwapo mteja atagundulika kuwa ameongeza vifaa vingi sana vinavyotumia umeme bila kulifahamisha Shirika ili likague upya mtandao wa umeme na hivyo kusababisha mita pamoja na waya za Shirika kuelemewa *(overload);*

10. Iwapo mteja atawakatalia wafanyakazi wa *TANESCO* kuingia ndani ya eneo lake kwa madhumuni ya kufanya kazi;

11. Iwapo mteja atatumia kifaa ambacho anajua wazi kinaweza kusababisha wateja wengine waliounganishwa katika laini hiyo kuathirika kwa kupata umeme usio bora;

12. Iwapo mteja atakutwa amepanua nyumba au kiwanja au amejenga ukuta au chochote kile kiasi kwamba ongezeko hilo liko chini ya waya za umeme au ndani ya upana unaohitajika kuwa wazi kwa ajili ya kupitisha nyaya za umeme;

13. Iwapo mteja ataendeleza ujenzi mahali mita ilipofungwa na kusababisha mita kuwa katika sehemu ambayo ni mbali kufikia mfano chumba cha kulala au kufanya mita iwe katika mazingira yasiyoridhisha mfano sehemu yenye vumbi sana, unyevunyevu mwingi au moshi.

(b) Zifuatazo ni taratibu zinazotumika kuwaarifu wateja kabla ya kuwakatia umeme. Kimsingi, ni kwamba sababu inayopelekea kukatiwa umeme ndio yenyewe pia inayochangia inachukua muda gani na taratibu gani za kumfahamisha mteja ili kuweza kumkatia umeme na kuweza kurejeshewa umeme. Sababu hizi au utaratibu huu umeelezwa kwa kirefu kama nilivyosema awali na tutampatia Mheshimiwa Mbunge.

Lakini kutoa mfano mmoja kwamba mteja ambaye hajalipa ankara, kila mteja huandikiwa katika ankara yake kuwa kama hajalipa ndani ya siku 21 kwa mfano atakatiwa umeme wakati wowote ule.

Pia *TANESCO* huchukua taratibu za kutangaza mara kwa mara katika vyombo vya habari kuwa wateja walipie ankara zao la sivyo *TANESCO* itawakatia umeme.

Hivi sasa kwa mfano kuna *operation* kubwa ambayo *TANESCO* inaendesha ya kukusanya madeni na kwa ajili hiyo wale ambao hawajalipa madeni yao huenda wakakatiwa umeme wakati wowote. Napenda nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wateja wote ambao hawajalipa ankara za umeme za *TANESCO* waende haraka kwenye vituo vya *TANESCO* kulipia ili kuondoa usumbufu ambao unaweza kutokana na kukatiwa umeme.

**SPIKA:** Pamoja na kumpatia Mheshimiwa Mbunge muuliza swali, Hansard itachapisha maelezo yote kwa ukamilifu ili yawasaidie Wabunge wengine wote. *(Makofi)*

Na. 83

**Upungufu wa Walimu wa Shule za Sekondari na za Msingi**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa hadi leo tatizo la upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari ni kubwa licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu katika kumaliza tatizo hilo, kwa mfano Wilaya ya Korogwe peke yake ina upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi wapatao 300 na Walimu wa Shule za Sekondari zaidi ya 36 katika masomo mbalimbali; na kwa kuwa, Serikali imekubali kuwaajiri Walimu-wanafunzi wanaochukua mafunzo ya mwaka mmoja chuoni na mwaka wa pili kazaini *(on job training),* na mpango huo umesaidia sana kuziba mapengo yaliyo wazi kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari:-

(a) Je, Serikali haioni ni busara pia kuwaajiri Walimu wengi wa Daraja la IIIA waliomaliza mafunzo yao ya miaka miwili katika vyuo vyetu badala ya kuwaacha Walimu hao wakizagaa tu mitaani bila kazi wakisubiri matangazo ya kazi ya Ualimu toka kwenye Halmashauri mbalimbali hali Serikali inatambua kuwepo kwa upungufu mkubwa wa Walimu nchini?

(b) Kwa kuwa utafiti umeonyesha kwamba shule za mjini zina Walimu wengi ikilinganishwa na shule za vijijini. Je, Serikali ina mikakati gani ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ambalo sasa limezidi kushamiri?

(c) Kwa kuwa Korogwe inalo tatizo sugu la upungufu wa Walimu kwa shule hizo. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuziba pengo hilo katika Wilaya hiyo na kwa Wilaya nyingine zenye upungufu huo kote nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kablda ya kujibu swali la Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, napenda kutoa utangulizi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, imeweka mikakati ya kuajiri Walimu wa kutosha wa Shule za Msingi na Sekondari. Lakini kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi chini ya mipango hiyo na kwa kuwa Walimu lazima kwanza wapewe mafunzo ya Ualimu ndipo waajiriwe, itakuwa hadi mwishoni mwa mipango hiyo ndipo tutakuwa na Walimu wa kutosha katika Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kusikia Mheshimiwa Mbunge akitaja baadhi ya mafanikio ya MMEM kwamba zoezi hilo limesaidia kuziba mapengo yaliyokuwa wazi kwa Walimu wa Shule za Msingi na nina imani MMES pia utasaidia kuondoa tatizo la Walimu wa Shule za Sekondari nchini, hasa baada ya *Mkwawa High School* na Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam kubadilishwa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia baadaye mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mwalimu yeyote mwenye Cheti cha Ualimu Daraja la IIIA hana haja ya kuzagaa mitaani bali atume maombi ya ajira ama kwa Halmashauri za Miji, Jiji na Manispaa wanaotangaza nafasi; au kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu ambaye atampanga kwenye Halmashauri iliyo na nafasi.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la mrundikano wa Walimu mijini limekwishatafutiwa ufumbuzi kwa njia ya Waraka wa Elimu Na.4 wa mwaka 2001. Waraka huo unahusu kuondoa mlundikano wa Walimu mjini ambao pamoja na masuala mengine uliwahimiza Maafisa wanaosimamia Shule za Msingi kuwapanga Walimu kufuatana na ikama. Aidha katika mgao wa nafasi za ajira mpya Halmashauri za Miji, Jiji na Manispaa zimekuwa zikipewa nafasi chache ikilinganishwa na Halmashauri za Wilaya. Kila Mwalimu anapoajiriwa huwa anasaini mkataba wa kutumikia Halmashauri iliyompa ajira kwa kipindi cha miaka mitatu bila kuomba uhamisho.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia MMEM na MMES inaendelea kuajiri Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari na hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe itapatiwa Walimu kulingana na uwiano na upungufu wa Walimu nchini na kadri Walimu

wapya wanapohitimu mafunzo ya Ualimu. Inategemewa ifikapo mwishoni mwa MMEM mwaka 2006 tatizo hili litakuwa limekwisha kabisa.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kwamba bado tatizo la Walimu lipo na ni hivi karibuni tu Wizara katika kusaidia kuziba pengo hilo wamejaza Walimu-wanafunzi wengi katika vyuo vingi nchini kwetu lakini kwa sababu ambazo mimi sifahamu na wananchi wangependa wafahamu, idadi ile ambayo wamesahiliwa katika vyuo hivyo ilikuwa kubwa lakini juzi juzi hapa wamewapunguza. Sasa nataka kufahamu na wananchi wanataka kufahamu ni kwa sababu gani wanafunzi-walimu wale waliokwenda katika vyuo wamekwenda shuleni na wakarudishwa wengi tu na yako malalamiko hayo na wazazi wanalalamika, ni kwa sababu zipi, naomba nifahamu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna Walimu ambao walirejeshwa vyuoni na sababu zilizosababisha kufikia hapo ni kama ifuatavyo:-

Walimu hawa wanapotakiwa kwenda chuoni wanapewa barua za uteuzi na kuna wengine ambao wanapewa barua za akiba. Sasa ilijitokeza kwamba wengine ambao walipata barua za akiba walijipeleka moja kwa moja kwamba nitasubiria huko huko. Sasa huo sio utaratibu, hawa walirejeshwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna ambao walikwenda wakashindwa ile *qualifying test.* Pamoja na shida yetu ya Walimu, tusingependa tuchukue tu kila mtu hata kama tunajua huyu baada ya mafunzo yake ya Ualimu hatakuwa Mwalimu mzuri. Kwa hiyo, wale ambao walishindwa *qualifying test,* samahani sio *Kiswanglish* ilibidi nao warejeshwe.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna wengine mamluki waliripoti na vyeti bandia, jina la cheti ni Mudhihir, lakini mwenyewe ni Athuman, hao nao walirejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara atatoa mtihani mwingine watakaoshindwa mtihani huo nao tutawarejesha lakini tunatoa mtihani huo ili tuweze kuona kama tunaweza tukapata vijana wengine ili pengo hili la Walimu liweze kuzibika kwa urahisi.

Na. 84

**Matatizo katika Sekondari za Serikali - Mpanda**

**MHE. LEPHY B. GEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekondari za Serikali zilizoko Jimboni Mpanda zikiwemo *Mpanda Girls* na Mwangaza zinakabiliwa na matatizo kadhaa ambayo yameshawasilishwa Serikalini lakini hadi sasa hakuna tatizo hata moja kati ya hayo limeshashughulikiwa:-

Je, ni lini Serikali itayashughulikia matatizo hayo katika Sekondari hizo kwani inayafahamu vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lephy Benjamin Gembe, Mbunge wa Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Mpanda, yaliyowasilishwa Wizarani yameshughulikiwa yote kama ifuatavyoo:-

(i) Ombi la kwanza la kuanzisha Kidato cha 5 lililowasilishwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa kwa barua Kumb.Na.RR.1/1/9025/15 ya tarehe 8/11/2001 na Wizara yangu ililijibu kwa barua Kumb.Na.SYCA/178/446/01/55 ya tarehe 7/12/2001 kuwa mpango wa kuongezewa nafasi za Kidato cha 5 na Kidato cha 6 katika shule hiyo upo katika MMES 2004/2009.

Aidha Mkuu wa Mkoa alikumbushia tena ombi hilo kwa barua Kumb.Na.RR./E.40/5/99 ya tarehe 31 Mei, 2004. Utekelezaji wa ombi hilo umeanza kwa kuteua wanafunzi 50 wa kuanza Kidato cha 5 mwezi huu wa Aprili, 2005. *(Makofi)*

(ii) Ombi la pili la kuruhusiwa wanafunzi 24 wa kutwa kuhamia hosteli, lilikubaliwa kwa barua Kumb.Na.SYCA/178/446/01/50 ya tarehe 8 Machi, 2004.

(iii) Ombi la tatu ukarabati wa majengo ya shule, limetekelezwa kwa Wizara yangu kupeleka Sh.70,00,000/= kutokana na fedha za MMES kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya nyaya za umeme shuleni hapo.

(iv) Ombi la nne la uongozi mbovu, limeshughulikiwa kwa kubadilisha uongozi.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Shule ya Sekondari ya Mwangaza yaliyowasilishwa ni ya ukarabati wa madarasa na uongozi mbovu wa shule hiyo. Fedha kwa ajili ya ukarabati bado hazijapatikana lakini Sh. 9,000,000/= zimepelekwa shuleni hapo kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa nyumba ya Mwalimu. Fedha hiyo ikisimamiwa vizuri itaweza pia kufanya ukarabati wa madarasa unaokisiwa kuhitaji Sh.3,000,000/=.

Kuhusu tatizo la uongozi shuleni hapo, Wizara yangu imeshachukua hatua za kubadilisha uongozi uliokuwepo. Endapo Mheshimiwa Mbunge anayafahamu matatizo mengine ambayo anaona hayajafanyiwa kazi, tunamwomba ayalete ili nayo tuweze kuangalia namna ya kuyashughulikia kulingana na uwezo uliopo.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwanza nimshukuru tu kwa kweli kwa yale yote ambayo yameshughulikiwa lakini bado nina matatizo ya ubovu wa vyoo, ubovu wa gari zote mbili Mwangaza na *Mpanda Girls* lakini vile vile kuna ubovu wa *generators* ambazo ziko katika shule ya *Mpanda Girls.* Kwa hiyo, naomba hayo nayo yashughulikiwe.

**SPIKA:** Hilo ni ombi sio swali kwa hiyo huna haja ya kulijibu, tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ujenzi.

Na. 85

**Ujenzi wa Barabara Wilayani Ukerewe**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ni muhimu sana katika kukuza uchumi kupitia kwa wananchi waishio vijijini na kwa kuwa hakuna mawasiliano yoyote kutoka Rugenzi, Nansio, Malegea, Mahande, Igalla, Rubya, Bukondo hadi Masonga na barabara ya Rugezi, Nansio, Murutunguru, Kamanye, Bukondo hadi Masonga Wilayani Ukerewe:-

Je, ni lini barabara hizo zitatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyotajwa vinapitiwa na barabara mbili, ya kwanza inapitia vijiji vya Rugezi, Nansio, Bukongo, Murutunguru, Bukonyo hadi Masonga yenye urefu wa kilometa 45.4 na ya pili inapitia vijiji vya Bukongo, Malegea, Mahande, Igalla, Rubya hadi Bukonyo yenye urefu wa kilometa 40.3. Barabara hizo ni za Mkoa chini ya Wizara ya Ujenzi na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mwanza. Kwa kujua umuhimu wa mawasiliano ya barabara katika kukuza uchumi kupitia kwa wananchi waishio vijijini, Wizara yangu imekuwa ikizifanyia matengenezo barabara hizo zilizopo Wilaya ya Ukerewe Mkoani Mwanza kulingana na upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2003/2004 barabara ya Rugezi - Nansio - Murutunguru - Bukonyo - Masonga ilifanyiwa matengenezo kwa kiwango cha

changarawe kati ya Bukongo hadi Murutunguru kilometa 9.0 na jumla ya shilingi 93.920 milioni zilitumika kugharamia matengenezo hayo.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2004/2005 jumla ya shilingi 1.013 bilioni zitatumika kugharamia matengenezo mbalimbali ya barabara za Mkoa zilizopo Wilayani Ukerewe kama ifuatavyo:-

Barabara ya Nansio - Murutunguru - Bukonyo hadi Masonga matengenezo yanaendelea kama ifuatavyo:-

Matengenezo ya kawaida *(Routine Maintenance)* kutoka Rugezi hadi Murutunguru, jumla ya kilometa 21.0 yamekamilika kwa gharama ya shilingi 21.0 milioni.

Katika barabara hiyo pia, kipande cha kilometa 6.0 kutoka Nansio hadi Bulamba kipo kwenye matengenezo makubwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia teknolojia mpya ya *Otta seal.* Kazi ya kujenga lami nyepesi *Otta seal* imegawanyika katika sehemu tatu. Ya kwanza inahusisha kilometa 4.0 na jumla ya shilingi 472.585 milioni zitatumika kukamilisha kazi hiyo. Sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa mitaro ya maji kwa gharama ya shilingi 149.9 milioni. Sehemu ya tatu inahusisha ujenzi wa kilometa 2.0 ambapo jumla ya shilingi 178.782 milioni zitatumika kugharamia kazi hiyo. Kazi hizo zote tatu Wakandarasi wapo kazini wanaendelea na ujenzi na kazi zinategemewa kukamilika katika mwaka huu wa fedha 2004/2005.

Aidha, Daraja la Mlyogwezi lililofunga barabara hiyo limefanyiwa matengenezo makubwa *(major repair)* kazi hii imekamilika na kiasi cha shilingi 24.999 milioni zimetumika.

Barabara ya Bukongo, Malegea, Mahande, Igalla, Rubya hadi Bukonyo iliyokuwa inatishia kujifunga nayo inafanyiwa matengenezo kwa awamu ili iweze kufunguka. Awamu ya kwanza inahusisha matengenezo ya kilometa 8.0 kuanzia Bukongo hadi Mahande, kazi hii inakaribia kukamilika na jumla ya shilingi milioni 68.188 milioni zitatumika kugharamia kazi hizo. Awamu ya pili inahusisha kilometa 6.0 kutoka Mahande hadi Lutale, utekelezaji wa kazi unakaribia kukamilika na jumla ya shilingi 47.446 milioni zimekadiriwa kutumika kugharamia matengenezo hayo.

Awamu ya tatu itahusisha kilometa 8.0 kuanzia Lutale hadi Bokondo. Kazi hii Mkandarasi ameshateuliwa na ameshaanza maandalizi ya kazi yaani *mobilization* na jumla ya shilingi 50.1 milioni zitatumika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kadri bajeti itakavyoruhusu kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizi na hasa Ukerewe.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo tu pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri eneo walilosema kwamba wameweka kokoto na mimi bahati nzuri nimetoka juzi kule ni mchanga mwingi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni umuhimu ukizingatia Jimbo hili la Ukerewe hasa Wilaya ya Ukerewe, Spika wa Bunge hili Tukufu na Mbunge wa Bunge hili akiwa pia ni Rais wa Bunge la Afrika - wkote wawili wametoka kule, tukawapa umuhimu wa kuweka lami katika maeneo hayo niliyoyataja pamoja na kuzingatia gharama. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Tunakushukuru kwa kutupigia debe. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Sehemu hiyo anayoizungumzia Mheshimiwa Nyawazwa siyo yeye tu aliyelalamikia. Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe *(DC)* alipiga simu kulalamika juu ya sehemu hiyo na tulipata habari tukamwelekeza *Regional Manager* aende akaangalie Mkandarasi anafanya nini na nitakapopata jibu, nitawasiliana na Mheshimiwa Nyawazwa.

Na. 86

**Ukarabati wa Barabara Wilayani Ngara**

**MHE. GWASSA ANGUS SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya kwanza Wilayani Ngara yenye urefu wa km.120 (iliyo chini ya *TANROAD* Mkoa) kutoka Nyakahura kupitia Keza, Rulenge, Murugaroma hadi Makao Makuu ya Wilaya huhudumia Tarafa tatu za Murugagamba, Rulenge na Kamazi kupitia Kata za Murusagamba, Keza, Rulenge, Mbuba, Kamazi na Kabanga zenye taasisi na asasi nyingi zikiwemo shule, zahanati, vituo vya afya, vituo vya biashara na Makanisa, imesahaulika kwa zaidi ya miaka kumi (10) tangu barabara ya lami ya Nyakasanza, Ngara Mjini kwenda Burundi ilipojengwa:-

(a) Je, barabara hiyo muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Ngara imetengewa shilingi ngapi kwa mwaka wa fedha 2004/2005?

(b) Je, Serikali inatambua kuwa hiyo ni sehemu ya barabara ya ulinzi Wilayani Ngara, kwani imo katika ukanda wa mapori na kambi za Wakimbizi na kutoikarabati kunahatarisha usalama wa raia na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nyakahura kupitia Kumubuga - Keza - Rulenge - Murugarama hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara ina jumla ya urefu wa kilometa 106, ambapo kati ya hizo kilometa 86 toka Nyakahura - Kumubuga - Keza - Rulenge - Murugarama ni za changarawe na kilometa 20 toka Murugarama hadi Ngara Mjini ni za kiwango cha lami.

Wizara yangu inatambua umuhimu wa barabara hii na imekuwa ikiifanyia matengenezo kila mara kupitia ofisi ya Mhandisi wa Mkoa hapo zamani na sasa Wakala wa Barabara Mkoani Kagera kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2001/2002 barabara hii ilifanyiwa matengenezo makubwa kupitia mradi wa KAROM *(Kagera Road Maintenance)*. Matengenezo hayo yaligharimu jumla ya shilingi 221.5 milioni. Mradi huo ulifadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Tanzania. Aidha, baada ya matengenezo hayo makubwa, barabara hii imeendelea kupata matengenezo ya kawaida kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2001/2002 ilipata matengenezo ya kawaida yaliyogharimu shilingi 16.52 milioni.

- Mwaka 2002/2003 ilipata matengenezo ya kawaida yaliyogharimu shilingi 26.6 milioni.

- Mwaka 2003/2004 ilipata matengenezo ya kawaida yaliyogharimu shilingi 13.05 milioni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kwa ufupi kabisa kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali imetenga jumla ya shilingi 35.25 milioni ili kuendelea kuifanyia matengenezo ya kawaida barabara hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii si kwa ajili ya ulinzi pekee, bali kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya wananchi wa eneo hilo. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imekuwa ikiihudumia barabara hii pamoja na barabara nyingine zilizoko katika eneo hilo.

Aidha, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili ipitike bila taabu na hivyo kuwahakikishia usalama raia na mali zao.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa matengenezo anayoyataja Mheshimiwa Naibu Waziri yalikuwa yanaanzia Murugarama - Rulenge na eneo la kutoa Rulenge - Kumubuga limekuwa halipati matengenezo kwa muda mrefu ambalo ndilo eneo kubwa na ndilo linalopita

katikati ya vijiji vinavyozalisha. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufika na kutazama hicho ninachokisema kwamba ni kweli?

(b) Katika hali kamili iliyopo Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kukubali kwamba eneo lililotengenezwa sasa hivi limeharibika zaidi kwa sababu ya mvua nyingi na hivyo linahitaji kufanyiwa kazi ili kusaidia kusomba mazao ya pamba na tumbaku ambayo vimelela vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama utakavyoona katika jibu langu la msingi nimesema Wizara inapeleka pesa za matengenezo ya kawaida. Sasa ni maamuzi ya bodi, maamuzi ya kule kule pesa zile zitengeneze kuanzia wapi hadi wapi. Sisi huku Wizarani hatupangi tena barabara hiyo ianzie wapi ili mradi tunapeleka pesa.

Kwa bahati mbaya sana na hili niombe kabisa kwa bahati mbaya sana Wabunge hawapati nafasi ya kushiriki kwenye *Board,* kwenye vikao vya *Board.* Kwa hiyo maamuzi ya pesa hizi zinatengeneza sehemu gani zinakuwa ni maamuzi yaliyokwisha fanywa wakati Wabunge wanafuatilia. Sasa nitoe mwito tu kwamba Mwenyekiti wa *Board* ya barabara ambaye ni Mkuu wa Mkoa na Katibu wa *Board* ya Barabara ambaye ni *Regional Manager* wahakikishe vikao vinakaa wakati Wabunge hawapo Bungeni ili Wabunge washiriki na baadaye uamuzi utoke. Tumekwisha toa taarifa hii rasmi kwa maandishi kwa wakubwa hawa ila hili nasisitiza tu ili muweze kushiriki na hii ndiyo itasaidia kuona barabara ya Bugalama mpaka Lulenge ndiyo inayotengenezwa na kwingine hakutengenezwi haya ni maamuzi ya kulekule sisi tunatoa pesa na ninaamini kabisa Waheshimiwa Wabunge mmepata taarifa za pesa nyingi kabisa tumegawa sasa hivi. Kwa hiyo, lazima zitumike huko kwa mpangilio mmaokubaliana. *(Makofi)*

Na. 87

**Daraja la Mto Nyikonga**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeifanyia matengenezo makubwa barabara ya Ushirombo - Buselesele ili kuboresha mawasiliano kwa wananchi wa Mikoa ya Shinyanga na Mwanza; na kwa kuwa tatizo kubwa linalokwimisha kazi hiyo nzuri iliyofanywa na Serikali ni kutojengwa kwa daraja lililopo katika Mto Nyikonga:-

(a) Je, Serikali iko tayari kulijenga daraja hilo ili kuimarisha kazi nzuri iliyofanyika na kuondoa kero kwa wananchi ya kutotumika kwa daraja hilo wakati wa masika?

(b) Je, kama Serikali iko tayari, itaanza lini ujenzi huo na utagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ushirombo - Buselesele, yenye urefu wa kilometa 59.5 ni barabara ya Halmashauri za Wilaya ya Bukombe yenye sehemu ya km.32.6 na Wilaya ya Geita yanye sehemu ya km.26.9. Kutokana na umuhimu wa mawasiliano ya barabara hiyo kiuchumi na kijamii kati ya Wilaya hizo mbili, Wizara ya Ujenzi imetenga jumla ya shilingi milioni 108 katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Aidha, Serikali imefanya matengenezo makubwa barabara ya Ushirombo - Buselesele, hasa sehemu ya Ushirombo hadi Mto Nyikonga katika mwaka huu wa fedha na hivyo kuboresha mawasiliano kwa wananchi wa Mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa kwa sasa ni kutopitika kwa barabara hiyo wakati wa masika kwenye sehemu ya bonde la Mto Nyikonga lenye urefu wa meta 170. Ili kuondoa kero hiyo kwa wananchi, Serikali inatafuta fedha za kujenga daraja katika mto Nyikonga, kuinua tuta katika bonde la mto huo na kufunga makalvati ili magari yaweze kupita kwa usalama wakati wote. Kazi hizo zitaanza mara fedha zitakapopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa samahani muda wa maswali umekwisha kwa hiyo hifadhi swali lako la nyongeza. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea kama kawaida kuna taarifa za Vikao vya Kamati. Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mwenyekiti wake anaomba Kikao kifanyike leo tarehe 20 Aprili, 2005 Chumba Namba 227 kuanzia saa 5.00 asubuhi hii.

Kamati ya pili, zipo mbili tu, nayo ni ya Miundombinu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Mgombelo, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 7.00 mchana, katika Ukumbi Namba 231 ghorofa ya pili kwa ajili ya kukutana na ujumbe wa Shirika la Posta Tanzania.

Mwisho wa matangazo ya Kamati na sina matangazo mengine ila ni kuhusu ratiba, niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba Muswada uliopo kwenye *Order Paper* ya leo umepangwa umalizike leo hii ili kusudi kesho tuingie kwenye Maazimio ya Serikali. Kwa hiyo, tujue tu hivyo kama ndiyo ratiba ya leo.

Tunaendelea na *Order Paper* Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao Yaliyowekwa kwenye Maghala wa Mwaka 2005
***(The Warehouse Receipts Bill, 2005)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu, lakini kabla ya hapo kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Mkutano huu wa Bunge nitoe na mimi rambirambi zangu nyingi kwa familia ya Marehemu Mabalozi, Balozi Bomani pamoja na mwenzetu Balozi Diria.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hapo niende kwenye Muswada wenyewe na kwanza ningependa kweli niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa kuleta Muswada huu na mimi niseme kwamba Muswada umekuja kwa muda muafaka. *(Makofi)*

Bila kusahau niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzuri wa Muswada huu ni tofauti na Miswada mingine ambayo tumeiona, ni Muswada ambao umekuja lakini umekuja kwa mpango ambao umeshajaribiwa. Kwa hiyo, mpango huu ulikwisha jaribiwa na mafanikio yake yameshaonekana kilichokuwa kinabaki ni kutunga sheria ambayo sasa itaweza kuelekeza majukumu ya wote ambao watashughulika katika kuitekeleza sheria hiyo.

Miswada mingine kama tunavyojua mara nyingine huja kitu ambacho hatujaona hata faida yake au hakijajaribiwa lakini kwa Muswada huu niseme moja kwa moja kwamba kwa kweli kama tulivyoelezwa kwenye semina wiki iliyopita tumeona mafanikio ya mpango huu wa kubadilishana Stakabadhi katika suala zima la ununuzi na uuzaji wa bidhaa za kilimo. Kwa hiyo, napongeza na kwa sababu tumeona kwamba umejaribiwa na umefanikiwa sioni kwa nini baada ya sheria kuwepo tusione mafanikio yake makubwa na ninasema hivyo kwa sababu kilichokuwa kinawaogopesha wale wote wanaohusika wadau kwenye suala zima hili ilikuwa ni sheria na kwa sasa sheria kwa sababu ipo Mabenki na wale *Warehouse Operators* na wanunuzi hawa wakopaji watakuwa wananalindwa na sheria. Tumeona vilevile faida za mpango huu, zimeelezwa na sina sababu ya kurudia faida kwa mkulima au Vyama vya Ushirika au Vikundi vya Wakulima kama wakopaji, faida kwa mkopeshaji kwa maana ya zile Benki ambazo zitakuwa zinatoa mikopo na kwa kweli faida kwa watu au makampuni yanayaouza bidhaa hizi nje ya nchi. Faida hizi ni nyingi na zimeelezwa na mimi sina haja ya kurudia kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mkakati wa kukuza Sekta ya Kilimo katika nchi hii *Agricultural Sector Development Strategy* imeeleza bayana kwamba tatizo kubwa la ukuaji wa kilimo katika nchi hii ni ukosefu wa motisha katika Sekta Binafsi kuweza kuingia kwenye biashara na shughuli za kilimo kwa ujumla kwani faida zake zilikuwa hazionekani vizuri. Lakini vilevile tumeona matatizo makubwa ambayo wakulima wanayapata wakijaribu kutafuta mikopo kwa ajili ya kukuza kilimo chao. Sasa sheria hii italeta unafuu katika kupata mikopo kwa kubadilishana stakabadhi za bidhaa ambazo zimetunzwa kwenye maghala. Kinachotakiwa sasa katika suala kama ambavyo limezungumzwa kwa sababu ni suala ambalo ni geni kidogo inatakiwa elimu kubwa sana

kwa wote ambao wanahusika na hasa kwa wakulima wetu. Inatakiwa hamasa kubwa na mimi nadhani hapa ndipo hata kabla sheria haijaanza kutumika. Mimi ningeshauri kabisa kwamba kusiwe na haraka sana hata ya sheria kuanza kutumiaka. Ipatikane kama miezi sita au zaidi na si chini ya hapo ya kupeleka elimu hii kwa wahusika wote, ili waweze kuielewa vizuri na wakiingia sasa iwe ni rahisi kwao kujikita katika kufanikisha shughuli zao na kushiriki vizuri katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, labda nijikite kwenye kwenye masuala ya kitaalamu ambayo nayaona katika sheria hii. Katika Sheria hii kwa kweli kinachozungumziwa hapa ni kitu ambacho kwa Wazungu wanasema *Commodity Collateral Management.* Sasa ni suala la kitaalam ambalo mhusika mkuu katika *Collateral Management* na hasa unapozungumzia hii *Warehouse Receipts* ni yule *Warehouse Operator* na mimi namwona kama Mdau mkubwa kuliko wote katika suala hili. *Warehouse Operator* ambaye hiyo ni lugha rahisi lakini kwa kweli huyu anaitwa *Collateral Manager* ndiye anayeunganisha wanunuzi na wale wakulima, ndiye anaye miti-*gate risks* au anayehakikishia mabenki kwamba fedha zao watakazo kopesha kwa wakulima au makundi ya wakuliama pesa zao zitakuwa salama kwa maana kwamba hawatapata hasara.

Lakini kubwa *Warehouse Operator au Collateral Manager* ndiye atakuwa muangalizi mkuu wa maghala haya au ghala hilo ambalo atakuwa analitunza na katika hili kuna masuala ya utaalam katika kutunza vifaa na vilevile katika kuhakikisha kwamba thamani ya bidhaa hazipungui au *quality assurance na quality control.* Sasa lazima tuwe na hakika kwamba huyu *collateral Manager* au *Warehouse Operator* ni mtu ambaye amejizatiti katika utaalamu, amebobea na wataalam ambao wanauwezo wa kuwa na hakika kwamba bidhaa zilizotunzwa kwenye maghala haya yako salama lakini vilevile afanye tathmini ya kina ya bidhaa zinazotunzwa kwa maana ya ubora wake vilevile usalama wake.

Kwa hiyo, mimi namwona huyu *Warehouse Operator* kama mtu ambaye lazima awe na wataalam wa kwenye masuala ya fedha yaani *Financial Analysts* ambao wanaweza wakafanya tathmini kwanza ya mkopaji kwa sababu bado kutakuwa na *risk* pamoja na kwamba unazo bidhaa lakini ufanye *indepth analysis* na *due diligence* ya huyo anayekopa anao uwezo mwingine kwa sababu wakati mwingine pamoja na kwamba una bidhaa zake hiyo haitoshi kama ni mtu ambaye historia yake ya ukopaji siyo nzuri, sasa hilo ni muhimu sana na linahitaji utaalam mkubwa. Je tunahakikishaje kwamba hawa wataalam wapo?au huyu ambaye ni *Warehouse Operator* au *Collateral Manager* ni mtu mwenye utaalam huu ambao ninauzungumzia. Lazima afanye tathmini ya uwezekano wa fedha kutorudi , afanye *transaction and repayment risk analysis.* Je, uwezekano wa fedha zile kupatikana ama kutokana na bidhaa zile au kama kuna tatizo la bidhaa kutorudisha fedha zile. Je, fedha zinaweza zikarudi au hapana.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi kama nilivyosema ni muhimu katika maghala yale kuwepo na wataalam ambao wanaweza wakatunza bidhaa zile kwa ubora ule unaotakiwa. Sasa tumeangalia katika maghala yetu kwa sababu mpaka sasa tumekuwa na maghala katika Vyama vya Ushirika, Wakulima wenyewe na ukiangalia uharibufu wa bidhaa zetu kwenye maghala ni mkubwa sana, kubwa linalojitokeza ni ukosefu wa utaalam katika utunzaji wa bidhaa, sasa tunahakikishaje kwamba wataalam

wa kutunza bidhaa huyu *Warehouse Operator* anao? Je, Wataalam wapo wa kutosha nchini katika suala hili la utunzaji wa bidhaa na hapa ndipo unapokuja kuangalia kwamba kuna Taaluma ya Ugavi ambayo tukiiangalia katika nchi hii kwa kweli kuna mapungufu makubwa na ndiyo maana upotevu mwingi unaojitokeza katika suala zima la bidhaa na vifaa linakuja kutokana na utaalam ambao hautoshelezi katika bohari zetu nyingi na haya maghala kwa kweli ni mabohari. Sasa sambamba na kuanzisha sheria hii ni vema basi tukatilia maanani vilevile elimu katika utaalamu wa utunzaji bidhaa, elimu katika kuhakikisha ubora wa bidhaa yaani *quality control/quality assurance* na tuangalie kwamba *Warehouse Operators* ambao watajitokeza au *Collateral Managers* watakaojitokeza kutaka kumiti-*gate* hizi *risks* za pande zote ni watu ambao kwa kweli wana utaalam huo.

Lakini watapataje utaalam kama nchi hatujatilia maanani mafunzo katika utaalam huu wa Ugavi, hivi karibuni tumepitisha Sheria ya Ununuzi na mimi nadhani tufike mahali pamoja na sheria hii na mambo mengine tuwe na Sheria ya Utunzaji wa Vifaa katika nchi hii. Nasema hivyo kwa sababu Sheria ya Ununuzi imechukua tu hali ile kwamba ukiisha nunua basi, lakini kuna masuala ya utunzaji.

Je, haya tunayafanyaje? Ndiyo maana katika kongamano fulani nilisema: "Kutilia maanani *Procurement* peke yake au ununuzi peke yake ni kama Mama anayekwenda kuchota maji mtoni na anakuja tena kilomita kama tatu anamwaga kwenye pipa kumbe lile pipa limetoboka anarudi mtoni anaendelea kumwaga pipa halitajai, akimaliza *trip* zake kumi hakuna maji hata kidogo". Hii ni kwa sababu hatuzingatii ubora wa lile pipa na utunzaji wa yale maji yanapofika pale kwa hiyo tusiangalie upande mmoja wa ununuzi tu, Tuangalie na upande huu wa utunzani wa vifaa. Haya Maghala haya yanatakiwa kuwa na wataalam wa aina hiyo. Je, tunao? Je tumezingatia utaalam katika utunzaji wa maghala? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mimi nilitaka nizungumzie hayo ya kitaalam kwa maana ya kusisitiza suala hili lakini kama nilivyosema sheria hii ni sheria ambayo itatusaidia. Wakulima wetu watafaidika na ule wasiwasi wa baadhi ya Wabunge walionyesha kwa kweli hautakuwepo, ili mradi tu wakulima wapate elimu na hamasa nzuri waungane katika vikundi vikundi katika Ushirika ndipo wataweza kupata faida zaidi ya mpango huu. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema mwishoni kuwepo na utaalam wa fedha, utaalam wa utunzaji wa vifaa, utaalam wa masuala ya *quality control* na kwa kweli utaalam wa mambo ya *Export and Marketing* na mambo kama yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono hoja hii na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na Wabunge wenzangu kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili naomba nitoe salaam za rambirambi kwa Ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Diria , aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Balozi Paul Boman, Mungu aziweke mahali pema peponi roho zao wote. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono Muswada huu ambao uko mbele yetu, kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi nimependezwa sana na Muswada huu na ndicho kilichonivutia kuweza kuchangia kwa siku ya leo. Kwanza mimi nasema Muswada huu ni muafaka kwa upande wa sisi wote na hasa wale ambao hatuzalishi mazao ya biashara. Wale ambao tunatoka sehemu ambazo hazina mazao ya biashara na baada ya ile semina ambayo ilitolewa wiki iliyopita kuonyesha kwamba baada ya mfano mzuri wa mazao yale ambayo yalichaguliwa sasa na mazao mengine yote yataingizwa katika mfumo huu ambao umewekewa sheria ya Stakabadhi ya Maghala ambayo itasaidia hasa kwa wakulima wanaozalisha mazao haya ambayo si ya biashara kiasili.

Mimi nasema niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge ambao walisema kwamba huu mfumo si mzuri. Lakini mimi nasema Muswada huu au sheria hii imeweza kuongeza wigo mkubwa sana kwa wakulima, hasa kwa wale wazalishaji wa mazao haya ya kilimo. *(Makofi)*

Pamoja na faida zote ambazo zimezitajwa wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha Muswada huu lakini vile vile itasaidia kwa Wizara ya Ushirika na Masoko kujua idadi ya mazao ambayo yapo na yamezalishwa na yamekosa soko kwa sababu tumekuwa tukitafuta soko unaweza ukasikia taarifa kwamba tunakosa soko la bidhaa fulani au zao fulani lakini yamewekwa ndani ya majumba ya watu binafsi. Huwezi kujua ni idadi ya kiasi ambayo mazao yanatafutiwa soko. Sasa kwa kuwa na mfumo huu tutajua idadi au Wizara itajua kwamba sasa kama ni Wilaya ya Mbarali, Siha na nyinginezo kwamba kuna idadi ya mazao kiwango fulani, katika maghala ambayo yanatafutiwa masoko na itawapa urahisi mkubwa wa kutafuta soko kwa mazao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile mimi nimefurahishwa sana na sheria hii kwa sababu maghala yalikuwepo na yamekuwa yakitumika lakini kama alivyosema aliyechangia kabla ya mimi kwamba taratibu zilikuwa hazifuatwi za maghala. Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Utunzaji mali zilikuwa hazifuatwi. Sasa baada ya kuwekwa sheria hii maghala haya sasa yatakuwa yatafuata taratibu na hii sheria itawalinda wale wazalishaji na wale watunza maghala na kuwaondolea wasiwasi lakini si hivyo tu itawafanya wajiongezee mitaji hawa wazalishaji wa mazao ya kilimo wakati wanasubiri bei. Sasa kwa sababu tatizo kubwa lililopo hasa kwa sisi ambao tunalima au tunaotoka sehehu za kilimo, wananchi wanazalisha wanavuna lakini wanakuwa na mahitaji muhimu wanashindwa kupata soko zuri lakini yale mahitaji yanawavutia kwamba wauze, inabidi wauze kwa bei ya chini sasa kutokana na mfumo huu ambao una uhakika na unawalinda na unawalindia kutokupata hasara ya mazao nina hakika kabisa utaboresha maisha ya wananchi wote, wazalishaji wote wa mazao haya ya kilimo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kupitia Muswada huu kuna baadhi ya vifungu ambavyo ningependa kutoa mapendekezo. Sheria hii kuna vifungu ambavyo imezungumzia hasa kwa upande wa Bima. Imemwekea *Warehouse Operator* kwamba pale atakapopata hasara na amepewa fidia na Bima atapaswa kupata siku kumi tu awe ameshamlipa yule mwwekaji wa mazao au *depositer* lakini ninavyofahamu Bima tulizonazo hapa Tanzania badoni matatizo ni makubwa. Sasa sheria ipi itamlinda huyu *Warehouse Operator* kwa Bima yenyewe kwa sababu kuna urasimu mkubwa. Sasa kungewekwa kanuni ambayo itamlinda huyu naye kwamba kuna kiwango cha siki ziwekwe baada ya kutoa taarifa na utathmini zifanywe ili kusudi aweze kupata fidia mapema na hatimaye aweze kumlipa huyu ambaye amepata hasara kutokana na kuweka mazao yake katika hili ghala lake. *(Makofi)*

Kwa upande wa Ibara ya tatu zile *content* za *receipts* kuna vipengele vimewekwa kwamba zile *Warehouse Receipts* zitakuwa na *content* ambazo si vizuri kuzitaja zote lakini nimeona kwamba kunakosekana kitu kimoja thamani ya mazao ambayo yamewekwa ndani ya ghala. Haizungumzii hapa kwenye kifungu 33 (1). Sasa nafikiri ingekuwa ni muhimu kuongeza hiyo kujua hiyo thamani kwa sababu unapokuwa na *receipt* ambayo ina thamani mimi nitajua ni kiasi gani ambacho nitapewa mkopo nitakapokwenda Benki na hii asilimia 65 hiyo thamani itakuwa ni kiasi gani ili niweze kuamua kuweka au kuuza.

Kwa hiyo, ningeomba hiyo labda irekebishwe. Kwenye Ibara namba 9(e) inapozungumzia kwamba mojawapo ya mapato ya *Board* itakuwa ni pamoja na kukagua zile *receipts*, kupitisha zile *receipts* ambazo *operator* atazipeleka. Sasa hii naona itaongeza gharama kwani mimi nimetayarisha vitabu vyangu vya *receipt* napeleka kwenye *Board* ili waviangalie kama viko sahihi sasa napo itabidi nilipie au yule *Warehouse Operator* alipie. Napendekeza hiki kifungu kingeondolewe ama kisiwe kipato au wachajiwe kwa sababu itaongeza gharama kwa huyu mzalishaji na lazima afidie hiki kiwangolakini sioni kama kuna umuhimu, *format* nimepewa, taratibu nimepewa na *receipts* zimetengenezwa kutokana na *format* ni kupitia na kukagua tu. Sasa sijui kama kuna haja ya kuweka hizo gharama. Baada ya kupitia hivyo vifungu nilikuwa na mapendekezo muhimu yafuatayo kwa Wizara husika kwamba Wizara kwa sasa baada ya kupitisha hii sheria tunaomba ujikite yaani iende sambasamba na Muswada huu kuhakikisha kwamba unatekelezwa kikamilifu mambo yafuatayo:-

Kwanza, isaidie kuhamasisha hivi Viwanda vya Ushindikaji viwe karibu kabisa na magodauni. Amezungumzia Waziri hapa, sasa kuna mazao ya chakula, mazao ambayo siyo ya biashara na kadhalika. Kwa hali halisi ambayo mimi ninayo. Nina mashamba makubwa kabisa matatu yanayozalisha mpunga na yana maghala yapo pale makubwa na vinu vya kukobolea pale mpunga lakini watu wamekuwa wana wasiwasi wa kupeleka mazao yao pale na kuyatunza sasa kama haya maghala yataboreshwa na hivi Vyama vya Ushirika vikahamasishwa vizuri, vikawezeshwa vizuri, ili kusudi waweze kupokea haya mazao kutoka kwa wakulima mbalimbali na hiki kinu cha kusindikia viboreshwe na viweze kuthaminishwa vizuri na hatimaye kupata soko.Kwa hiyo, ningeomba Wizara husika sasa ianze kusimamia Vyama vyake vya Ushirika vilivyopo vile vya msingi na ambavyo vimeshaanza tayari kuwawezesha kuboresha kabisa

usindikaji wa mali hizi au mazao haya ambayo yataletwa na wakulima na wazalishaji mbalimbali.

Lakini la pili la msingi ni soko. Kuhusiana na soko Wizara husika tunaiomba ijikite hasa kwa sababu watatunza mazao yao katika haya maghala. Huyu *Warehouse Operator* akiachiwa peke yake kutafuta soko siyo rahisi kupata. Kwa hiyo, Wizara ijitoe mapema ihakikishe kwamba haya mazao baada ya kujua huu mfumo umeitikiwa vizuri na wananchi na vyama mbalimbali, wahakikishe kwamba wanatafuta masoko hasa kwa yale mazao ambayo ni ya chakula. Wizara ilikuwa imeachia wakulima na wazalishaji wenyewe wajitafutie soko.

Sasa waingie kwenye haya mazao ya chakula kama mahindi, mpunga, mhogo, karanga na hata korosho ambazo bado zimekuwa zina matatizo ya soko.

Mheshimiwa Spika, lingine ni elimu kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi kwamba vijiunge na huo mfumo kwa sababu tunaamini Vyama vya Ushirika ndiyo chombo pekee ambacho kinaweza kuondoa umaskini kwa wananchi mbalimbali. Ili mfumo huu ufanikiwe na kwa sababu Benki hizi ziko mbali na Vyama vya Ushirika vitatusaidia sana kuhakikisha kwamba huu mfumo unakubalika na unafanikiwa kwa sababu sio rahisi kwa mwananchi kutoka Kijijini kwenda kutafuta Benki ambayo ipo mbali. Sasa vikiboreshwa na vikafanywa kama Benki mahsusi vitasaidia sana kutoa mikopo kwa hawa ambao wamekuwa na hizi stakabadhi za maghala.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilikuwa na pendekezo kwa huyu *Warehouse Operator,* mwenzangu amesema kwamba awe mtaalamu wa utunzaji, lakini hapa inaonekana kwamba kazi ya *Warehouse Operator* itakuwa ni kupokea na kutafuta soko lakini vile vile awe na utaalamu wa kuwasaidia wale ambao wanakuja kuweka mazao, kujua jinsi ya kupata mikopo kwa sababu tatizo lipo hapa ni urasimu wa Mabenki yaliyopo. Huyu mtu atapewa risiti, lakini itakuwa bado tatizo kwenda Benki nenda rudi, nenda rudi, hatapewa huu mkopo na hataona umuhimu vile vile wa mfumo huu na hataona kwamba hii Sheria kweli imemsaidia.

Kwa hiyo, tungependa kuona leseni inapotolewa kwa *Warehouse Operator* aangaliwe kama ana-*qualify* kwa vitu vyote. Kwanza ni mtaalamu wa utunzaji, pili ana uwezo wa kusaidia hawa watu wanaowekeza kupata mikopo na mwisho na taratibu nyingine ambazo zimetajwa katika huu Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile taarifa ya bei mbalimbali kwa mazao ambayo yatawekwa kwenye maghala kwa sababu ni kitu ambacho kinasumbua sana kwa sisi wazalishaji au kwa watu wote wanaozalisha, zile taarifa za bei zitolewe kwa wakati muafaka ili mtu aweze kujua na awe na taarifa kwamba sasa bei ya mazao imepanda na imekuwa kiasi gani na iwe ni wakati mzuri wa kuuza kusudi asipoteze ile faida ambayo angeuza moja kwa moja au ile faida ambayo ataipata katika kuweka maghala. Kwa hiyo, tunaomba huu utaratibu wa kutoa taarifa za bei kadri zinavyobadilika kwa msimu uimarishwe ili ziwafikie wadau wote kwa wakati muafaka. Lakini la msisitizo ni urasimu wa benki na bima, kwa kweli kanuni iwepo kwa sababu Waziri amepewa nafasi ya

kutunga kanuni mbalimbali katika Muswada huu, kwa hiyo, ihakikishwe kwamba kanuni zinatungwa kuwalinda wote ambao watatumia bima na hizi benki zihakikishe kwamba zinapunguza urasimu bila kusahau riba za mikopo, isionekane kwamba naweka benki ile faida ambayo nitaipata inamezwa na riba ya ule mkopo ambao nimepewa. Kwa hiyo, hilo ningeomba sana lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema tena naunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie katika kujadili Muswada huu. Awali ya yote naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa ndugu na familia za Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Marehemu Balozi Paul Bomani. Katika uhai wao walitoa mchango mkubwa katika mafanikio na maendeleo ya nchi hii. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi Muswada huu ulivyowasilishwa kwa ufasaha na Waziri wa Ushirika na Masoko, Mheshimiwa George Clement Kahama na baada ya kuusoma na kuuelewa, natamka kwamba naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo unaopendekezwa wa kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala na utumiaji wa mazao kama dhamana kuweza kukopa kwenye Mabenki kwa kutumia stakabadhi na vile vile kutumia stakabadhi za mazao kwenye maghala, kubadilishana fedha ni mambo mapya kabisa.

Kwa mara ya kwanza kabisa mazao ya kilimo yatahalalishwa kisheria ili yatambulike na kutumiwa kama dhamana ya kupata mikopo kutoka benki. Naamini huu ni ukombozi wa kuwatoa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo kutoka kwenye lindi la umaskini na kuinua kipato chao na hali yao ya maisha kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, wakulima ili wafaidike zaidi katika mfumo huu hawana budi kujiunga kwenye vikundi vilivyosajiliwa na Vyama vya Msingi. Hii itawawezesha kuzalisha mazao mengi na kupeleka mazao mengi kwenye maghala kwa nia ya kupata bei nzuri kutegemeana na soko na kwa kweli Muswada huu utatusaidia kuhamasisha wananchi wajiunge kwenye Vyama vya Ushirika. Vile vile kukiwa na utaratibu wa kueleza bei za mazao, wananchi watajua ni wakati gani watumie mazao yao kujipatia fedha na kwa maana hiyo kipato chao kitaweza kuinuka na hawatapata hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Muswada huu wakulima watatakiwa kupeleka mazao yao kwenye maghala yenye sifa zinazotakiwa. Bahati mbaya hali halisi ilivyo hivi sasa huko Vijijini ambako ndiko wakulima walipo maghala hayo hayapo, lakini tunayo maghala ambayo yalikuwa mali ya Vyama vya Ushirika vilivyosambaratika. Kwa mfano, katika Jimbo letu la Gairo tunayo maghala hayo katika Vijiji vya Gairo, Msingisi, Rubeho, Iyogwe, Kinyolisi, Chakwale, Leshata na Nongwe na Shirika la Msaada la *AFREDA* kwa kushirikiana na wananchi walitusaidia kujenga maghala ya kuhifadhi nafaka katika Vijiji viwili vya Mkalama na Majawanga.

Mheshimiwa Spika, tegemeo langu ni kwamba maghala yote hayo yatafanyiwa ukarabati na maghala mengine yatajengwa huko Vijijini ili yarahisishe utunzaji wa mazao hayo kwenye maghala. Vile vile mategemeo yangu ni kwamba maghala haya yatakuwa yanakaguliwa mara kwa mara kuhakikisha mazao yaliyohifadhiwa hayaharibiki.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu vile vile unategemea kuwepo kwa Benki zitakazokuwa tayari kutoa mikopo kwa wakulima kwa kutumia mazao kama dhamana. Benki tulizonazo Vijijini ni *SACCOS* Benki ambazo zina mitaji midogo. Tumeambiwa hivi sasa kwamba ni Benki tatu tu *CRDB, Exim Bank* na *Kilimanjaro Cooperative Bank* ndio zimekubali na kuingia katika utaratibu au mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali ishawishi na Benki nyingine kwa mfano *National Microfinance Bank* na Benki ya Posta nazo ziingie kwenye mfumo huu na kukopesha wakulima kwa kutumia stakabadhi za mazao na vile vile kuiomba *CRDB* ambayo ndiyo mdhamini mkubwa wa *SACCOS Banks* iweze kuziongezea *SACCOS Banks* mitaji ili nazo ziweze kuingia katika mfumo huu. Kwa mfano, katika Kijiji cha Gairo tunayo *SACCOS Bank* ambayo imeimarika sana na hivi sasa inatoa huduma hata za *Tembo Card.*

Nadiriki kusema kwamba inaweza kuingia katika mfumo huu na kwa maana hiyo wakulima wa Jimbo langu la Gairo wanaweza kufaidika sana ikiwa *SACCOS Bank* ya Gairo inaweza kuingizwa katika mfumo huu na maghala hayo niliyoyataja yakikarabatiwa wakulima watafaidika.

Mheshimiwa Spika, tumejulishwa kuwa zipo gharama zitakazobebwa na mkulima kwa mfano, Bima ya mazao, gharama ya kuhifadhi mazao kwenye maghala, gharama za usafirishaji, riba kwenye mabenki na kadhalika. Upo uwezekano kwa gharama hizi kuwa kubwa kiasi cha kuwafanya wakulima wapate hasara. Naiomba Serikali ihakikishe kuwa inaweka mazingira yatakayohakikisha kwamba mkulima haathiriki na kupata hasara kutokana na gharama hizi.

Mheshimiwa Spika, ngoma hunoga kutegemea wachezaji. Wachezaji wakuu katika sheria hii inayopendekezwa ni wakulima wenye mazao yao, waendeshaji na wamiliki wa maghala, wanaotoa stakabadhi za mazao, mabenki yanayotoa mikopo na Serikali yenyewe. Mafanikio yatapatikana kama kutajengeka uelewano wa kutosha, ushirikiano wa kutosha na dhamira ya kutosha katika sehemu zote. Watu husema imani huzaa imani. Kwa mfano, wakulima wakiamini kwamba mazao yao yatahifadhiwa kwa usalama kwenye maghala, watapeleka mazao yao kwenye maghala hayo. Wakulima pia wakiamini kwamba hawatadhulumiwa na hao wenye maghala, watapeleka mazao yao kwenye maghala na benki nazo ikiwa zitajua kwamba kuna sheria ya kuzilinda zisipate hasara na hizo benki zitakuwa tyari kujiunga katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo kubwa zaidi ni la elimu. Elimu hii itolewe kwa wakulima na wananchi kwa ujumla waelewe mfumo mzima wa sheria hii na kukubali na kutambua kwamba sheria hii ni kwa manufaa yao na watambue kuwa stakabadhi za

mazao kwenye maghala zitatambuliwa kisheria kuwa na hadhi ya fedha na zinaweza kubadilishwa na fedha na zinastahili kuhifadhiwa kama fedha hapa panahitaji elimu ya kutosha, wananchi wengi hawataamini.

Kama nilivyosema hili jambo ni jipya, hawataamini kwamba hizi stakabadhi ambazo zinatolewa na wawekezaji wa maghala kweli zina haki ya kisheria ya kuweza kubadilishana kwa fedha. Kwa hiyo, mategemeo yangu kwamba wananchi kwa ujumla wataelekezwa na kufundishwa hadi waelewe na kukubali na hapo naona kwamba na sisi Wabunge ambao sasa tumekwishaeleweshwa juu ya utaratibu na mfumo huu tuna nafasi nzuri ya kuwaelimisha wakulima kwenye Majimbo yetu na wakaweza kuingia katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Waziri kwa kutuletea sheria hii ambayo utekelezaji wake kama nilivyosema naamini utakuwa ukombozi kwa wakulima. Kwa kuwa mimi nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nilishiriki katika kujadili Muswada huu kabla haujaja Bungeni. Kwa hiyo, sina mengi zaidi isipokuwa niliona nisisitize haya machache na narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa jana na Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia madhumuni kama yalivyotolewa ukurasa wa 41 na ukifuatilia jinsi Mheshimiwa Waziri alivyotoa mawasilisho yake inaonekana kama kwamba tunaunda kitu ambacho kwa kweli ni cha kumkomboa Mtanzania na hasa mkulima mdogo. Inaonekana kwamba mwelekeo na matarajio ni hayo na hata Waheshimiwa Wabunge ambao wamekwishazungumza wanaonyesha kuunga mkono suala hili. Mimi nataka kwa kifupi nitoe angalizo kwamba, maudhui ya Muswada ni mazuri lakini utekelezaji wake haulengi kabisa na kwa uwazi katika kumnufaisha mkulima na hasa mkulima mdogo mmoja mmoja ambalo ndio nafikiri ni tatizo linalotukabili.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaelekea kama kwamba mkulima anachokihitaji ni mahali pa kuhifadhi mazao yake wakati akisubiri kupata bei nzuri. Sidhani kwamba ndicho mkulima wetu wa kawaida anachokihitaji. Mkulima wetu baada ya kuwa amezalisha mimi naamini anachokihitaji ni soko la uhakika na pesa ya kuweza kumsaidia ili aweze kuzalisha kwa wingi na kwa ubora. Hili ndilo tatizo tulilonalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tutaweza kumhakikishia mkulima kwamba atazalisha kwa wingi kama Muswada unavyosema kwa maudhui na akazalisha kwa ubora na akawa na uhakika kwamba mazao yake yatapata soko lililo *stable* na lenye uhakika na kwa bei nzuri hatutakuwa na haja ya kuanza kufikiria fikiria haya tuliyo nayo kwa sababu kukopa ni dalili ya umaskini, kama una pesa ya kutosha huhitaji kwenda benki kukopa. Kwa hiyo, nataka nitoe angalizo na tahadhari kwamba wakati huu Muswada unaweza kuwa

mzuri kwa vikundi, kwa wazalishaji wengi, kwa mzalishaji mkubwa lakini si mzuri sana kwa kusimamia peke yake au kumhudumia mkulima mdogo.

Mheshimiwa Spika, katika hili tunahusisha Mabenki na tunatunga sheria kwamba yeyote atakayepata hiyo risiti aitambue na aikubali kama dhamana ya kumpa mkulima mkopo. Hivi tujiulize katika Tanzania hivi sasa tulivyo, tuna benki ngapi hivi sasa ambazo tunaweza kuziita za kwetu ambazo tunaweza kuwatungia sheria. Kama benki si zetu na zimekuja kufanya biashara, hivi tuna uhakika gani kweli kwamba hizi benki tunazitungia sheria na zitakuwa tayari kukubali yale mazao yaliyopo katika ghala kama dhamana maana yake hivi sasa hatuna benki, *NMB* tuliyokuwa tumebaki nayo hivi sasa sio yetu. Hivi utamwambiaje *Exim Bank* kwamba aingie kwenye utaratibu huu, utamwambiaje *NBC* aingie kwenye utaratibu huu wakati hizi beni si zetu. Tunaweza kuwa na tumaini zuri tu kwamba watakubali, lakini tukafika mahali tukajikuta kwamba mfumo tumeuweka lakini benki zikatu-*let down* na zikawa hazipo tayari, je, na sisi tumejiandaa vipi kukabiliana na hali kama hii itakapotokea? Maana yake kama benki ikishagoma kukubali hizi risiti basi mfumo mzima unakuwa hauna maana. Sasa ni vema tukawa kwanza na uhakika na benki ambazo zitakuwa zimekubaliana na huu mfumo na zenye mtandao mpaka huko Vijijini ndio tuanze kufikiria mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho kinanipa wasiwasi sana katika huu mfumo ni gharama ambazo zinajitokeza na ambazo mkulima lazima azibebe. Tumeanza na Bodi, tuna watakaojenga maghala, watakaoendesha maghala yenyewe, tuna wakaguzi, tuna bima, tuna *classifiers,* wote hawa wanategemea kulipwa na kwa kweli ndio wale Mheshimiwa Edson Halinga anaowaita walaji tu. Hivi hatuoni kwamba tunamwongezea mzigo mkulima? Maana yake hawa wote ni wafanyabiashara na kama ni biashara nina hakika atakayebeba huu mzigo ni huyu mkulima atakayekuja kuwekeza na wala haitwi *owner* anaitwa *depositor.* Nina wasiwasi mwisho wa siku hata ile bei yenyewe atakayokuja kupata mkulima zikishakatwa hizi gharama bado mkulima atabaki na hela ndogo sana mfukoni.

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya bima. Ni vizuri na ni vema kwamba mazao na maghala yawekewe bima, sina ugomvi na hilo. Lakini tunajua yameingia makampuni mengi ya bima nchini na tuna Shirika letu pia la Bima la Taifa, je, yana uwezo gani kifedha kuweza kukidhi kulipa fidia kama matatizo haya ya kuungua kwa maghala au mazao yatakapokuwa yametokea na ni utaratibu gani ambao sheria inaweka sasa kwamba itakapotokea *priority* ya kulipwa aanze huyu *depositor* ambaye ni mkulima ambaye tunatakiwa kumsaidia kwa sababu mashirika mengine kwa kweli likiwemo Shirika letu la Bima la Taifa hayana kabisa uwezo wa kuweza kuhudumia kwa sababu hata sasa hivi bima nyingi zimeiva, madai mengi ya bima yapo na tumeshindwa kulipa?

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba katika hili tumwangalie mkulima mmoja mmoja kwanza kabla ya kuangalia makundi ya wakulima. Lakini labda ni nafasi nzuri kwa Wizara sasa kuimarisha mfumo wa Vyama vya Ushirika ili kama mkulima mmoja mmoja hataweza kufaidika angalau kikundi chake au Chama chake cha Msingi kiweze kufaidika kwa kutumia utaratibu huu wa risiti katika maghala.

Mheshimiwa Spika, katika hili Mheshimiwa Waziri anayehusika amepewa madaraka ambayo kwa upande wangu nafikiri ni makubwa mno. Yeye ndiye anachagua wajumbe wa Bodi, yeye ndiye anachagua Mwenyekiti wa Bodi, yeye ndiye anachagua Mkurugenzi Mtendaji na yeye ndiye mwenye uwezo wa kumfukuza *Chairman.* Lakini pia kunapotokea matatizo kutokuelewana kuanzia kwa *Operators, Classifiers* na wengine rufaa zote zinapelekwa kwa Waziri huyo huyo ambaye washauri wake ndio hao watakaokuwa wamefanya vibaya. Hili mimi naliona kama halitendi haki hasa katika mfumo wa biashara huria. Kungekuwa na utaratibu mwingine ili hizi rufaa za kutokubaliana na Bodi ambayo Waziri aliiunda, kutokubaliana na *DG* ambaye Waziri alimteua, ziweze kutoka kwenye mfumo wa Waziri, kuwe na chombo kingine cha kusikiliza rufaa nje ya utaratibu huu ambao umewekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 44 kinatoa haki kwa yule mwendesha ghala kuuza mazao ya mtu aliyewekeza mle kwenye ghala lake bila hata kuwasiliana na mwenye mazao ili mradi tu atakuwa ama anataka kukamilisha kulipa yale madeni yake. Sasa hii mimi nafikiri ni hatari sana. Ili tumlinde huyu mkulima na huyu *depositor* mwenye mazao nafikiri kungekuwa na mawasiliano ya karibu kabla ya kufanya hivyo ili aone kama kweli ameshindwa kumlipa zile gharama zake kuliko mwenye ghala kuamua peke yake na kuuza yale mazao bila kumhusisha mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika orodha ya Wajumbe wa Bodi ambao watateuliwa na Waziri ukurasa wa 36 ipo wazi. Lakini katika mfumo huu ukija kuangalia hawa wanaoitwa *Warehouse Operators* ni wadau wakubwa sana katika hii shughuli nzima. Ningeshauri basi, *Warehouse Operators* wawe na mwakilishi wao kwenye Bodi ambayo Mheshimiwa Waziri ataiunda.

Mheshimiwa Spika, *section* ya 17 (2), wanazungumzia juu ya muda wa leseni *(validity of the licence)* kwamba ni mwaka mmoja na baada ya hapo inaweza kuwa *renewed.* Nina hakika kuna gharama za kupata hii leseni na nina hakika wakati wa ku-*renew* kutakuwa na gharama.

Mimi nafikiri na hasa tukizingatia kwamba wengi wa *Warehouse Operators* watakuwa Vyama vya Msingi, ningeshauri kwamba badala ya kuwa mwaka mmoja basi tufanye miaka miwili ili kuwapunguzia mzigo hawa *Warehouse Operators* ambao wengi naamini watakuwa Vyama vya Msingi.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tena kwamba maudhui ya Muswada ni mazuri na nina hakika tukienda kwa mfumo wa vikundi na Vyama vya Msingi inaweza kuwa na maana zaidi. Iwapo Muswada ungejikita katika kumsaidia mkulima mmoja mmoja mimi nisingekuwa na tatizo la kuunga mkono moja kwa moja. Lakini ni mfumo mpya ambao unahitaji kufundishwa ili na wale wakulima wadogo wadogo waweze kuelewa watafaidika vipi wao wenyewe. Cha msingi ni kwamba mkulima mdogo ni vema akalindwa akawa na uhakika wa soko, akawa na uhakika wa kusaidiwa kuzalisha kwa ubora. Hapo ndipo atakapokuwa amefaidika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa kifupi sana katika Muswada huu. Kwanza, naomba na mimi niungane na wenzangu kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia katika kikao hiki nitoe pole kwa jamaa na ndugu wa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria pamoja na mzee wetu Marehemu Balozi Paul Bomani.

Mheshimiwa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria nilikuwa naye kwenye Bodi ya *LART* kwa hiyo, nilifanya naye kazi vizuri. Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamechangia mambo mengi mazuri katika Muswada huu. Napenda niipongeze sana Serikali kwamba kwa sasa hivi inajitahidi sana kutafuta njia za kuwasaidia wananchi katika kujikwamua ili kuondoa umaskini. Tunachokifanya sisi hapa ni kuboresha tu nia njema ambayo Serikali inaonyesha. Nina mfano mmoja, inaonekana ardhi yetu ilikaa, lakini ilikuwa inaonekana haina thamani, wanasema *dead capital,* ilionekana mazao kama vile thamani yake ni kidogo.

Kwa hiyo kwa mfano, unakuta Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi aliamua kabisa kuleta sheria hapa kuthamanisha ardhi na kwa hiyo, ardhi imekuwa ni bidhaa, imepewa thamani ambayo tumekuwa tukikaa nayo kwa muda mrefu. Lakini sasa mtu anaweza kuitumia kwa kuweka kama dhamana au kama *collateral* na akapata gari, akapata trekta na hivyo hivyo Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko lakini ni Serikali kwa ujumla wanaona kwamba mazao haya haya kwa sababu walikuwa hawana njia nyingine yanaweza yakathamanishwa yakawekwa katika utaratibu na watu wakapata dhamana kwa kutumia risiti.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa na Madiwani wangu wawili wa Mbozi ambapo Mbozi ni *pilot area* ya kupima ardhi za kimila. Sasa Madiwani wale wamekuja hapa, lakini wamekuja kuchukua trekta kwa sababu sisi tumeshapata zile leseni za ardhi za kimila kutoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Imethamanishwa tu ni ardhi ya kawaida lakini wale Madiwani wana zile hatimiliki za kimila na mmoja anakopeshwa shilingi milioni 35 kwa kununua trekta. Lakini tunamshukuru Naibu Waziri alimsaidia angeweza kuinunua juu zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka kusema tu kwamba Serikali inaona raslimali ambazo watu wanazo kama tukifanya utaratibu kwa hiyo, wanaweza wakazitumia kuondoa umaskini. Sasa ndiyo hilo nalo limekuja la mazao ambapo kwa kweli tunayo mazao. Wakati fulani kama kule Sumbawanga unakuta mahindi ni mengi sana na kule Ruvuma na wapi yamekaa yanaoza kumbe mtu angeweza kuwa ameyaweka kwa utaratibu huu ingemsaidia sana kupata chochote kuliko kukaa na mazao lakini hupati kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema hii ni *new thinking,* ni mawazo mapya, ni mfumo mpya wa kuleta maendeleo kwa wananchi na ni dunia nzima inakwenda mtu anaringia kile alichonacho. Mzee Jackson Makwetta mwalimu wangu anahangaika sana

na kila wakati husema kwa nini hatuwezi kutumia jiografia ya nchi tu kupata fedha nyingi, *forex* mnapata fedha nyingi sana kwa jiografia tu. Nchi yetu tumejaaliwa jiografia nzuri kuna mambo ya ajabu sana. Sasa nchi zingine zina mawe tu lakini mawe tu mnakwenda kushuhudia tu wanapata fedha. Ni kwa maana hiyo kwamba sasa hivi mtu anatakiwa kile alichonacho ndicho kimsaidie katika kuleta maendeleo kwake.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wetu ni mdogo tu tunapochangia hapa wenzetu watuelewe tu kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi tunataka kusema tuboreshe nia njema hii kama ni mambo ya ardhi kwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, basi yasimamiwe vizuri, yakishakamilika Mbozi yaenee katika nchi nzima ili watu wapate hatimiliki.

Mimi jana nimepata hatimiliki yangu kutoka kijijini kwangu ninayo hapa nzuri tu nimechukua eka 100. Kwa kweli naweza nikakopa hata milioni 50 mpaka 200 wamesema kwa hii hatimiliki. Ni ardhi tu iko pale na nyasi, lakini mimi nimerithishwa ni hatimiliki ya kijiji ya mila. Sasa naona ardhi kumbe *it was laying fallow,* lakini *I can earn a lot of money* na nikaendesha maisha yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mazao nayo hivyo hivyo na Waziri mwingine naye atuambie kitu gani anaweza kuleta, namna gani, hivyo hivyo wananchi waweze kuondokana na umaskini. Sasa tunaboresha ni kwamba kwa kawaida kwa tabia zetu, nia njema hugeuka kuwa kilio ndiyo tatizo. Kwa nini, kwa sababu ya watu watakaosimamia, kwa sababu ya namna itakavyosimamiwa. Muswada huu umekuja hapa una mlolongo wa mambo mengi sana. Lakini la msingi ambalo mimi kwa kifupi nataka niliseme ni mafunzo au elimu kwa kila mmoja atakayehusika sheria itakapopita siyo mafunzo ya redio tu bali ya vikundi hata ikiwezekana kwenye vijiji kwenyewe wananchi waweze kuelewa.

Dhana ya ardhi ilipoanza natoa mfano hapa kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi ilileta shida. Kwenye Kamati yangu watu walikuja wakasema sasa Serikali inataka kuuza nchi kwa sababu tumezoea mambo ya namna nyingine, sasa mambo mapya haya ni lazima tujitahidi kubadilisha mawazo ya watu. Binadamu wabadilishwe mawazo tuingie katika mawazo mapya *new thinking, new ways of doing things* hatuwezi kuendelea kuruka kwa ubawa ule ule tu hata kama hauna manyoya itabidi tufike mahali tutafuta namna ya kwenda. Kwa hiyo, tuliambiwa ooh, wanauza nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi mimi nafurahi sana *to report to you* kwamba hii hatimiliki niliyonayo hapa kwenye begi langu kumbe naweza nikakopa hata basi. Lakini mafunzo sasa katika maghala haya, katika bodi hii na kwa wale watakaotoa leseni na hivi na hivi kila mmoja, hasa watu wetu wapate elimu ya kubadilika na ni kazi ya Serikali na sisi Waheshimiwa Wabunge kujitahidi kufafanua jambo hili lieleweke. Wananchi wasipoelewa jambo njema kwa kweli wataliona ni baya. Lakini wanaweza wakaelewa na wakaenda kwa nia njema. Kama vile watu wanavyoamua kujiingiza kwenye mifuko fulani baadaye wanakuta kwamba ni *dubious play* wanasema kumbe mchezo tunapelekea watu fedha. Kwa hiyo, ili kukwepa hili Waziri wa Ushirika na

Masoko mjitahidi kutoa elimu, mafunzo kijiji kwa kijiji ikiwezekana kila atakayehusika aweze kuwa mwadilifu na aweze kuwa kumwaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jirani yangu hapa ameongea kwamba ni nani anayekopesha maana hawa ni *small holders* na wafanyabiashara ndogo ndogo. Maana biashara inakwenda kwa biashara. Sasa biashara hii ni ngumu benki iko wapi, ile ya ardhi wanapata *Exim Bank* iko Dar es Salaam na hivi na hivi. Sasa hii benki iko wapi ni *NMB* ambayo nayo lazima tuwe waangalifu sana katika kuibinafsisha hiyo Benki *NMB* kama tutampa mtu wa hivi hivi tu maana mambo haya lazima tuwe waangalifu. Hii ni *NMB* maana tunaoifahamu ni *NMB* labda kuna zingine hizi *Bank of Malaysia.* Ni benki gani itakayokuwa *ready* kufanya biashara ya namna hiyo. Hilo ni vizuri Mheshimiwa Waziri alione.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli labda tungeanzisha Benki ya Wakulima au Benki ya namna fulani kwa ajili ya shughuli hii kwamba maadamu tumeanzisha shughuli hii basi Serikali iji-*organize* ikae kwa pamoja iseme sasa benki itakayoshughulikia suala hili ni hii hapa. Labda Benki Kilimo sijui na Ushirika na hivi. Huko nyuma tulikuwa *Cooperative Bank* kitu cha namna hiyo. Lakini ni benki ipi kama ni ya kutoka nje ni benki ipi kama ni ya hapa nchini ni benki ipi. Kwa hiyo, hilo nalo mimi nilifikiri ni vizuri kabisa niliongelee.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna benki zingine zitafika mahali zitasema zimefilisika hawana, wanaondoka. Sasa wananchi wanapoanza kukata tamaa ni pale tu ambapo mambo waliyotegemea kumbe yanakuwa sivyo. Kweli na mimi naona mwenzangu mwingine alikuwa ananidaka sijui aliona *notes* hapa kwamba Waziri anapewa madaraka mengi ya kuteua na kufanya hivi na hivi na baadaye rufaa inaishia kwake. Sasa ikanikumbusha habari wakati tuko kwenye mfumo wa Chama kimoja. Mtu mmoja alikuwa ni *DC* au sijui alikuwa mtendaji, lakini wakati huo ni Mwenyekiti, mkigombana katika shughuli za utendaji anasema utakuja kwenye Ofisi ya chama.

Mheshimiwa Spika, wewe ulikuwa Katibu Mtendaji Mkuu kwa muda mrefu, unafahamu hali ilivyokuwa. Kwa hiyo, mkikosana kwenye utendaji anasema aletwe kwenye chama. Ukienda katika chama unamkuta mumiani ni yule yule ndiyo yuko pale. Sasa unasema ahaa, yule si ndiye tuliyegombana, anasema ahaa, sasa hapa siyo mimi hapa sasa ni chama, nitakudhibiti. Utaratibu wa namna ile tunashukuru sana Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, aliliona akasema hivi vitu vitenganishwe ili haki iweze kutendeka. Sasa na Mheshimiwa Waziri nafikiri ni vyema kama kutakuwa ama hii bodi yenyewe au kutakuwa na Kamati fulani ambayo itashughulikia masuala ya rufaa.

Kwa hiyo, hawezi yeye mwenyewe kufanya mlolongo wote halafu baadaye anakuwa ndiye wa kutoa maamuzi. Kwa sababu katika mlolongo huo kuna mengine yeye mwenyewe atakuwa ameyadhibiti kwa hivi na hivi. Sasa rufaa inakujaje wakati na yeye mwenyewe wakati mwingine walikuwa wanaandikiana na hivi katika taratibu zenu. Mimi nafikiri tungefikiri Kamati ndogo au nini itakayoshughulikia rufaa, lakini baadaye Mheshimiwa Waziri anaona kama maamuzi yamekwenda sawasawa au namna gani? Kusema yeye mwenyewe moja kwa moja inaweza ikamletea matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema nashukuru sana la msingi ni elimu, la msingi ni benki gani na la msingi ni kwamba Serikali imetusaidia kweli kuona matatizo ya wananchi. Lakini tuwaweke wananchi sawasawa kwa mafunzo na kila mhusika na sisi Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kuingiza elimu hii wananchi wabadilike kwamba walichonacho ndicho hicho wanachoweza kujiletea maendeleo nacho na Serikali iendelee kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niseme kidogo kuhusu Muswada huu ulio mbele yetu. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa ile Wizara kwa kazi nzuri na juhudi wanazozifanya kumshughulikia mkulima. Wanastahili pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi mimi sina tatizo na Muswada huu naunga mkono mia kwa mia. Sina tatizo nao sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichangie maeneo machache katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada huu inaweka utaratibu wa kutoa leseni kwa maghala. Lakini hata hivyo, kifungu 16(1) kinasema kwamba taratibu za kuomba leseni zitatolewa kwenye kanuni ambazo zitatolewa na Mheshimiwa Waziri baadaye. Kwa maana hiyo kanuni hazijulikani zitakuwaje. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri bado hajazitoa na wala hajaziambatanisha kwenye nyongeza kule mwisho wa Muswada.

Mheshimiwa Spika, kama ninavyofahamu jambo hili Waheshimiwa Wabunge tumelipigia kelele sana kwamba ni vizuri kama Waziri anaweza akaandaa Muswada wote kwa nini isingewezekana kuandaa kanuni zinazofungamana na ule Muswada. Tumepitisha Miswada mingi hapa, upo Muswada na zipo kanuni zake zimefungamanishwa pale. Kwa hiyo, mtu ukichangia unaoanisha kile kinachozungumzwa katika Muswada na kile ambacho kitafuatiliwa katika utekelezaji kwa maana ya kanuni.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema pengine Muswada huu unahitaji muda zaidi au vipi sielewi. Lakini kwa kweli ingekuwa bora zaidi Mheshimiwa Mbunge anapochangia anaangalia utekelezaji utakuwa wa namna gani kwa kutumia kanuni zipi na je, zinafungamana na zinawiana na maana na maudhui ya Muswada wenyewe au sivyo. Sehemu ya pili, katika sehemu hii ni ile ambayo inaonyesha taratibu au masharti ambayo yatafanya maghala yapewe leseni.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia haya masharti vipengele vyote vile kwa kweli yale maghala tuliyonayo vijijini kwangu kuna ghala pale Kidenge, Kibakwe, Pwaga, Rudi

ukiangalia yaliyoelezwa katika Muswada huu maghala haya kwa mujibu wa masharti haya yanakosa sifa ya kuwa maghala ya kupewa leseni. Kwa mfano, kifungu cha 18(c) kinasema: "Mwombaji wa leseni awe ni Meneja au Mkurugenzi." Sasa kule vijijini Mkurugenzi na Meneja watapatikana wapi? Aweke bima ghala lake, kule vijijini bima inatoka wapi? Mwombaji wa leseni aweke *bond* ambayo itambana afanye yale yanayo kusudiwa katika sheria. Hata kama ni kikundi hiki cha wanaushirika wanataka kupata leseni kweli *bond* hii ambayo inatakiwa hawa wakulima wadogo wadogo wapataje hii *bond.*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ninachotaka kusema ni kwamba maghala ambayo yapo kwa wakulima wadogo wadogo vijijini hivi sasa hayatakuwa na sifa bila ya Serikali kusaidia kuyaweka katika hali ya kupata sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nashauri kwamba Wizara ifanye tathmini ya maghala yote yaliyopo vijijini na itenge fedha za kutosha kuyaweka katika hali ya kutumika. Aidha, kuweka utaratibu wa kuunda usimamizi wa namna fulani ambao utakuwa na utaalamu kama wenzangu walivyosema. Lakini usitegemee mkulima mdogo akapata ghala lenye sifa katika vijiji vyetu kwa hali ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini siyo tu Wizara ifanye tathmini ya maghala yaliyopo lakini iangalie mtawanyiko wa maghala yaliyoko vijijini na kuona umuhimu wa kujenga mengine mapya. Kwa sababu kama mfumo huu unatakiwa uende nchi nzima, basi kuna haja ya kwenda huko kuhakikisha kwamba watu wote wanafaidika na mfumo huu. Katika kujenga Serikali inaweza ikajenga yenyewe au inaweza ikashirikisha sekta binafsi chini ya usimamizi wa Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano, inazungumzia stakabadhi zenyewe na ukiangalia sehemu hii madhumuni ya stakabadhi za mazao kwa mujibu wa Muswada huu ni kuhakikisha ongezeko la uzalishaji wa bidhaa zenye ubora na madhumuni ya pili, ni uwezo wa kutumia bidhaa hizo kuongeza mtaji wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza ubora wa mazao kwa kutumia stakabadhi halikujitokeza wazi wazi katika Muswada huu. Hakuna vifungu katika Muswada huu vinavyoonyesha waziwazi ubora wa mazao utakuwaje kwa kutumia stakabadhi za mazao. Mimi ningependa ama hapo mwisho Mheshimiwa Waziri ajaribu kuviainisha tuvione wazi wazi. Lakini kilichokuwa wazi wazi kabisa hapa ni namna stakabadhi za mazao zinavyoweza kutumika kupata mikopo kutoka benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamekwishasema kwamba suala la mkulima mdogo kupata mkopo benki linaweza kuwa lisimpe ahueni huyu mkulima tuwe na tahadhari na jambo hili. Kwa sababu kama wenzangu walivyosema mkulima anachotaka ni fedha kwa mazao yake na siyo akaweke mazao kwenye ghala na badala yake aende benki akakope fedha ili alipe riba.

Mheshimiwa Spika, lengo la kupeleka mazao kwenye maghala ni nzuri na mimi naliunga mkono kwa sababu mbili ninazoziona. Moja, linamuondoa mtu wa kati, lakini la

pili linampa nafasi mkulima kusubiri bei itakapokuwa nzuri. Lakini mimi ninachofikiri kitakachomsaidia mkulima mdogo mdogo ni kuwa na *Organization* ambayo itafanya kazi hiyo na katika nchi yetu *Organization* ambayo inaweza kumsaidia mkulima ni ya Ushirika.

Kwa hiyo, wanapoweka mazao yao kwenye maghala ni sawa sawa na kuweka fedha zao benki. Mazao yanakuwa ni fedha na fedha zinakuwa ni mazao. Wakulima wadogo wadogo wahamasishwe kuunda Benki Mazao. Benki Mazao kwamba wakulima wadogo wadogo wakihamasishwa kupeleka mazao yao kwenye Benki yao ambayo wataisimamia wao wenyewe na watatafuta soko lao wao wenyewe. Uwezekano wa kumwondoa mtu wa kati ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini utaratibu wa stakabadhi za mazao kwa maoni yangu siyo rahisi kumkwepa mtu wa kati anayeitwa mwendeshaji wa maghala ambaye naye ana gharama zake kama wenzangu walivyosema. Mtu wa kati kwa maana ya muendeshaji maghala ambaye sasa tunamuundia sheria alikuwepo lakini sasa tunataka awepo kisheria. Mkulima huyu akitaka kupata fedha kwa mazoea yake atakwenda benki.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme utaratibu wa kupata fedha benki si wa urahisi rahisi kama tunavyofikiri sisi hapa au kama unavyoelezwa katika Muswada au kama tulivyoelezwa katika semina mstari mmoja tu benki kwa wakulima. Ni mlolongo mrefu. Mkulima huyu kwa kweli anakuwa ametoka kwenye kikaango anaingia kwenye moto wenyewe. Anatoka kwa mtu wa kati ambaye alikuwa hajulikani alikuwa anajificha sasa anaingia kwa mtu wa kati anayeitwa muendeshaji maghala ambaye kwa kweli siyo lazima amwekee mazao yake kwenye ghala anaweza akayanunua hata kabla hajayaweka kwenye ghala. Kwa hiyo, ni mtu wa kati yule yule tu kwa maneno mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa nia ya Serikali ni nzuri sana kabisa kama walivyosema wenzangu kwa kutaka kuwasaidia wakulima hasa mkulima mdogo. Lakini mimi nasema tuone jinsi gani Muswada huu unavyoweza kumpunguzia mzigo huyo mkulima mdogo. Mimi nasema sharti la msingi kabisa la mafanikio ya hoja hii ni kumuondoa mkulima kutoka kilimo cha jembe la mkono na cha kujikimu na kuingia katika kilimo cha kisasa na kilimo cha biashara ndiyo jawabu. Lakini kutaka kukusanya mazao ya mkulima huyu mdogo anayetumia jembe la mkono kwamba utamsaidia bado kutakuwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na ile sehemu ya mwisho ya nane ile inayohusu makosa na adhabu. Muswada huu umekuwa mkali sana. Kwa kweli toka nianze kupitia Miswada hapa huu naona umekuwa mkali kabisa umeweka adhabu za kiwango kikubwa na mimi nafikiri makusudio ni kuhakikisha mazao ya mkulima yanalindwa. Kwa hiyo, mimi nimeridhika kabisa na adhabu hizi na ninaziunga mkono mia kwa mia. Ni adhabu ambazo kwa kweli ukitaka kufanya kosa unajitazama mara mbili itakuwaje? *(Makofi)*

Mwisho, pengine nimalizie na jambo dogo hapa ambalo nimewahi kusema huko nyuma Ibara ya saba inahusu nafasi ya Mkurugenzi Muendeshaji. Kifungu kinasema: “Atateuliwa na Waziri na kadhalika.” Mimi ninaomba kiboreshwe kama nilivyoomba

sehemu nyingine kuboreshwa kwamba hawa watu watatu ambao watakwenda kwenye *Board* na baadaye kwenda kwa Waziri watokane na kitu kinachoitwa *Search Committee* inaleta uwazi zaidi katika kumpata huyo Mkurugenzi Mwendeshaji. Katika chombo kikubwa kama hiki kwa kweli ingefaa utaratibu mzuri utumike wa kumpata Mkurugenzi Mwendeshaji ili aweze kuwa na sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema tena kwamba kwa kweli Serikali inajitahidi na katika Wizara zinazojitahidi kumwangalia mkulima Wizara hii imejitahidi sana na inastahili kupata pongezi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. DR CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu hoja hii iliyo mbele yetu. Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri *Sir* George Kahama. Kwanza niseme kwamba Mheshimiwa George Kahama ni mtu ambaye ana sifa nzuri sana katika nchi hii. Kwa sababu hajapata kupewa madaraka akashindwa kufanya vizuri na watu ambao mara nyingine wanatania watu wazima wajifunze kwa Mheshimiwa George Kahama. Mheshimiwa George Kahama ni mtu mzima lakini anafanya kazi kuliko baadhi ya vijana. Kwa hiyo, tunakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hayo, ningependa kusema mambo yafuatayo, la kwanza, naunga mkono Muswada huu.

La pili, ningependa niseme kwamba tatizo ninaloliona mimi na ambalo litaendelea kuwa tatizo kama halikupewa umuhimu ni kwamba hivi sasa Wizara ya Kilimo na Chakula wala Wizara ya Ushirika na Masoko hawajafanya juhudi ya kutosha ili mkulima wa Tanzania naye aweze kujua gharama ya kuzalisha mazao yake. Kwa sababu wakulima wetu wanalima na kutoka jasho bila kujua hasa kwa kila gunia moja la kilo 100 amegharamia shilingi ngapi ili anapoliuza ijulikane kama amepata faida. Sasa mimi naomba tuanze hapo. Mambo mawili, kwanza, wakulima wetu wafundishwe namna ya kujua gharama ya uzalishaji wa mazao yao na pili, mafunzo ya ubora. Kwa sababu kinachoweza kusaidia kupata bei nzuri na huu utaratibu wa maghala kuwa mzuri ni ubora wa mazao ya wakulima.

Lakini pia ubora wa mazao ya wakulima utategemea aina ya mbegu ambayo tunapata. Nchi nyingi tunazopakana nazo wamefanikiwa sana katika kuhakikisha kwamba wakulima wao wanapata mbegu bora. Sisi Tanzania asilimia 98 ya wakulima wanapanda mbegu ya kuokota wenyewe. Hakuna maendeleo ya kilimo wala uzalishaji mbegu bora na kwa kiwango kikubwa hii imetokana kwa sababu utafiti katika nchi yetu unazidi kudidimia. Kilimo ni sayansi na maana yake ni utafiti. Sasa utafiti hapa kwetu hamna, kwa hiyo wakulima wetu wanaendelea kulima kama vile walivyolima karne za nyuma zilizopita. Sasa mimi naomba jambo hili Wizara hii isaidiane na Wizara wenzao ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hayo ningependa tu niseme Muswada huu mzuri yako mambo ambayo nadhani ingekuwa vizuri Wizara waanze kuyawekea alama kwa sababu sisi tumeyawekea alama kwa sababu baadhi ya maeneo hayo tuna mashaka nayo kwamba yasipoangaliwa tunaweza kuleta madhara. Shaka namba moja na ambayo ningependa kuomba ni kuwa Ushirika tulizozijua walizoanzia akina Mheshimiwa George Kahama hazipo leo. Kwa sababu kwanza hakuna mafunzo ya kutosha kwa Maafisa Ushirika na wasaidizi wao wala hakuna vyama vinavyofundisha ma-*secretary* kujua kazi ya Ushirika. Kwa hiyo wasi wasi wetu hivi ni kwamba hata kwa kazi hii ya maghala tunaweza tukafungua maghala mengi lakini hakuna watu ambao wamesomeshwa kwa kazi hii. Maana hii ni kazi sio habari ya kuchukua mtu kwamba nenda kakae stoo uwe unapokea mazao ya wakulima. Ni suala linalohitaji mafunzo ili watakaofanya kazi hii waweze kuleta mafanikio.

Katika Muswada wenyewe ibara ya 54 kifungu kidogo cha kwanza wale mliyonayo mnaweza kwa urahisi mkasoma ile karatasi tulioletewa jana ya mabadiliko. Hapa inazungumzia habari ya *operetor* kupata mapato. Kifungu cha (a), (b), (c ) na (d) vya aya ya 54(1) mimi vinanipa wasi wasi. Kwa mfano ukisema *all off charges for storage and preservation of goods,* nani ata-*determine* hii. Nani atakayesema *charge* hii ndiyo halali. Maana mkulima anawekwa kando, *operator* ndiye ata-*determine* haya.

Sasa mimi nauliza swali, kwa nini mtu mmoja atakayepokea ndio apewe uwezo wa kusema gharama zake ni hizi. Hakuna kikao cha ghala kinachowahusisha wakulima kitakachobishania kuhusu gharama. Hivyo hivyo *loaf claim for money advance, interest, insurance, transportation, labour, weighing* vyote hivi atapima *operetor,* sasa mimi mkulima nina nafasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vifungu vyote hivi amepewa mtu mmoja. Mimi nauliza tusipoangalia utaratibu huu unaweza kuwa mzuri kwa jumla lakini ndani kukawa mwanya kwa watu wachache kuwanyonya wakulima. Kwa hiyo, mimi napendekeza tutazame mfumo kwa maana ya ushirikishi nani watakaoshiriki katika kupanga haya asiachiwe mtu mmoja. Vile vile nataka niseme kwa msingi huo huo tunaomba kwa sababu suala hili ni la ukombozi kwa wakulima tunaomba safari hii Bodi itakayoundwa izingatie kuwemo wakulima wanaohangaika kule wasichukuliwe ma-*technical cooperative* waliosema *theory* ndio waongoze Bodi hii. Maana lazima tuzungumzie maslahi nani hasa mwenye maslahi ni mkulima. Kama ni mkulima wako watu waliosoma wanalima huko Vijijini *retired* wasaidie.

Vile vile Wabunge wengi hapa ndani akili yao yote sasa ni kwa mkulima hizi Bodi zikiundwa wanawekwa wasiohusika na ukulima. Hata Tume mara nyingine mtu anachagua Kamati ya kuchunguza kilimo wanawekwa watu ambao hawajapata kulima hata nyanya. Hawana hata mashamba, wanaingia kwenye Kamati za kuchunguza kupendekeza kilimo. Ndiyo maana zote zinakuwa ni karatasi tu na wanapata posho bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme jambo lingine suala la soko litakuwa pia sehemu ya msingi wa ghala. Maana haiwezekani mkulima akapeleka mle na *operetor* akarundika tu bila soko. Kwa hiyo, naomba soko linapotafutwa bei inayopatikana

wakulima wa eneo hilo wa mazao wanayohusika watangaziwe. Isiwe siri wenye mazao walioweka wajue kwa sababu inawezekanaje wakapata malipo ya kwanza na ya pili kama hawajui soko walikouza mazao yao. Kwa hiyo, lazima ijulikane isiwe siri, kuwe na uwazi katika soko la mazao ambayo wakulima hawa wataweza kuuza.

Mheshimiwa Spika, sina mambo mengi nilitaka niseme hayo ila la mwisho ambalo ningependa kumalizia ni lile alilosema Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga. Mimi nakubaliana naye kwamba uchunguzi ufanyike nchi nzima kujua maghala yaliyopo. Maghala yaliyo Vijijini yabakie maghala ya Serikali za Vijiji au yabakie ya Ushirika zinazohusika katika maeneo haya. Ikitokea Serikali ikifanya juhudi kwa mfano kama hizi juhudi anazofanya Mheshimiwa George Kahama za kujenga masoko kama hilo moja limejengwa hapo njiani tunapopita yahusishwe Vyama vya Ushirika vya maeneo yale sizitafutwe fedha ya kujenga maghala ya watu binafsi. Yawe ama ya Vijiji au ya ushirika. Hii ndiyo itakuwa njia bora ya kujenga ushirika.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutoa wito kwamba kwetu katika Mkoa wa Rukwa Serikali kwa kushirikiana na Wajerumani tulipata fedha ya kujenga maghala. Tumejenga maghala mengi Vijijini. Wakati ule yalikuwa ya ushirika baadaye baada ya chama chetu cha ushirika kufa tukakubaliana kuyakabidhi maghala yale kwa Vijiji. Wakati Mheshimiwa Waziri anaingia Serikalini kule kwetu Maofisa wa Wizara yake walianza kuuza maghala. Tukazuia mimi mwenyewe nilimpelekea ujumbe kwa *fax* akasema naagiza Mkuu wa Mkoa azuie maghala yasiuzwe. Lakini ningependa Mheshimiwa Waziri ajue kwamba katika maghala haya yaliyozuiwa baadhi ya maghala, maghala mawili yalishauzwa na moja ni la Kijiji cha Myangalua mpaka leo Serikali imeshindikana kumrudisha lile ghala kwa wananchi na fedha hazijulikani zilikwenda wapi. Ushahidi tulionao ni kwamba yule Ofisa wa Ushirika aliyeuza lile ghala kwa mtu binafsi aliingiza fedha mfukoni.

Sasa mimi naomba Mheshimiwa Waziri ghala hili lirudi kwa wanakijiji haraka iwezekanavyo kwa sababu kuna siasa katika ghala hilo. Watu wengi wanaamini kama wewe unapenda ushirika. Wewe ni mtoto wa ushirika ulizaliwa kwenye ushirika. Kwa hiyo, tunakuomba utusaidie ghala hili lirudi kwa wakulima na maghala yote ya Rukwa sisi hatutaki wapewe watu binafsi tunataka yabakie kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, *Sir* George Kahama. Nampongeza kwa dhati kwa sababu yeye kwanza ni mtu aliyebobea sana katika masuala ya ushirika na masoko. Kwa hiyo, nampongeza sana na kazi hii ameifanya kwa dhati kabisa tangu enzi za ukoloni na leo hii

bado anaendelea na utaalamu wake huo na ni vizuri akautumia vizuri kusaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Vile vile napenda nimpongeze Naibu Waziri amesomea Vyama vya Ushirika, *profession* yake ni *Cooperative Inspector* ambaye mambo yake ni ya ushirika kabisa. Watu hawa ni wazuri kabisa katika Wizara hii ya Ushirika na Masoko na ninawatakia wafanye kazi vizuri ili kuweza kutusaidia katika suala hili zima la ushirika na masoko. Wote ambao wanahusika Katibu Mkuu na wasaidizi wake napenda kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nasoma na kupitia Muswada huu nilikuwa nafikiria kwamba hasa kwa suala la stakabadhi na maghala ambayo wameyatamka. Nilikuwa nafikiri labda kama alivyosema ndugu yangu Dr. Chrisant Mzindakaya labda hakuna utafiti unaoweza kufanyika vizuri, tuna upungufu wa watu wanaoweza kufanya utafiti na kuweza kubaini mambo ambayo yanaweza kusaidia au yanaweza kuchafua hoja ambayo inaweza ikatungiwa sheria. Hili ningeiomba iwe kabla ya hoja kuletwa Bungeni utafiti uwe wa kina kuweza kusaidia Waheshimiwa Wabunge wanapojadili hapa lakini mambo mengi ya kitaalamu yameshapitiwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ningependa nizungumzie suala la zao la pamba. Zao la pamba lina masharti kumi mpaka ukitaka ufanikiwe lazima uyajue hayo masharti ya zao la pamba. Usipoyajua basi utakuwa na tatizo na wakati unaandaa hivyo lakini unajua kwamba kuna gharama zake na hasara zake.

Kwanza zao la pamba lina masuala ya pembejeo na ni gharama lazima uyakabili. Siku hizi kuna tatizo la mbegu nazo zinatakiwa ziwe mbegu bora nalo uliangalie na zina gharama vile vile. Uandae shamba kuna gharama, ulime gharama, kuna kung’olea kupunguza miche katika kila shimo ni tatizo, palizi pengine mara mbili au tatu, upulizie madawa ya kuua wadudu ni gharama, uvunaji una gharama, kuchambua pamba kama *AR* na *BR* nako kuna gharama zake. Sasa inafikia hatua ya kusafirisha hayo mazao kuyapeleka ghalani kama anavyosema vile vile kuna gharama za kusafirisha. Kuyapeleka kule unakoyapeleka lazima kuwe na gharama. Pale ulipoyatoa mazao kuna ushuru wa Kijiji. Ukitoka pale tena kuyaweka mazao hayo ghalani kuna gharama zake. Kuna Bima, masuala ya riba katika Mabenki sasa yote hayo yanamlenga mkulima na mkulima huyu ni mkulima mdogo mdogo, sio mkulima ambaye ana uwezo wa kuweza kuhimili yote hayo.

Mheshimiwa Spika, unapopeleka mazao yako hayo una imani kwamba lini utalipwa fedha zako. Tukumbuke kwamba hili ni suala biashara na mazao tunayoyauza tunayopeleka nje ya nchi ni mazao ya biashara. Sasa mkulima kama huyu wa zao la pamba kwa kufuata masharti ya kilimo bora ameanzia mwezi wa Novemba, Desemba anashughulika na zao hilo, Januari, Februari, Machi, Aprili, Mei anaanza kuvuna na Juni anatakiwa kuuza mazao yake hayo. Anayapeleka kwenye ghala ambalo linakusudiwa nako anayaweka tu bila kulipwa. Aanze pengine kufuatilia hayo mazao siku hadi siku mpaka atakapopewa hizo fedha. Hizo ni gharama kubwa sana. Sasa kwa muda wote huo pengine fedha mpaka mwezi Oktoba tena, shida nyingi zimemkabili.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba hapa hapakufanyika utafiti wa kina wa kuweza kusaidia mkulima huyu mdogo mdogo, gharama hizi ukizifanya ni mkulima ambaye anapata hasara kubwa sana mara tatu. Pesa zake alizotumia na nguvu zake na uwezo wake wote huo ni hasara tupu. Hatujamsaidia mkulima huyu tunayemtegemea tumsaidie.

Mheshimiwa Spika, kwa hili mimi pamoja na kwamba wenzangu hapa ni wazoefu, wataalamu waliobobea mimi nahitilafiana nao kwamba mimi siwezi kuridhika na utaratibu huo. Nilikuwa narudi tu kwamba labda tuendelee na utaratibu wa zamani. Mzee George Kahama alipambana na watu tuliokuwa na soko huru. Wakoloni wale walikuwa wanatumia taratibu zao na si vibaya kutamka tulikuwa na Wahindi. Wahindi ndio walikuwa wameeneza sera zao hizo za biashara na ma-*ginnery* yote kama ni Kanda ya Ziwa walijenga Wahindi.

Mheshimiwa Spika, walikuwa ni soko huru kwa sababu Muhindi ananunua zao la pamba pale na Mwafrika ananunua zao la pamba pale wanashindana, lakini alikuwa anatumia mbinu zake. Anapoona kwamba anataka kuzidiwa alikuwa anachukua fedha mfukoni anazimwaga, watu wanaanza kugawana pale huku anaendelea kupima kuwapunja wakulima anawapunja na zinamwagwa tena nyingine anazidia tena kupunja mpaka hapo mwishowe watu wakagundua. Mheshimiwa George Kahama ndio alituondoa katika hali hiyo mbaya ambayo ilikuwa ni mbaya kweli na tukapata ushirika. Kwa sababu waliweza kuomba Bodi ambazo zilikuwa zinanunua mazao mbalimbali katika soko la dunia. Nao wakawa wanaletewa fedha zao. Utaratibu ulikuwa mzuri mno.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Kununua Mazao katika soko la dunia ni zaidi ya 150. Utaratibu tuliokuwa tunakwenda au mnawaita mnaelewana nao mnazungumza mnawekeana mikataba kabla hata ya kulima zao la pamba. Mnakubaliana kwamba mwaka huu mkulima zao na mkiniletea tani kadhaa mimi nitawanunulia kwa bei ya shilingi kadhaa. Tunatangaziwa kabla hata ya kuanza kulima. Tulikuwa tunalima kwa njia ya kufahamu bei utakayouzia zao lako hilo. Inapofika wakati huo tunatumia utaratibu wa kalamazoo kutunza rekodi zote za mtu aliyeuza mazao pale *AR, BR* zinakuwa na kalamazoo zake na zinafungiwa kwenye *safe.* Kama ni malipo yalikuwa yanagawanywa mara mbili. Kama ni shilingi 350 au 370 utalipwa malipo ya kwanza shilingi 250 pengine, baada ya mazao hayo kuyasafirisha unalipwa tena malipo ya pili ya shilingi 120 na ulikuwa utaratibu mzuri sana mkulima alikuwa ananufaika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, leo mtu unachukua mazao usilipwe usubiri wakati wowote ambao huelewi, kwa kweli kinasikitisha. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri nisingependa niwaunge mkono kwa suala hili. Ni bora tukaanza tu mtindo wa zamani wa kuungana kwamba tutafute zile Bodi ambazo zinanunua mazao mbalimbali kwenye soko la dunia. Soko la dunia ni moja tu sio kila nchi yamezagaa masoko ya dunia, ni moja tu. Ukishawapata wale wanaonunua mazao kwenye soko la dunia mnaafikiana mnapanga mkataba. Wanakuja mkulima mdogo mdogo anatakiwa auze pamba kama ni zao lake la biashara alipwe *cash.* Sio kuanza tena kusumbuka kufuata risiti zake au stakabadhi zake

kwenye ghala, ilikwenda wapi, ilikwenda lini mwingine anapoteza pamba inaungua moto inafanya nini, mambo ya Bima tena muanze kukadiria ni jambo tofauti kabisa.

Hata hivyo wakati ule wanafanya hivyo Mzee George Kahama kulikuwa na utaratibu wa kufundisha wakulima na wanaushirika . Sasa hivi elimu ya ushirika haipo. Wale ambao wanakaa kwenye *society* fulani kwa mfano sasa hivi wanakuwa watu kumi au ishirini pale si wanaushirika hasa, wao wenyewe vile vile wanauzia mazao kwenye *society* nyingine au kwenye soko huru hawauzii pale. Kwa hiyo, hakuna hata cha mapato wala nini sijui wamekaa tu pale kusubiri kuwanyonya wakulima wengine kwa sababu hawana elimu. Suala la elimu katika Vyama vya Ushirika halipo. Linatakiwa litiliwe nguvu watumishi wenyewe wapate mafunzo hayo na mara nyingi hata mimi nilikwenda Moshi mwaka mmoja unajifunza masuala ya Vyama vya Ushirika. Wakati nakwenda pale tunajifunza Mzee Kahama ndio mwanzilishi na tena unajifunza kabisa Mzee Kahama usipojua hilo kwenye mtihani unashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Marehemu Mzee Paul Bomani, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi pamoja na Mzee Kasambala walikuwa waanzilishi wa Vyama vya Ushirika, unakwenda Moshi kujifunza Vyama vya Ushirika. Sasa hayo yameisha na walikuwa wanaeneza sera nzuri, elimu nzuri ya Vyama vya Ushirika. Leo hii kukosekana hata tukipata namna hiyo ya kwamba tufuate taratibu za stakabadhi kwa vyovyote vile hakuna mtaalamu ambaye anaweza kuhimili matatizo hayo. Hatuna mtaalamu kabisa. Ukienda ufanye ukaguzi, wakaguzi wenyewe wengine hawana taaluma ya ukaguzi. Anakwenda kukusanya vitabu vya ma-*secretary* anakwenda nyumbani kwake, taarifa hatoi. Lakini kwa utaratibu inavyotakiwa asahihishe pale pale akimaliza atoe taarifa yake kwenye Halmashauri hiyo inayohusika kwenye chama cha msingi kwamba mna kasoro hizi, mna tatizo hili au mmefanya kazi vizuri. Halipo hilo sasa hivi, watu tu wanabaki kwamba vitabu vyetu vimepelekwa ukaguzi wanafuatilia kwa fedha, wakaandikiwe taarifa nzuri lakini huku wana hasara.

Mheshimiwa Spika, hilo nilikuwa nafikiri kwamba wangerudisha utaratibu wa zamani ili mambo yaweze kuendelea. Elimu kwanza kwa wanaushirika, elimu kwa watumishi wa ushirika na utaratibu wa kupeleka stakabadhi mimi siuelewi. Nashukuru sana naishia hapo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na tahadhari ya kutorudia hayo yaliyokwishazungumzwa ili nisiyazungumze tena. Lakini kwa sababu Muswada pia unafanana kuna maeneo ambayo hatutakwepa kuyarudia naomba mnivumilie kwa hilo na wenzangu watakaokuwa wananisikiliza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi naomba kwa sababu ndio nasimama kwa mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu kuchangia, naomba niungane na wenzangu kutoa salaam zangu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria pamoja na wapiga kura wa Jimbo la Rahaleo, Zanzibar kwa msiba huu uliowapata wa mzee wetu. Naomba Mwenyezi Mungu aweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Lakini pia nichukue fursa hii pia kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Mzee wetu Balozi Paul Bomani ambaye pia ametutoka katika siku za karibuni na hasa ukizingatia kwamba ndio wazee wetu ambao waliingia kwenye Bunge la kwanza katika Serikali yetu. Kwa hiyo, naomba Mwenyezi Mungu pia aweze kumrehemu aweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni Muswada kwa kweli ni mzuri lakini wasi wasi wangu ambao unanifanya nizungumzie ninayokusudia kuzungumza ninapata wasiwasi kwamba maandalizi ya kutumika kwa sheria hii bado hayajatosheleza. Kwa sababu lengo la Muswada huu au sheria hii ambayo tunakusudia kuipitisha ni kuwawezesha wakulima wadogo wadogo waweze kupata kipato au kuboresha uchumi wao. Lakini sina hakika kwamba tunapomzungumzia mkulima mdogo mdogo tunamaanisha nini. Nirejee tu pale ambapo tunaweza kuwa na tofauti mmoja akaona hizi ni kokoto mmoja akaona huu ni udongo. Kwa hiyo, hata tunapomzungumzia mkulima mdogo mdogo hivi tumefanya maandalizi ya kutosha huko waliko wakulima wadogo wadogo ambao tunakusudia sheria hii iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa najaribu kutazama kwamba sasa hivi tunazo Bodi za Mazao. Nilikuwa natazama Bodi ya Korosho, Bodi ya Pamba, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pareto, Bodi ya Chai. Hizi Bodi ndizo ambazo zina maghala tunayozungumzia ya kuhifadhi haya mazao ya mkulima. Lakini tunapozungumzia maghala kwenye Vijiji hatuna maghala ya namna hii ya viwango hivi ambavyo tunavizungumzia katika sheria tunayokusudia kutunga. Sasa leo tunazungumzia kutengeneza Bodi nyingine iweze kuungana na Bodi hizi na Bodi hii kazi yake kubwa itakuwa ni *administration* kwa sababu hawana miundombinu ambayo ndiyo tunaizungumzia kama kitu cha msingi kabisa kwenye hii sheria. Maana kama tunazungumzia maghala hizi Bodi za Mazao ndio zenye hayo maghala ambayo yanakidhi viwango hivyo vinavyozungumzwa na sheria hii.

Kwa hiyo, sheria ni nzuri, lakini nadhani pamoja na kwamba tunakusudia kuipitisha bado Serikali itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba huu muundombinu wa maghala katika Vijiji ambako ndio waliko wakulima wadogo wadogo tunaowazungumzia basi upangiwe mpango wa kuboresha hiyo miundombinu kwa maana ya maghala ambayo yatatumika kuhifadhia mazao ya mkulima.

Mheshimiwa Spika, lakini ukichukulia hali tuliyonayo sasa hivi hayo maghala yako wapi na mkulima yuko wapi. Kinachotokea hapa ni kwamba wakulima wako mbali na haya maghala watatoka itabidi wasafirishe mazao yao kuja kwenye haya maghala na kuanzia hatua hiyo ambapo mazao haya yatakuwa yanapokelewa zitaanza kuongezeka gharama ambazo gharama hizi sina hakika kama mkulima wetu ataweza kuzikidhi. Tumezungumzia suala la umuhimu wa wakulima wapate hiyo *collateral* ya kuweza kukopa Benki wanapofikishwa mazao yao kwenye mabohari.

Mheshimiwa Spika, zamani wakati wa Vyama vya Ushirika vikiwa vina nguvu kulikuwa na Benki hii ambayo sasa ni *CRDB Limited* wakati huo ikiitwa Benki ya Ushirika nadhani ilifanya kazi nzuri kwa wakati huo. Lakini leo hii ukizungumzia

kwamba Benki ambazo zimekubali kuingia kwenye mpango huu wa kukopesha wakulima Benki tatu kwa maana ya *CRDB, Exim Bank* kama tulivyoelezwa *Exim Bank* ina matawi matatu katika nchi nzima. Ukizungumzia Benki ya *Exim* nadhani wana matawi Dar es Salaam, Tanga na Mwanza. Sasa unapozungumzia kutunga sheria inayotakiwa kufanya kazi katika nchi nzima basi walengwa sio Watanzania wote kuna kundi tu la eneo fulani ambako sheria hii inatakiwa kuwanufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unazungumzia Benki ya Kilimanjaro, Benki ya Kilimanjaro ina tawi kwenye Mkoa wa Kilimanjaro tu haina tawi Mwanza, Mara au wapi, sasa unaiweka kwamba ndio Benki ya mfano kwamba hii itakuwa miongoni mwa Benki zitakazokopesha wananchi. Kuna Benki ya *CRDB* vizuri ina matawi ya kutosha kwenye Makao Makuu ya Mikoa lakini inafika kwenye maeneo mengine ya Vijiji?

Kwa hiyo, mimi nilichotaka kusema ni kwamba bado suala la kuzungumzia umuhimu wa kuwepo Benki ya Wakulima na Benki ya Ushirika kwenye mfumo mzima wa uchumi ili kuwasaidia wakulima ni suala la msingi. Kwa sababu kama hatuna Benki ambayo itakuwa inaweza kuwahudumia wakulima na ushirika wazo la kusema tunafufua ushirika katika mazingira ya ushindani ya Kibenki katika Benki hizi tulizonazo tutakuwa tunawaongopea wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuzungumzia ubora wa mazao kwamba tunazungumzia moja ya madhumuni ni kuhifadhi yale mazao kwenye maghala kuyaongezea ile thamani. Lakini pia mazao yale yawe katika ubora unaotakiwa na Mabohari yawe katika ubora unaotakiwa. Sasa nilikuwa nasoma kwenye Ibara ya 28 ya sheria hii. Katika ibara ya 28 wamezungumzia suala la kwamba Bodi itakuwa na uwezo wa kuteua Wakaguzi wa Mabohari na ubora wa mazao.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nadhani kitu cha msingi hapa ni hawa Wakaguzi wanatamkwa na sheria lazima tuwaelewe ni Wakaguzi wenye sifa zipi. Maana kama haikutamkwa kwenye sheria labda kama Mheshimiwa Waziri atakuja na kanuni ambazo atazionyesha kwamba kwenye kanuni atatoa sifa hizo za hawa *Inspectors* wasi wasi wangu ni kwamba tunaweza kujikuta tunakuwa na Wakaguzi au Mainspekta ambao hawana sifa za kuweza kukidhi hii kazi ya ukaguzi wa Mabohari haya pamoja na ubora wa mazao.

Mheshimiwa Spika, maana hapa kuna vitu viwili kwamba ukiwa na mkaguzi, unakagua nini, unakagua ubora wa *godown* au unakagua ubora wa mazao? Kwa sababu hapo wanatakiwa wawepo watu wenye taaluma mbili tofauti. Huyu anayesimamia ubora wa bohari ni mtu wa ugavi, lakini anayekuja kusimamia ubora wa mazao anatakiwa awe na taaluma ambayo inaendana na shughuli za kilimo. Sasa hapa sheria haijasema hawa ma-*inspector* watatakiwa wawe na taaluma ipi. Kwa hiyo, nadhani ingeelezwa wazi kwamba ni taaluma ipi inayotakiwa ili hawa ma-inspector waweze kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Ibara ya 26 imetoa uwezo wa bodi kuweza kufuta leseni kwa wale *operators,* lakini haijaeleza pale ambapo *operator* atakuwa hajatendewa haki ana-*appeal* wapi maana hiyo ndiyo haki ya msingi wa mtu kwamba bodi kama

imepewa uwezo wa kufuta leseni je, huyu ambaye atakuwa anaona hajatendewa haki aende kulalamika wapi baada ya kuwa amefutiwa leseni yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia nadhani wenzangu wamelizungumzia ni suala zima la elimu. Nadhani katika kuwahusisha wananchi na hizi sheria ambazo tunapitisha Bungeni nadhani wadau kwa Wizara husika ingeanza kutoa elimu huko kwa wananchi kama walivyozungumza wenzangu ili tunavyokuja kujadili sheria, basi tayari wale wadau wanajua hii sheria itawanufaisha vipi. Kwa ujumla Muswada huu ni mzuri lakini bado ni wajibu wa Serikali kwenda kuboresha miundombinu kwa maana ya ujenzi wa maghala katika maeneo ya vijiji ambako ndiyo waliko wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nina hakika sikurudiarudia maneno yaliyokwishazungumzwa na wenzangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa naomba nitamke wazi kwamba hoja hii naiunga mkono ni hatua ambayo itatusaidia katika kupunguza makali ya ununuzi wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba kusema kwamba Baba wa Taifa aliwahi kusema kwamba ukitaka kuongelea umaskini lazima uongee na maskini *(if you want to address poverty you must address the poor).* Sasa sidhani jinsi gani Wizara imewahusisha wakulima katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka nitambue tu kwamba Mheshimiwa *Sir* George Kahama ni muasisi wa Vyama vya Ushirika, ukiwakumbuka vile vile Marehemu Paul Bomani, Eliofonkya, wakina Kasambala, hawa ndiyo walisaidia hata kupata uhuru wa nchi yetu ya Tanzania. Vyama vya Ushirika vimesaidia mambo makubwa sana na tukivibeza na vikafa basi tutakufa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba sheria hii ninaamini kabisa kwamba ni sheria ambayo imeletwa ili tuboreshe Ushirika wetu na vile vile tutatue matatizo ya kutolipwa wakulima. Sheria hii ni nzuri na ni akiba kwa mambo yajayo hasa mimi niseme kwamba sheria hii itawasaidia zaidi wanunuzi wa mazao wakubwa. Watanunua kwa wakulima, halafu mkulima ninaomba awe analipwa *cash. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba ninukuu methali ya Kisukuma inasema hivi: *"Bulekana Mbise Butipungungijaga Misoji,"* (mkigawana mbichi hamuwezi mkalaumiana upungufu wa mchuzi, siyo bwana! Anayetaka kuchoma nyama hewala bwana, ukitaka kukaanga hewala, ukitaka kuweka mchuzi mwingi hewala. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kwa maana hiyo, nasema kwamba mkulima akipeleka mazao yake kwenye chama basi alipwe *cash* ili akafanye analotaka. Akitaka kunywa pombe hewala, akitaka kununua nguo hewala, kila analotaka kufanya hewala. Ninaamini kabisa kwamba sasa

hivi wenzangu wameliongelea kwanza tuna matatizo, kama mnavyofahamu kwamba tuna matatizo ya ku-*control* hizi *documents.* Kama watu wanaweza waka-*forge* noti ukaipokea bila kuijua je, hizi karatasi zitafanana na nini? Ninaamini kabisa kwamba wengine watazi-*forge.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba mkulima alipwe *cash.* Halafu isitoshe mazao ukiyaweka kwenye maghala kuna *(shrinkage),* unyaufu na uzito unapungua kutokana na *moisture.* Sasa tunataka kuanzisha sheria hii kama na kumui-*involve* mkulima tunatafuta namna labda ya kumdhulumu zaidi. Mimi nasema kwamba sheria hii iwasaidie wanunuzi wakuu wanaonunua mazao kama vile vyama vya ushirika. Kwa mfano, tuna wanaonunua pamba sheria hii itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba lingine limeongelewa sana kuhusiana na maghala, mimi la maghala nasema kwamba huko nyuma tulikuwa na utaratibu mzuri wa kuwa na maghala halafu na kuyakarabati. Kwa muda mrefu sana vyama vyetu vya ushirika hasa vya Shinyanga utakuta kwamba maghala yamechakaa sana na hayajawahi kutengenezwa kwa muda mrefu.

Kwa hiyo, mimi nasema kwamba inawezekana kutokana na ubovu wa maghala, mali inawekwa mle ya mkulima halafu baadaye inakuja labda mvua inanyesha na upepo, halafu mazao yale mazao yanaharibika litakuwa ni jukumu la nani? Biashara ya Ushirika pamoja na ya Benki pamoja na insurance ni biashara mama. Ukitaka kukope hela lazima awepo mtu wa *insurance.* Sasa utakuta kwamba *insurance companies* zetu sasa hivi nyingi zimelegalega. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba mkulima alipwe *hard currency.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka niseme kwamba sheria hii, kwa kuwa itahusisha watu wengi na wengine hawajui kiingereza nilikuwa naomba sheria iandikwe kwa Kiswahili, ili watu waweze kuielewa zaidi na kuifanyia kazi na kupunguza matatizo kama tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine napenda kusema ni kwamba yapo makosa ya msingi ambayo tukitaka ushirika wetu ushamiri lazima tutafutie ufumbuzi, kwa sababu tunayo mapungufu mengi, pungufu mojawapo ni kwamba ukienda kule kijijini wanachama wengi utakuta kwamba wanachama na viongozi wengi wa vyama vya ushirika mazao yao wameweka mikataba na kuuza mazao kwa watu binafsi. Halafu bado wanapoitishwa kwenye mkutano wanakuja kwenye mkutano pale, wanakuja kufanya nini kwenye mkutano mkuu wa chama ushirika? Utakuta kwamba hata viongozi wanaochaguliwa wengi wao hawauzi mazao katika vyama vya ushirika. Kwa nini kusiwe na utaratibu hawa watu mkawa-vet na mkawajua na wasiwe wanaruhusiwa kuja kuvuruga mikutano ya wanachama kwenye mikutano mikuu. Sasa hilo nilitaka mlifanyie kazi lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba hawa watendaji wetu lazima wapewe vitendea kazi. Ukitazama kwa mfano Mkoa wa Shinyanga sina uhakika sana kama wako wanne au watano mabwana ushirika. Halafu hata gari hawana. Sasa nilikuwa naomba

watumishi wa ushirika waongezwe na ikibidi hata wale ambao waliacha kazi ambao bado wana nguvu si vibaya wakapewa mikataba ili kusudi wasaidie kuboresha matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba ukitazama kwa mfano kwetu Shinyanga na Mwanza kuhusiana na *ginneries, ginneries* nyingi zimeharibika mno na zimekuwa *run down.* Huko nyuma tulisaidiwa na Wadachi, miaka ya 1980 katika ku-*rehabilitate.* Nilikuwa naomba Serikali itafute hela zake ama za wafadhili ili ku-*rehabilitate* hizi *ginneries* ambazo kwa kweli kama bado ziko vile vile ushirika hatutaweza kuufufua kwa sababu zimekuwa *run down. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu waliotusaidia sana katika ushirika miaka ya nyuma ni *Scandinavian Countries.* Nilikuwa naomba Wizara kama inawezekana wawaombe tena hawa wenzetu wajaribu kutusaidia kufufufa Ushirika wetu. Ninaamini kabisa kwamba ushirika ukifa kule kijijini umaskini utakithiri kwa sababu ukitazama sasa wanaonunua pamba utakuta kwamba wana mapungufu chungu mbovu ikiwemo pamoja na upimaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta jinsi wanavyowapimia wananchi, hawapimi vizuri. Utakuta wakati mwingine na bei wanayotoa si nzuri, utakuta huduma ya pembejeo siyo nzuri. Kwa hiyo, ushirika lazima tuujenge.

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kuwaambia Shinyanga kwamba ushirika ukifa kama nilivyosema uchumi wetu utakufa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Ya kwanza? *Okay thank you. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka kuongelea kuhusu viongozi wa ushirika. Bahati nzuri hili nimelifuatilia kwa Mheshimiwa Waziri, nilikuwa nataka nimuulize kwa sababu huko nyuma viongozi wakuu wa ushirika walikuwa wanajulikana tu pale kwenye mkutano mkuu. Wanaposema sasa hivi tunataka uchaguzi nani anataka uongozi anajitokeza pale, *that was very wrong.* Lakini bahati nzuri amethibitishia kwamba ile sheria wameibadilisha. Sasa hivi watakuwa wanaomba, halafu maombi yao yanapelekwa kwenye Wizara wanakuwa *vetted,* halafu wanaonekana na uzuri wao pamoja na *experience* yao. Wako watu wamepata madaraka makubwa ya kuongoza ushirika, lakini hata ukiona integrate yao, hata ukiona uzoefu wao ni zero. Sasa kwa namna hii tunachangia katika kuua ushirika. Kwa hiyo, mimi nasema nimeridhika sana na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda nishukuru sana na ninaamini kabisa kwamba ushauri wangu Wizara itaufanyia kazi.

Labda la mwisho tu, mimi ninakaa Shinyanga na kwa bahati nzuri nimefanya kazi kwenye pamba kwa muda mrefu, zaidi ya miaka 20, halafu kwa bahati nzuri nilishiriki hata kuianzisha *SHIRECU* wakati naondoka mwaka 1988 *SHIRECU* niliIacha ina nguvu sana. Lakini nashangaa hata siku moja sijaitwa kutoa hata ushauri. *(Makofi/Kicheko)*

Wakati mwingine hata ushauri siyo vibaya kwa sababu *experience is a best teacher.* Mimi naomba wakati mwingine wale ambao tuna uzoefu wa ushirika tunaomba tusaidie kwenye mikutano tu ya kawaida siyo lazima tulipwe, ili tutoe mawazo ya kujaribu kujenga ushirika na kuhakikisha ushirika unaendelea kwa sababu ushirika umetutoa mbali na mpaka sasa leo tunao ukitufia kama nilivyosema umesaidia *contribution* nyingi kwa Baba wa Taifa, akina *Sir* George Kahama hawa ndiyo wame-*contribute* hata nauli, *living cost* kwenye *United Nations.* Kwa hiyo, lazima Ushirika tuulinde ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Leonard Derefa, mashine zetu za *Hansard* zimekataa kabisa kuandika maneno ya Kisukuma. Kwa hiyo, kama unataka yaingie kwenye *Hansard* tuandikie maneno hayo kwenye karatasi umletee Katibu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia Muswada ulioko mbele yetu kama ilivyo kawaida.

Kabla ya kufanya hivyo naomba na mimi nijumuike na Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo aliyefariki, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Pia naomba nitoe rambirambi zangu kwa familia na ndugu wa Balozi Paul Bomani, ambaye pia amefariki siku chache zilizopitwa naye Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tulipofanyiwa semina ya Muswada huu ili tuweze kuelewa kwa kweli kwa bahati mbaya au bahati sijui ya namna gani, sikuelewa vizuri, sikupata vizuri. Kwa maana hiyo, nilipata nafasi pia ya kuchangia, katika dakika tatu nilizochangia kwa kweli nilitokwa na jasho kwa sababu ulionekana kama vile ulikuwa umeniudhi kidogo. Niliona kama wakulima tunakuja kuwadhulumu kabisa kwa Muswada huu. Lakini baadaye baada ya Mheshimiwa Waziri pamoja na watoa mada kujaribu kujibu yale ambayo tulikuwa tumeuliza ili kuelewa nashukuru kwamba walinibadilisha mawazo yangu. Kwa hiyo, leo naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walinibadilisha mawazo yangu kwa sababu moja kubwa, kwanza kwa sababu ya kueleza kwamba taratibu hizi wanazozileta si taratibu zinazokuja kuzuia taratibu zingine zote ambazo zilikuwa zinanunua mazao. Ni taratibu ambazo ni za nyongeza katika kuboresha ununuzi wa mazao pamoja na kumsaidia mkulima taratibu zake anavyokwenda. Sasa hilo kwa kweli limefariji sana na kwa hiyo, nasema naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika kufanya hivyo lazima kuna matatizo ambayo lazima tuangalie taratibu nzima zinavyokwenda ili hatimaye tuweze kutoka na taratibu nzuri zitakazoweza kuwasaidia wakulima wetu. Tunakumbuka kwa kweli wakulima wamepita katika hatua nyingi sana katika kuhakikisha kwamba angalau tunawaboresha

waweze kuwa na mfumo mzuri wa ununuzi wa mazao yao. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza hapa kwamba tulikuwa na ushirika wa zamani tunaoufahamu wa Waheshimiwa Waziri wetu *Sir* George Kahama, Marehemu Paul Bomani na wengine ambao wameuanzisha, ni ushirika ulioshamiri na ambao kwa kweli mpaka sasa tunauenzi.

Lakini kwa kuona labda pengine tunataka tuboreshe zaidi ushirika huo tuliuvunja. Tumekuja kwenye mamlaka za mazao tukafika mahali napo tukakwama. Tukarudisha ushirika tena kwa ushirika tuliourudisha sasa ndiyo umetupa matatizo. Ushirika wa kwanza ambao Serikali iliuvunja ulikuwa ni ushirika kama tungeendelea nao, mimi nafikiri tusingekuwa na matatizo. Lakini kwa bahati mbaya basi maji yalishamwagika na mambo yalikwenda hivyo. Hasa ushirika tuliokuja kurudisha mara ya pili ukawa na matatizo mengi kiasi kwamba pakawa na madeni makubwa kwa watu, ushirika ukafilisika, kila mahali pakawa na matatizo ndiyo ikabidi tena turudi tuje kwenye soko huria ambalo tumeliita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, soko huria pamoja na kwamba linaendelea kufanya kazi, lakini limeonekana nako pia kuwa na matatizo mengi. Matatizo yaliyojitokeza katika soko huria kwanza ni kutokuwa na hata ubora wa mazao, maana watu wanaanza kununua hata mazao yakiwa mashambani. Sasa ubora wa mazao, kidogo ukaenda vibaya. Lakini pia tumeshuhudia sasa hivi bado kuna madeni ambayo wakulima walishauza mazao yao lakini bado wanadai. Sasa hii yote nako ni matatizo. Sasa Mheshimiwa Waziri amekuja na Muswada huu ambao anafikiri pamoja na taratibu zingine hizi, unaweza ukatusaidia katika kumuinua mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kutumia stakabadhi za mazao, ambazo mazao lazima yapelekwe ghalani mimi nauunga mkono lakini naomba Mheshimiwa Waziri, kwanza kabla ya yote elimu kwa wakulima wetu ifanyike. Kama sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, hapa tulifanyiwa semina, lakini bado tukatoka na uelewa wa kuelewa kwamba huu msaada hautatusaidia ni mfinyu sasa je, kwa mkulima itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, naomba basi utaratibu huu hebu uwaendee wakulima waweze kupata elimu inayostahili ili hatimaye pale hata wale ambao watamiliki haya maghala wamiliki maghala, isije ikawa ni dhuluma moja kwa moja badala ya kusaidia, badala yake ikawa ni tatizo tena kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi bado naamini kwamba pamoja na utaratibu huu kwamba uendelee lakini bado naamini kwamba vyama vya ushirika ni muhimu hata katika hili kwa sababu tukiviimarisha vyama vya ushirika vya msingi hasa katika hili ndivyo vitakavyosaidia ukusanyaji wa mazao wa kuunganisha wale wakulima wadogo wadogo ili waweze kushirikiana kupeleka mazao hayo mpaka kwenye ghala. Vinginevyo mkulima mdogo mmoja mmoja hataweza kufanya kazi hiyo ya kupeleka mazao yake kwenye ghala na kupatana na mpaka kwenda kuchukua mkopo kwenye Benki.

Sasa mimi bado naamini kabisa kwamba ushirika kwenye vyama vidogo vya msingi tuimarishe ili uweze kusaidia sana taratibu hizi za kuwafanya wakulima wetu waelewe na hatimaye waweze kupeleka mazao yao kukabidhi kwenye maghala. *(Makofi)*

Lakini pia pamoja na kufanya taratibu hizi za kupeleka mazao haya pia tuangalie tusije tukamuingiza mkulima huyu kwenye gharama kubwa sana tukifikiria kwamba baadaye atakuja kupata bei nzuri. Tunaona jinsi Muswada ulivyozungumzia matatizo mengine kwa mfano usafirishaji, *storage,* mambo ya ufukizaji wa madawa, mambo ya kwenye maghala pale, yote haya ni gharama, lakini ni vipi, Muswada huu unaweza ukamsaidia mkulima ili katika gharama zote mkulima asije akapewa gharama hizo zote na hatimaye baadaye wakati bei imepatikana nzuri na sasa analipwa akajikuta anakatwa sehemu kubwa ya pesa yake ambayo ilikuwa aipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimejaribu kufikiria pia kwamba katika mazao mengi licha ya pamba au kahawa unaweza ukakuta hata pamba yenyewe kuna wakati unaweza ukaiweka pamba kwa mfano wakulima wamepeleka pale, wasipate bei inayostahili na ambao walikuwa wanaifikiria ni kwamba ni bei nzuri watakayoipata kutoka kwenye soko la dunia. Ukakuta badala ya kukaa labda pengine miezi michache, wakakaa mpaka msimu unaofuata.

Mheshimiwa Spika, msimu mwingine wa kuuza pamba ukakuta pamba bado iko ndani. Sasa taratibu hizo zitafanywa nini? Ni vipi tena wakulima watakuja kuleta pamba nyingine. Halafu mkulima atapata wapi fedha tena nyingine, pamoja na kwamba atakuwa amekopa, lakini hii pamba nyingine bado haijauzwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo mkulima huyu atafanywa nini? Maana tumeshuhudia katika miaka mingine unaweza ukakuta pamba kwenye world market ina flad au kwa makusudi pengine wakati mwingine tunachelewa kuvuna na kuuza pamba tunakuta pamba sehemu nyingine ya dunia imekwenda kwenye soko la dunia na kwa hiyo, sisi tukakuta bei imeshachafuka imekuwa mbaya tukasema basi ngoja tungoje, halafu ukakuta msimu mwingine unaingia.

Sasa ningeomba basi Muswada huo labda uweke taratibu nzuri za kutueleza ni vipi tunaweza kumsaidia mkulima likitokea tatizo la namna hii? Hili ni tatizo labda la zao la pamba lakini tunategemea kwamba mazao mengine pia nako yataingia katika mfumo huu kwa mfano mahindi, alizeti ambalo ni zao moja kubwa katika Mkoa wa Singida. Sasa mahindi kama tunavyoona ni kwamba yanakuja kuwa na soko wakati inapotokea njaa. Tena na wakati ule pengine mmeweka mahindi yenu katika maghala haya, hakuna mnunuzi, wala hamuwezi kupata bei katika sehemu zingine, msimu mwingine unaingia, sasa sijui nalo hilo tutasaidiaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hayo mimi ninachosema ni kwamba katika kuimarisha huu mpango tusije tukasahau kuendelea na mifumo mingine kuendelea kuiimarisha tukitegemea huu mfumo peke yake.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kuwasaidia wakulima katika mifumo mingine ya ushirika, katika soko huria ili mkulima asije akakwama pengine kwa upande mmoja huu wa kutegemea. Tumsaidie mkulima ili aondokane na matatizo yake ya kuuza mazao yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya machache ambayo nilikuwa nayo, kwa kweli naomba tena nirejee niseme kwamba baada ya kuelewa huu mpango wa stakabadhi, naunga mkono asilimia mia kwa mia na kwa hiyo, uendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maombi ya kuchangia Muswada huu yalikuwa mengi na hadi sasa bado wafuatao hawajapata nafasi ya kuchangia, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Getrude Mongella. Kwa ajili hiyo, tutaendelea na mjadala kipindi cha mchana kabla Mheshimiwa Waziri hajahitimisha.

Waheshimiwa Wabunge, uzoefu tulioupata ni kwamba Mheshimiwa Waziri akianza kuhitimisha saa 11.00 Bunge linakwisha mapema sana kama saa 12.00 au saa 12.30 kwa hiyo, kumbe anaweza akaanza kuhitimisha baadaye na bado Muswada ukapita katika hatua zake zote.

Kwa hiyo, tumekubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba wataendelea kuitwa wachangiaji mpaka saa 12.00 baada ya hapo ataitwa mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake pamoja na Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, wale niliowataja kama bado wana hamu ya kuchangia tafadhali wawepo kipindi cha mchana. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mchangiaji wa kwanza, napenda niwaarifu kwamba ninaomba niwaarifu kwamba tunao wachangiaji wanane na kwa kanuni zetu kila mmoja akipewa si zaidi ya dakika 15 inatufikisha saa

moja na saa moja hatutakuwa na nafasi ya kumalizia Muswada huu kwa leo. Kwa hiyo, kila mmoja atapata dakika 10 na ukiweka *point* sawasawa nadhani tunaweza kumaliza saa 12.20 ili kutoa nafasi kwa watoa hoja ku-*wind up* na shughuli za Kamati zimalizike leo.

Kwa hiyo, tusishangae kengele zikilia haraha haraka tumetenga dakika saba za kwanza, kengele ya kwanza, dakika tatu za mwisho italia tena. Tumepewa dakika kumi. Kwa hiyo, tunaendelea. Sasa wachangiaji wa kwanza ni Mheshimiwa Mohamed Abdulziz, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Danhi Makanga na Mheshimiwa Nazir Karamagi. Lakini katika hao niliowataja, namwona tu Mheshimiwa Nazir Karamagi, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa wa kwanza adhuhuri hii kuchangia Muswada huu wa Sheria ya kusimamia mfumo wa kutumia maghala ili kutumia mazao kama dhamana ili kukopa katika Benki. Nampongeza Waziri aliyeleta Muswada huu tunaouzungumzia sasa hivi hususan ukizingatia kwamba ni wakati muafaka wakati tunazungumza namna ya kuwawezesha Watanzania walio wengi ili kujiunga na mfumo wa kisasa wa kibiashara duniani.

Mheshimiwa Balozi Kahama, tunajua ni mzoefu katika mambo ya Ushirika na amejifunza mengi kutokana na matatizo ambayo tumekuwa nayo. Tunajua kati ya matatizo ambayo wananchi walikuwa wanalalamikia kwa wingi ilikuwa ni kununua mazao yao kwa kupewa risiti tu bila kupewa pesa taslimu. Wafanyabiashara wadogo wadogo hawakuweza kushindwa kujiunga na mfumo huu. Hii ilikuwa ni kitendawili ambacho kilikuwa kikubwa ambacho kilikuwa kinawakatisha tamaa Watanzania hususan kwa kuona kwamba ni wafanyabiashara wakubwa wakubwa tu wengi ambao ni wageni ambao walikuwa wakifanya hii kazi ambazo kweli hata Mtanzania angeweza kuifanya kama mfumo ungekuwa unaruhusu. Muswada huu unategua kitendawili hicho kwa sababu tunajua sisi sote hapa kwamba pesa zipo nyingi kwenye mabenki lakini ilikuwa ni tatizo kukopesha kwa Watanzania walio wengi ambao hawana dhamana ambazo zilikuwa zinakidhi masharti ya kibenki. Kwa kuweka Muswada huu ambapo mazao ambayo yamewekwa kwenye ghala, ndiyo yatakuwa ni dhamana itakayowasaidia na kuwawezesha Watanzania walio wengi ambao haitakuwa na lazima ya kuwa na kipato kikubwa sana ili kuweza kuingia katika mfumo huu na kufanya biashara inayotakiwa.

Mfumo huu sio mpya katika biashara ulimwenguni isipokuwa ni mgeni tu hapa Tanzania na kwa sababu ni mgeni na tunataka ufanikiwe haraka, ningependekeza mambo yafuatayo yazingatiwe hasa mwanzoni wakati ukianza. Kwanza, kama walivyozungumza Wabunge wenzangu ni elimu kwa Watanzania walio wengi ili kuweza kujua huu mfumo unafanya kazi kwa njia gani na wanaweza kuufaidi kwa njia gani. *(Makofi)*

Pili, ningependekeza kwamba ili ufanikiwe, humo kuna *element* ya gharama za usafiri. Haya maghala yanajaribu kuwa karibu na wakulima ili wasishindwe kutumia huu mfumo kwa sababu ya kushindwa kumudu gharama za usafirishaji. Tunajua kwamba

sehemu nyingi hususan Bukoba Vijijini karibu kila Kijiji kilikuwa kina ghala zikimilikiwa na *Primary Societies.*

Haya maghala yakikarabatiwa yanaweza kutumika na yakawa kichocheo kikubwa ambacho kitakuwa karibu na wananchi na kuweza kuona huu mfumo kweli unawasaidia vinginevyo wataona kwamba ni mfumo unaoambatana na gharama kubwa na utawafanya wachache tu ambao wanaweza kuhimili gharama ndiyo waufaidi, lakini wananchi ambao ndiyo tunawa-*target* wasiweze kuufaidi.

Tatu, kwa kuanzia, najua kwamba *Warehouse Operators* watakuwa ni wachache, kwa sababu ya ule ubora wa *Warehouse* zilizozungumziwa. Kwa sababu watakuwa ni wachache, ni rahisi kufanya ukiritimba wa bei. Kwa hiyo, hizi bei za *Warehouse Operators* kwa kuanzia ziangaliwe. Tunajua kwamba baadaye zikiwa nyingi watashindana wenyewe kwa wenyewe. Lakini kwa kuanzia zinabidi ziangaliwe. Vile vile riba za mabenki zitakazotozwa kwa kuanzia na zenyewe ziangaliwe ili ziweze kuwa nafuu.

Lazima tuangalie kwamba hawa Watanzania, wafanyabiashara wadogo wadogo wakikumbwa na gharama kubwa ya riba na gharama nyingine watashindwa kulipa na mazao yao ambayo wameyaweka kama dhamana ya *receipt* yatanadiwa. Najua wanapoweka dhamana, dhamana hiyo itakuwa ya bei ya chini ya bei halisi ya zao wasije wakapoteza hayo mazao na wakakata tamaa na mfumo huu ambao ni mzuri na ambao unataka kuwakomboa.

Kwa kuhitimisha hoja yangu kwa sababu tunataka kuokoa muda, naomba kwamba Sheria hii, Bodi ambazo zitasimamia Sheria hii isimamie hasa mfumo mzima wa gharama itakayopangwa yule mtu ambaye anaweka mazao kwenye ghala. Kwa sababu ni gharama hii ambayo itaweza kuamua ku-*determine* pesa gani yule mkulima mdogo atapewa wakati mtu ananunua mazao yake. Gharama ya mfumo mzima ikiwa kubwa, itabidi kuiondoa katika gharama yake yote na yule mwananchi ambaye tunamlenga aweze kunufaika kwa bei nzuri.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kutumia Wizara yake asimamie huu mfumo vizuri hususan gharama za mfumo huu wote kusudi mwananchi wetu aweze kupata bei nzuri ambayo ataona kweli hiki chombo, hii Sheria tunayoiweka imelenga katika kumnufaisha. Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru jioni hii kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada wa *The Warehouse Receipts Bill, 2005.* La pili, nichukue nafasi nyingine kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu, kwa dhamira yao nzuri katika Serikali ya kutaka kuboresha hali ya soko la mazao ya wakulima wetu huko Vijijini na Mijini.

Lakini pamoja na dhamira yao nzuri, ningependa kwanza kuanzia na kuangalia hali halisi ilivyo kule kwa wakulima wetu Vijijini. Hali halisi ilivyo ni kwamba baada ya Vyama vya Msingi kushindwa kununua mazao ya wakulima, watu binafsi walianzisha utaratibu wao wa maghala. Huu utaratibu ulishaanza kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, wana maghala yao kule na wakati wakulima wanapovuna mazao yao, wafanyabiashara hao wamekuwa wakiyanunua na kuyahifadhi katika maghala yao kwa dawa, wakisubiri bei nzuri.

Katika msingi huo wafanya biashara hao wamekuwa wakiendesha hiyo biashara kwa njia ya upunjaji kwa ajili ya kupata faida kubwa. Kwa sababu lengo la mfanyabiashara yoyote ni ku-*maximize profit* kwa hiyo wakulima wetu wamekuwa wakipunjika sana. Wakati mwingine walikuwa wanapunjwa kwa sababu wakati wanapotoka katika kazi ya kilimo na kupata mavuno yao wamechoka, wana shida na wafanyabiashara hao wamekuwa wakiwalipa fedha taslimu moja kwa moja wala siyo kwa ajili ya kukopwa. Hivyo, walikuwa wanalipwa fedha taslimu hapo hapo wakiuza mazao yao. Lakini walikuwa wanalipwa kwa bei ya chini.

Wafanyabiashara hao nao wamekuwa katika hali ya wasiwasi kwa sababu walikuwa wanaendesha maghala yao hayo bila ya kuwa na Bima. Wao wenyewe ndiyo *inspectors,* ndiyo wanaofanya ukaguzi, wao wenyewe ndio wanaoweka kumbukumbu za ununuzi wao na ndio walikuwa wanaweka taratibu za kuhifadhi ili mazao yasiharibike na bei inapokuwa kubwa wanauza na kupata faida kubwa.

Katika mfumo wa sasa ambao Mheshimiwa Waziri anatuletea, lazima afahamu kwamba huko tunakokwenda, tunakwenda kukuta watu ambao wamekuwa wakifanya biashara hii. Kwa maana nyingine ni kwamba, itabidi utaratibu huu uweze kuboreshwa vizuri zaidi na wakulima wetu wakaelimishwe kwa sababu wakulima hawakuzoea kupewa risiti. Wamezoea kupewa risiti ya fedha taslimu. Sasa leo akipewa risiti akiambiwa aende Benki, huo mzunguko mzima anauona ni mrefu sana. Wakati mwingine mkulima akishampa kazi ya kwenda Benki labda kwa ajili ya Sh.50,000/= au Sh.80,000/= maana labda mazao yake ni kidogo, anaona ni usumbufu. Anaona kabisa urasimu mzima unamweka katika hali ngumu ya kupanda gari kwenda Benki na kurudi nyumbani kwake, anaona ni usumbufu. Kwa hiyo wafanyabiashara kule wamekuwa maarufu kwa sababu wao malipo yao ni papo kwa hapo.

Sasa mimi ningependekeza kwamba pamoja na utaratibu huu ambapo wakulima wetu watakuwa na nafasi ya kwenda katika mabenki kupata fedha, basi Muswada huu uboreshwe ili wananchi waweze kuwa na hali ya kutokuwa na urasimu mbaya wa kupata malipo yao.

Kule kwetu kuna zao moja linalimwa linaitwa fiwi nyeusi na wanunuzi wakubwa ni Wakenya. Wakenya wanakuja pale Wilayani Same kununua fiwi nyeusi, wanakaa katika mahoteli na vijana walioko pale, wafanyabiashara wadogo wamefungua maghala yao, wao ndiyo wanunuzi, wanapatana bei na Wakenya. Kwa vyovyote vile wanapatania bei ambayo labda ni Sh.7,000/= kwa kilo.

Lakini kwa mkulima wanakwenda kwa mnunuzi kwa Sh.3,000/= mpaka 4,000/=. Kwa maana nyingine wana-*maximize* karibu asilimia 200 mpaka asilimi 300. Kwa maana nyingine ni kwamba wakulima wanapunjika sana kwa sababu vyama vyetu vya ushirika vimeshindwa kushika ile nafasi. Ningeiomba Wizara ichukue tahadhari kabisa, ikiwezekana maghala ambayo yamekuwa yakimilikiwa na Vyama vya Msingi yaendelee kukarabatiwa na Vyama vya Msingi viendelee kufanya jukumu hili la kufanya ununuzi wa mazao hayo na kuyahifadhi na kutoa stakadhi. *(Makofi)*

La pili ni kuhusu Benki. Je, Benki zinaelewa utaratibu huu mzima? Ninafahamu mfano mmoja ambao na Mheshimiwa Waziri anaujua wa kule kwetu ambapo Chama chetu Kikuu cha Ushirika cha *VUASU* kiliomba kupata mkopo wa Lori la kubebea zao la kahawa kutoka kwa wakulima kwa mpango wa *Export Credit Guarantee Scheme* na Wizara yake ikaandika barua Benki Kuu na Wizara ya Fedha ikaandika barua Benki Kuu na barua zile nilipewa nikapeleka Benki Kuu. Kwa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili nimekuwa nikizunguka na ndugu zangu wale wa Chama Kikuu cha Ushirika, lakini Benki ile ikawa inatuzungusha na kusema hatujaweza kufikia masharti yaliyowekwa.

Sasa mimi inanipa shida sana kama Waziri wa Ushirika na Masoko na Waziri wa Fedha wameandika barua na bado mpaka leo Chama kile Kikuu hakijapata gari. Sasa tueleweje? Huu ni mzunguko mbaya, kwamba hawa wakulima wanataka waweze kuboresha kilimo chao cha ushirika wao kwa kununua kahawa; lakini wanafika kwenye Benki wanakwamishwa. Isije ikatokea kwamba sasa hivi katika utaratibu ambao tunasema wakulima wataweza kupewa stakabadhi waende kupata mkopo Benki wakafika katika Benki wakarudishwa. Itatuletea adha kubwa sana kwa wakulima kuona kwamba hawafikii lengo waliloahidiwa. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi nyingine ya kumwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia; je, katika vipengele vilivyowekwa kuna sehemu ile ya Ibara ya 38, kuna sehemu ile ya adhabu. Sehemu ya adhabu inasema kwamba, sehemu ile ya kupoteza stakabadhi, kama mkulima amepoteza stakabadhi, hilo ni tatizo lingine ambalo litaleta shida kwamba mkulima akishajua karatasi yake ile ya mazao imepotea na hawezi tena kuwa na uwezo wa kudai fedha hii, itawakatisha tamaa na watakosa imani na huu utaratibu. Itafutwe njia nyingine maana anatakiwa aende Polisi, aende akaandikishe, akatoe taarifa Benki, apelekwe mpaka Mahakamani kwa *Affidavit.* Huu utaratibu kweli mkulima anauweza?

Naomba tuangalie utaratibu ambao iwapo stakabadhi zitapotea, watakuwa na njia nyingine ya kuweza kuwapa dhamana ya mazao yao waliyoweka katika maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda niunge mkono hoja ya Muswada huu, lakini nikiweka tahadhari kwa Mheshimiwa Waziri kuangalia jinsi ya kuboresha ili asije akawakatisha tamaa wakulima katika lengo la kutaka kutumia mazao yao kama dhamana ya kupatia fedha Benki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya jioni niweze kuchangia machache katika Muswada huu. Kwanza kabla sijaenda mbali niweze kuungana na familia ya Marehemu Balozi Hassan Diria kwamba Mwenyezi Mungu amuenzi kuiweka roho yake mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa bado nasoma *Primary School, Sir George* Kahama ni Waziri. Kwa hiyo leo tupo wote hapa na nina imani kwamba ni mchapakazi mzuri na mimi ninamkubali. Naomba asi-*step down* aendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikubali kwamba haya tunayojaribu kuyatoa kwa kusaidia, Mheshimiwa Waziri, yeye ni mzoefu na watu wameshamwambia kwamba anayafahamu. Huu ushirika ni nia nzuri ya Watanzania hata kabla haijawa Tanzania, bado ni Tanganyika kulikuwepo Ushirika na watu waliuitikia. Lakini kadri siku zilivyokwenda, ujanja usioeleweka, si wakulima hawa tunaowawakilisha, wanaotupigia kura, tena walio wengi, hapana.

Mabadiliko ya makusudi na yasiyoweza kuendeleza kizazi hicho yanatokana na hawa waliokwenda Shule. Sasa katika hili suala la stakabadhi, naamini kabisa wasiwasi wangu kwamba ujanja kama ule ule ambao umedidimiza Vyama vya Ushirika umo katikati, unaweza ukajitokeza. Hakuna Mkoa hata mmoja ambao haukuwa na Vyama vya Ushirika. Hakuna Mkoa hata mmoja ambao haukutumia utaratibu huu. Kwa hiyo, haya ni marudio tu. Sasa yanahitaji mtazamo wa aina yake usio kama ule wa kudhulumu. Tulikuwa kule Kigoma na Buha *Co-operative* stakabadhi za mazao yote sijui ya mchele, ya mpunga, dagaa na kahawa na nyanya, lakini watu wale walimfilisi, mwisho vitu vingi vikawa vimepotea. Wakati fulani kwenye Kamati tulikwenda mpaka huko Kanda ya Ziwa, Mwanza na Shinyanga.

Nakumbuka mpaka waliikoromea Serikali kwa sababu wakulima walipeleka pamba yao wakapewa stakabadhi ya muda mrefu ya mabilioni. Mpaka leo nafikiri bado wanadai Wasukuma huko, bado wanadai hela na hata huko Kagera wengine wanaelewa. Lwakatare nilikuwa namwambia hapa. Sasa sijui kama alikwishapewa hizo hela. Na naelewa Sir George anaelewa hiki kitu kwamba watu wamedhulumiwa kwa stahili hii hii. Mimi ningeomba hili ujaribu kuliangalia.

Pili, niseme kwamba huu msukumo ni mzuri. Hivi Sera ya Kilimo cha mazao ya biashara hasa ambayo yamekuwa yakisaidia Taifa hili iko wapi? Maana inakwenda inasuasua. Sasa sijui kama tunawanyanyua kweli wakulima hao. Inakwenda, yaani kama mwendo wa kinyonga, inataka kusonga mbele mwishowe unaona inarudi tu. Kinyonga unaweza ukaenda mpaka Dar es Salaam na ukarudi hajavuka hata barabara. Sasa hii safari ya namna gani? Sera ya kilimo kile kilimo kilichoanza, Wasukuma wanalima kuanzia asubuhi mpaka jioni, wakiwa na matumaini ya ongezeko. Sasa leo mpaka mbolea, yaani unapiga magoti! Hakuna! Juzi tumepitisha hapa, mbolea, yaani

zinunuliwe zote kwa ruzuku. Sasa ajabu mpaka leo Kigoma nina watu wenye pesa zao wanataka wanunue hiyo mbolea haipo. Haipo kabisa!

Namwomba Waziri wa Kilimo na Chakula na Waziri wa Ushirika na Masoko, washirikiane kutatua hili tatizo ili nchi yetu isonge mbele kwa sababu siyo suala la humu humu tu. Haya yatatuchosha. Naomba Sera ya Kilimo, kama utaweza kulijibu, basi kwenye Jimbo langu kuna zao la kahawa.

Humu tumekuwa tukivutana kuhusu suala la *STABEX* hii inakwenda wapi? Maana hii *STABEX* nayo ni ahadi kama hii ya stakabadhi. Tena ile inasema kwamba wale wa kwenye mazao ya kahawa, watapewa mapesa ya kutengeneza barabara. Kwa wakulima hawa wa kahawa hizo barabara zilizotengenezwa na pesa za *STABEX* hakuna. Hizo pesa ziliko hata haijukani, hawa wakulima wanasubiri kitu hicho hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko hii mikahawa na yeye ni Waziri wa Masoko, pamba wamepata, pareto wamepata; tena hapa tulishaambiwa kwamba hizi pesa badala ya kupewa mtu mmoja mmoja, sasa zitatengeneza barabara. Ile barabara Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula anajua kwa kuwa yeye mwenyewe amekaa Kigoma. Hakuna barabara tena ya Mwandiga/Manyovu. Imekufa kabisa.

Sasa tunaomba hata hizo hela ziweze zikafufue ili hizi stakabadhi ziweze kukamilisha kitu halisi. Sipendi kusema maneno mengi sana kwa sababu wakati mwingine rungu linaweza likaja kusema huyu alikuwa ni mkali sana aondoke. Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, hatuwezi kwenda kwenye uchaguzi bado tunaulizwa barabara, tunaulizwa hela za *STABEX,* mpaka lini? Taifa la namna gani? Wewe umeliona wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo uzoefu umeonyesha kwamba Serikali ikishatamka ilikuwa haiwezi kuchukua muda bila kutimiza ahadi ya Serikali. Tuanze jambo hilo kwamba Serikali ikishatamka, hicho kitu kikamilike. Sasa tunakwenda namna gani? Naomba kuunga mkono hoja Muswada uweze kupita mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kwa kifupi sana kuhusu Muswada huu. Kwanza kabla sijafanya hivyo, naomba niishukuru sana Serikali kwa taarifa iliyokuja nayo leo kuhusiana na soko la mtama mweupe huko Italia. *(Makofi)*

Sisi katika Mkoa huu wa Dodoma, tumekuwa tunawahimiza sana wananchi wetu kulima mtama mweupe kutokana na hali halisi ya ukame wa Mkoa huu na wakati mwingine tumekuwa tunazalisha ziada na wananchi hawakujua wafanye nini na ziada yao na mara nyingi sana wamekuwa wakipiga kelele sana kuhusiana na soko. Kwa hiyo kupatikana kwa soko hili la Italia, kwetu imekuwa ni faraja kubwa sana na nina hakika kabisa kwamba wananchi wote wa Mkoa naamini hata Mkoa wa jirani wa Singida

watakuwa wameipokea taarifa hii kwa faraja kubwa na tutaifanyia kazi ili tulitumie soko hili kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka niende moja kwa moja kwenye Muswada na nitamke kwamba nauunga mkono Muswada huu, kwa sababu kwa sisi wa Mkoa wa Dodoma hatuna Chama chochote cha Ushirika tangu *CRCU* ilipokufa, tumekuwa na matatizo sana na mazao yetu ya biashara ambayo hayana Chama cha Ushirika wala Bodi katika nchi hii, imekuwa ni tatizo sana kupata soko. Wananchi wetu wamekuwa wanayapeleka mazao haya kidogo kidogo kwenye soko kwa kiasi kidogo kidogo na soko limekuwa tatizo sana wakati mazao yenyewe kwa kweli yana bei nzuri sana katika soko hasa la Kimataifa. *(Makofi)*

MHeshimiwa Naibu Spika, mazao kama alizeti, ufuta, karanga yana soko zuri lakini wananchi wamekuwa wanashindwa kunufaika na soko hilo kwa sababu ya kupeleka mazao haya kidogo kidogo katika soko. Kwa hiyo, nafikiri utaratibu huu utatusaidia sana sisi na ndiyo maana nauunga mkono. Ila tu ambacho nataka nizungumzie ni kwamba licha ya lengo kuu la utaratibu huu wa kuwezesha wananchi kupata mkopo kutoka kwenye mabenki lengo lingine ambalo vile vile ni muhimu ni matumaini ya kwamba tunapoweka bidhaa katika maghala tunaweza tukasubiri mpaka tukapata bei nzuri katika soko ndipo tukauza mazao yetu. Lakini hili siyo kwamba ni lazima iwe hivyo. Inawezekana kabisa bei katika soko ikaanguka sana. Sasa tunaweka hayo mazao katika ghala mpaka lini? Misimu miwili, mitatu au vipi?

Kwa hiyo, nadhani hili nalo lingelipewa umuhimu katika Muswada huu kwamba jawabu la hili litakuwa ni nini. Mimi nilikuwa napendekeza katika Muswada huu kwamba pamoja na kuunda Bodi ya kusimamia tatizo hili, lakini vile vile tungeunda Mfuko kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi pale bei ya mazao yao ambayo yapo kwenye maghala inapoteremka sana katika soko na kuendelea hivyo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitegemea tu kwamba mpaka tupate fedha kutoka nje kwa utaratibu wa *STABEX* ndiyo usaidie kutoa fidia kwa wananchi wetu na kadhalika, hatuwezi kwenda mbali. Tunapojiimarisha hivi katika utaratibu kama huu, lazima vile vile tuelewe kwamba na wenzetu nao huko wanaweza kupanga mikakati ya namna ya kutufanya tubaki hapa hapa tulipokuwa tusiweze kusonga mbele. Kwa hiyo, wanaweza kufuta haya yote na hatimaye tukajikuta tunakwama na mazao katika maghala.

Kwa hiyo, kama tulivyofanya kwenye suala la kupeleka umeme Vijijini, tuliunda Mfuko pale ambao lengo lake ni kusaidia kuteremsha gharama za umeme unaotumiwa Vijijini, mimi nilikuwa napendekeza katika utaratibu huu tuangalie namna ya kuunda Mfuko ambao utatumika kuwalipa wananchi fidia pale ambapo kwa kweli inatokea tatizo la dhati kabisa la kushuka kwa bei katika soko la ndani au la nje ambalo hatuna uwezo nao ama sivyo itafika mahali ambapo wananchi wetu watakatishwa tamaa na utaratibu mzima ukashindikana.

Tunategemea hizo ni *speculations* tu. Tunategemea kwamba, tukiyaweka mazao yetu kwenye maghala, tutaweza kusubiri mpaka bei zikawa nzuri ndiyo tukauza. Lakini lazima tuelewe kwamba kuna upande mwingine, upande wa pili wa shilingi ambapo bei

ya mazao inaweza kwenda chini na ikabaki hivyo kwa muda mrefu. Tunafanyaje kama hatuna utaratibu wa kuwasaidia wakulima wetu katika hali kama hiyo? tunaweza kufika mahali utaratibu mzima ukakwama. Nilitaka nipendekeze hilo.

Lakini vile vile, niungane na wenzangu kusema kwamba utaratibu mzima utafanikiwa kama suala la maghala mazuri katika Vijiji nalo vile vile tutalitilia maanani sana. Hakuna maghala sasa hivi. Kuna maghala yaliyowahi kujengwa siku za nyuma, lakini kwa kweli yote yako katika hali mbaya na kwa utaratibu huu, tutakuwa kama tunaanza upya. Kwa hiyo, maandalizi lazima yaanze mapema na tujitayarishe kwa kweli kuwekeza katika kuhakikisha kwamba kuna maghala yanayostahili kwa mujibu wa Muswada huu ili tuweze kuanza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni lazima litiliwe maanani sana ni elimu. Kuanzia sasa elimu itolewe kwa wananchi na kwa kila mtu atakayehusika katika utaratibu huu ili kwa kweli manufaa ambayo tunayategemea wananchi wetu wayapate kwa mujibu wa Muswada huu yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo na narudia tena kusema kwamba naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kutoa pole sana kwa niaba yangu binafsi na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma kwa ndugu zetu na hasa ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Ahmed Diria na Paulo Bomani na tunamwomba Mungu azilaze roho za Marehemu hawa Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pole hizo, ninaomba nichukue nafasi nyingine pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya Watendaji katika Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ni mashahidi wa namna gani Wizara hii katika kipindi hiki cha miaka mitano chini ya Uaskari wa Miavuli wa maaskari hawa wawili kwamba umeweze kufanya mambo makubwa sana. Ninaomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba vile Vyama vya Akiba na Mikopo vya wanawake Mkoa wa Ruvuma alivyovisimamia kwa nguvu yake yote vimeanzishwa, vinafanya kazi nzuri na sasa vitasubiri kwa hamu kujiunga na mpango huu ili viweze kuendelea kusaidia wanawake na hata wanaume na jamii nzima ya Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja tu ambalo wanawake wa Mkoa wa Ruvuma walinituma kwa Mheshimiwa Waziri ni kumpa salamu zao kwamba ile ahadi tuliyokuwa tukiifuatilia kwake mwaka jana ya uwezeshaji wa kufanyika kwa Mkutano wao na kufanya tathmini ya kimafunzo ya mafanikio waliyoyapata, basi wanaomba aendelee kuifikiria na aone ni namna gani ataweza kuwasaidia kufanya tathmini ya uhakika kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba mpango huu ama Mjadala tunaouendesha leo katika Bunge letu wa kutumia stakabadhi za maghala na mazao katika kuwasaidia wakulima, umekuja katika kipindi ambacho nadhani ni kipindi muafaka na hasa unaendelea kuipa heshima Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi Serikali yetu imekuwa na wazo moja kubwa la kimsingi na hasa katika kuleta na kuanza sera ya uwezeshaji wa jamii. Muswada huu, unalenga kabisa katika azma ya Serikali ya kuiwezesha jamii. Katika suala zima la kuiwezesha jamii, yako mambo ya kimsingi ambayo yanatakiwa kuangaliwa ili jamii kweli iweze kuwezeshwa na iweze kujiletea maendeleo na kupambana na umaskini kwa kutumia vyazo mbalimbali vya kiuwezeshaji ambavyo vipo katika maeneo husika.

Chanzo kikubwa cha kupambana na umaskini kwa wananchi wengi waliyo Vijijini ni suala nzima la kilimo, kama tunavyosema kilimo ni sekta kiongozi na ndio uti wa mgongo wa Taifa. Lakini katika kuangalia Muswada huu, tunapozungumzia suala nzima la stakabadhi, maghala ya mazao ya wakulima, mimi nafikiri tunawaangalia wakulima hawa katika makundi yao matatu. Liko kundi la wakulima wakubwa, wakulima wa kati, wakulima wadogo wadogo ambao mara nyingi wakulima ndio wamekuwa wakipata matatizo makubwa katika siku zao zote za shughuli hizi za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa stakabadhi ya mazao, utafanana na mfumo wa soko huria kwamba mwenye uwezo atafanya kazi na atafaidika. Lakini inawezekana asiyekuwa na uwezo akapata shida na akaendelea kutokufaidika ipasavyo. Wakulima wadogo wadogo ndio hao wanaokabiliwa na matatizo makubwa ya jinsi na namna ya mfumo mzima wa Benki unavyofanya kazi katika nchi yetu ya Tanzania. Masharti yaliyowekwa katika Mabenki yetu mengi yanawafanya wakulima wadogo wadogo wasipate nafasi ya kujikwamua kupata mikopo na kadhalika.

Sasa mfumo wa stakabadhi ya mazao una lengo la kuwasaidia wakulima kupata mikopo hiyo kutoka kwenye Mabenki. Lakini kama suala la msingi ambalo ndilo litakaloweza kusaidia la kubadilisha mfumo huu wa Mabenki ili uweze kufikiwa na wakulima wadogo wadogo hautaangaliwa, basi bado mfumo huu wa stakabadhi wa mazao unaweza ukaendelea kuwa ni tatizo la kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ambao nafikiri ndio walengwa wakubwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo bado kinakabiliwa na matatizo ya uboreshaji. Ili mazao hayo yaweze kuhifadhiwa vizuri katika maghala na yaweze kweli kuwa na soko la ndani au hata la nje, basi nilikuwa naomba sana utekelezaji wa Muswada huu na Kanuni zitakazotungwa zilenge katika kuboresha zana bora za kilimo. Kwa mfano kuondokana na majembe ya mkono na kuingia kwenye matrekta au majembe ya kukokotwa na ng'ombe ili basi mazao yatakayozalishwa katika mfumo huu yaweze kuwa mazao bora na yaweze kuingia katika soko na kuwapatia faida wakulima badala ya kuendelea kuwadididimiza na kuwarudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu mimi nashauri pia uendelee kufanya kazi sambamba na sekta nyingine mtambuka ambazo zinashughulikia masuala yanayofanana na kilimo. Haitoshi tu kuzungumzia suala nzima la Wizara ya Ushirika na Masoko bila

kufuatilia Wizara nyingine ambazo zingeweza kufanya kazi kwa pamoja na kuboresha suala hili kwa ujumla. Lakini hivyo hivyo kama walivyozungumza wenzangu na mimi naomba niseme kwamba suala la kujua ni Benki ya namna gani inayoweza kuwasaidia wakulima na kuwafikia wakulima mpaka Vijijini ni suala la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Ruvuma, tunayo Benki ya wananchi ya Wilaya ya Mbinga na inafanya kazi vizuri sana. Sasa Benki hizo za wananchi zingeweza kuwa ni kitu kingine muhimu sana cha kuweza kuwasaidia wakulima hawa kufikiwa na faida ya mpango huu na hasa kundi hilo la wakulima wadogo wadogo nililolisema. Lakini viko Vyama vya Akiba na Mikopo katika nchi yetu. Ni bahati nzuri kwamba
Vyama hivyo vinasimamiwa pia na Mheshimiwa Waziri. Nadhani Kanuni au taratibu zitakazotungwa zilenge katika kuboresha hata mfumo wa Vyama vya Akiba na Mikopo ambao uko mpaka sasa hivi na umeenea katika maeneo mengi ingawa bado maeneo mengine havijaweza kuwepo. Kwa mfano katika Jimbo la Namtumbo tunavyo Vyama vingi sana vya Akiba na Mikopo katika Jimbo la Songea ama Wilaya ya Songea.

Mimi nikitolea mfano katika Mkoa wetu ingawa kidogo katika Wilaya ya Songea Vijijini, bado havijaenea kwa wingi, lakini tupo katika harakati ya kuhakikisha kwamba tunahangaika ili kuviwezesha. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ni wakati muafaka wa kuona hayo yanafanyika kwa pamoja. Kwa ujumla niseme kwamba mfumo huu uzingatie sana wakulima wadogo na hasa katika kuanzisha maghala hayo, mimi nadhani kwamba wangefikiriwa wakulima wadogo na siyo kuzingatia wale wakubwa ambao tayari wana uwezo na wanaweza kamiliki na kuchukua uchumi wa wakulima wadogo na wakaendelea kuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kilimo kiendelee kuboreshwa kwa zana bora na pembejeo za kutosha. Vile vile, mfumo huu uzingatie kabisa kuona ni namna gani taratibu za uendeshaji hazitawapeleka wakulima katika hasara na kujutia utaratibu mzima wa uendeshaji wa mfumo huu wa maghala na leseni za mazao. Katika Muswada wenyewe tumeona kwamba kutakuwa na Bodi na Bodi hiyo itakuwa na nguvu za maamuzi makubwa sana ya uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada katika Bodi nyingine, Wajumbe wengi wa Bodi wanateuliwa lakini wakitajwa katika Muswada, namna au aina ya Wajumbe ambao wanatakiwa kuingia katika Bodi hiyo, nilikuwa naomba kama inawezekana, basi pia hata Wajumbe wa Bodi katika bodi hii, wangetajwa angalau kwa namna au aina yao kwa uzoefu au kwa namna ya elimu walizonazo ili tuweze kujua kabisa utaratibu wa muundo wa Bodi utakuwa umeunganisha Wajumbe wa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hayo yote yanaweza yakafanyika na yakawekwa vizuri, ninaamini kabisa kilio cha wakulima wa Tanzania na hasa wakulima wa Vijijini kinaweza kikawa kimepatiwa muafaka. Wakulima wa Tanzania ni kweli kabisa wanachokosa ni masoko na hivyo huu utakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo. Kabla sijasema yote, naungana na wenzangu kwa masikitiko makubwa kwa kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Diria ambaye kwa kweli kati ya viongozi wa nchi hii waliyochangia yeye ni mmojawapo hasa kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo ni pengo kubwa katika kipindi hiki ambacho tunahitaji busara ya hali ya juu katika kuendesha mambo yetu. Hapo hapo, pia napenda niseme kwamba katika kipindi hiki kifupi tumepata tena pigo lingine la kumpoteza Mwasisi wetu wa Chama, Ndugu yetu Paul Bomani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa niseme haya machache kuhusu Muswada huu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kahama kwa kazi ambayo ameifanya ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Ilani ya Uchaguzi tuliyoitumia mwaka wa 2000 katika kujinada kama Wagombea ilikuwa inasema wazi ya kwamba; "Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakapoingia madarakani, itaendelea kuzingatia na kuweka fursa kwa Watanzania ili waweze kuneemeka na kazi wanazozifanya". Hili suala la maghala ni hatua mmojawapo ya kuboresha hali ya wakulima kama kweli Muswada huu utatekelezwa kama ulivyoandikwa hapa. Kwa hiyo napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji ambao wamekaa kwa makini na Kamati ya Bunge hili ambao imeupitia Muswada huu.

Baada ya kusema hayo, ninayo machache tu. Moja nina wasiwasi juu ya wataalam kama tunao ambao wataweza kuangalia hali ya maghala kisayansi, siyo kwa macho kwa sababu unapoweka hasa nafaka katika maghala kunahitajika utaalam wa aina fulani. Kwa mfano mahindi lazima *moisture content* nayo ifahamike kabla hujaweka kwenye ghala, kuna vitu kadhaa vinavyokuwepo. Sasa swali langu ni kwamba, hivi sasa wataalam wengi wanapata shida kufika katika Wilaya za pembezoni kwa masuala mbalimbali. Waziri atanihakikishia kwamba hawa wataalam wa hali ya juu watafika katika Wilaya za pembezoni kama Nkasi, Ukerewe, Muleba, Kibondo, Kasulu na mahali pengine? Ninalisema hili kwa sababu tusipofanya hivyo wale walioko pembezoni mwa nchi hii hawanufaika na maghala haya.

Kwanza usafiri wa kutoa mazao haya kwenda kwenye sehemu za kuuzia umekuwa ni wa utata wakati wote. Kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba suala la maghala haya na jinsi yatakavyoweza kufanya kazi siyo suala la Wizara moja. Wizara hii imetuonyesha namna ya kuwa na maghala haya. Lakini lazima Wizara nyingine nazo ziwe karibu sana na utekelezaji wa jambo hili kwa mfano Wizara inayohusika na usafirishaji ili mazao haya yaweze kutoka kwa wakati. Vinginevyo, *insurance* kubwa zinatumika sana katika kulinda mazao badala ya kuwa ni faida ikawa ni hasara kwa yule anayeweka au yule anayepokea mazao kutoka kwenye maghala.

Suala la pili, sikuona maghala ya samaki na hii ni tabia ya kuwa na fikra finyu. Chakula ni pamoja na nafaka na *protein* ambayo ni samaki. Dagaa, wanawekwa tu hovyo hovyo kwenye magunia, hatuna maghala na hili halikuzingatiwa. Baadaye unachukuwa ugali uliyowekwa vizuri unautafuna bila kitoweo. Hii ni kutoendelea. Kwa

hiyo, kwa sababu tumeanza kuingia katika hatua za kuendelea, mimi natoa pendekezo maghala ya samaki yajengwe mapya. Yajengwe Ukerewe, visiwa vya Muleba, Musoma. Sisi mkitupa na huku anakotoka Mheshimiwa yule mwenye kipara samahani ni Mheshimiwa Sarungi. Kigoma kwa sababu ni sehemu ya chakula na mazao pia. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa hivi tunapata utata kwa wavuvi. Wavuvi wananyonywa kwa sababu ya kutokuwa na maghala ya samaki. Anapovua samaki wakati mwingine tani 10 kwa usiku mmoja anapaswa kuuza kwa bei ya kutupa kwa sababu hana mahali pa kuhifadhi. Hivi juzi juzi tu nimepata taarifa ambayo nimempa Mheshimiwa Waziri Meghji, wavuvi wameniletea taarifa ya kwamba kama hawatahudumiwa vizuri, wako tayari kuuza samaki Kenya na Uganda kwa sababu wanapewa bei nzuri. Sasa mimi nikasema hili ndilo tatizo la kutotatua matatizo ya uvuvi kila mara tunawaacha. Wakija mifugo, ugali wa kutafuna bila kitoweo hatumo. Kwa hiyo, mimi nasema hili liingizwe. Kama Mheshimiwa Waziri aliona ya kwamba ni la Waziri anayehusika na samaki, si kweli. Serikali ni moja. Hatuwezi kuwa na Muswada wa maghala ya ugali na samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, samaki sasa hivi ndio zao kuu linaloleta *foreign exchange* kwa uhakika katika nchi hii. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nimesimama kusema kwamba ninataka kuona maghala yale kuanzia pale Nansio - Ukerewe.

Ninashukuru Mheshimiwa Waziri Yona ambaye anafanya kazi kama Askari wa Mwavuli analeta umeme Ukerewe. Kwa hiyo, hakuna tatizo, tuleteeni maghala ya samaki tutawapa kitoweo na wakerewe wataacha kuhangaishwa na wale wenye viwanda Mwanza ambao wanawafanya wauze kwa bei ya kutupa na wakati mwingine wanawachezea. Wakati wakiona ya kuna samaki wengi wanateremsha bei au wanachelewesha makusudi ili Wakerewe waingie hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo na najua kwamba Waziri kwa umakini wake kwa kweli hili lilimpitia tu na ningekuwa karibu angekuwa ameliweka. Lakini bahati mbaya nilikuwa mbali na yeye alipokuwa anaandika Muswada. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kabla sijachangia, napenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Bomani, Mzee wetu ambaye ametutoka. Kwa kweli Mheshimiwa Bomani alikuwa *think tank.* Nilisoma historia yake nilishangaa kuona mambo aliyofanyia Taifa hili, yalikuwa makubwa sana. Kwa hiyo, kututoka imekuwa masikitiko makubwa. Vile vile, nitoe pole kwa familia ya Marehemu Diria, alikuwa ni rafiki yangu na kupotea kwake kwa kweli nimesikitika sana. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Serengeti, naomba kutoa rambirambi zangu kwa familia hizi.

Vile vile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Kahama kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Mheshimiwa Kahama mimi nilimsikia nikiwa mdogo kabisa. Kilichonifurahisha, ni kuja kuwa naye pamoja humu Bungeni na yeye akiwa kama Waziri. Sikutegemea katika maisha yangu nitakuja kukaa naye kwenye

Bunge moja. Lakini Mheshimiwa Kahama haishii hapo, yeye alikuwa Balozi wetu Zimbabwe. Mimi wakati nafanya kazi Zimbabwe alikuja pale. Sasa yeye hakuwa Balozi, alikuwa baba kabisa. Alikuwa baba yetu na tulimpenda na mpaka leo tunampa heshima kubwa. Ametumikia Taifa, kwa kweli kwa nguvu zake zote pamoja na umri wake lakini kazi alizozifanya hapa, kila mtu anakubali kwamba kweli huyu ni *Sir* George. Kwa hiyo nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, nami naunga mkono Muswada huu. Nitakuwa sina nidhamu kama kweli Mheshimiwa *Sir* George ataleta Muswada halafu mimi nikawa na wasiwasi nao. Kwa hiyo mimi naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka kuuchambua Muswada kidogo kwa kusema kwamba, ukiangalia mkulima anapolima, hekta ya kilimo kama atalima na trekta atatumia Sh. 20,000/=. Halafu atapanda kwa kutumia labda Sh.10,000/=, pembejeo ataweza kutumia huenda Sh.40,000/=, palizi mara mbili na huenda itam-*cost* hela nyingine Sh.20,000/=, atapiga dawa, huyo ni mkulima wa pamba. Kwa hiyo, atatumia tena labda Sh. 20,000/=. Kuvuna pamba siyo mchezo! Kwa hekta anaweza kutumia Sh.20,000/=. Akishavuna ataichambua na atatumia kama Sh.20,000/=. Sasa hapo ukiangalia kwa hekta anaweza kupata kilo 1000 kama ana bahati. Akiuza kilo moja kwa Sh.200/= atapata kama Sh.200,000/= tu na ni wakulima wachache wanaoweza kupata kilo 1000 kwa hekta. Ni wachache mno wanaambulia kilo 200 au 300.

Kwa hiyo kinachoonekana hapa ni kwamba tayari mkulima anapolima pamba huenda analima kwa sababu hana njia ya kufanya. Lakini huwa anapata hasara. Sasa kama atakuwa ameingia hasara, halafu tena aisafirishe hii pamba kitu ambacho ameshapata hasara kwenda kwenye ghala na sasa hivi *petrol* imepanda sana kama kule Serengeti sasa hivi *petrol* pale ni karibu Sh.1,200/= *per litre,* kwa kweli ni hasara. Hii ni kweli kwa sababu kule ni mbali, ni porini na ndio maana hatuna simu za mkononi, umeme mpaka leo hakuna. Kwa hiyo barabara ni mbaya na watu wanatoza bei ghali. Kwa hiyo atasafirisha labda kilometa 60, itabidi tena atumie labda Sh.30,000/=.

Kwa hiyo katika zile Sh.200/= alizopata, ameshatumia Sh.30/= imebakia Sh.170/=. Halafu akifika pale, atalipia gharama za ghala na riba. Kwa hiyo anaingia hasara.

Sasa kama atachukuwa Sh.200,000/=, riba itabidi alipe Sh.40,000/= kwa mwaka. Kwanza ameingia hasara na anaendelea na kile kitu alichoingia hasara kukigharamia. Halafu itabidi aweke *insurance*. Sasa mimi nilivyokuwa nafikiria, kwa kweli lazima wakulima tuwaangalie. Wakulima ndio wengi, tuko karibu asilimia 80 ya Watanzania. Sasa mtindo kama huu ni lazima tuuangalie.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba Serikali iweke ujasiri kwamba mtu akishavuna inunue, hayo mambo yakusafirisha, *insurance*, maghala yenyewe ndio ipeleke huku ilipe huko. Tusiwape wananchi hizi gharama. *There so many ways you can skin a cat* yaani kuna njia nyingi unaweza kuchuna paka. Mimi ninaangalia hii njia siyo kwamba tukiishia pale Serikali inunue yale mazao. Mimi nakubaliana na Muswada huu Halafu Serikali yenyewe ndio iingie hizi gharama. *(Makofi)*

Lakini sasa kamanikienda Serengeti leo wakiniuliza umepitisha Muswada huu, vipi ng'ombe zetu? Sasa na zenyewe zitawekwa kwenye maghala gani? Kwa sababu kama mimi mjomba wangu ana ng'ombe zaidi ya 5,000. Sasa kwa nini zisiwekwe kwenye ghala? Ana mbuzi, kwa nini nazo zisiwekwe kwenye ghala? Njia itafutwe mbuzi ziwekwe kwenye ghala mkulima apate kipato. Kwa mfano unaporuka na ndege, unatoka kule unaingia huku Ngorongoro, Wamasai wana ng'ombe hawalimi. Sasa na hawa nao wawekwe kwenye ghala wapate hela wafanyie kazi kwa sababu wamesahaulika. *(Kicheko/Makofi)*

Halafu kitu kingine tutumie ardhi, acha mazao. Tutumie ardhi kwani ardhi ni yetu na haihami. Hatuna haja ya kuvutavuta *Title Deed.* Wewe unafikiri mimi nitakimbia kwenda wapi? Ardhi ni hii, tuweke ndio tu-*guarantee*. Halafu mjue kwamba mazao yanakuja kwa *demand and supply.* Sasa kama utaya-*hold* mahali, watu hawatapandisha bei, kwani si wanajua yapo? Tukae tuone yanakaa, msimu mwingine unakuja sasa ndio yanateremka bei. Sasa hapo utafanyaje? Mtu akichuka pembejeo akalima kama mwaka huu hapa Dodoma, mazao yote yamekauka hivi atalipaje? Hilo nalo lazima tuone atalipaje huu mkopo. *Insurance* ita-*cover* kweli ukame wa nchi hii!

Kwa hiyo, Muswada pamoja na kuunga mkono unatakiwa ufanyiwe kazi kubwa. Kama nilivyosema, *there is so many ways to skin a cat*, sasa tusikatalie kwamba hii ndio njia pekee. Tuunde Benki ya Ushirika hasa riba ningetaka iwe *just one percent* kwani si Benki yetu tunaweka hela na mbona keshokutwa tunaanza *UTT* ambayo ita-*subsidize* watu wanaoweka Sh.70/= unapewa Sh.100/=, kwa nini mkulima naye asiwe na njia hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na kuunga mkono, lakini naomba sana haya yazingatiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi waliohusika kuandaa Muswada huu. Naunga mkono kwa dhati kwa sababu Muswada huu hauzuii utaratibu mwingine uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko haja ya kuufafanua sana kwa wadau ili wauelewe vizuri. *They need proper education* ili wasidhani ni wa lazima, bali kwa manufaa ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukaandaa maelezo kuhusu gharama na hasara zinazoweza kujitokeza katika zoezi lote hili. Nashauri utekelezaji wa Muswada huu uwe wa uangalifu mkubwa hasa kwa mazao ambayo yanaweza kuharibika haraka wakati yakiwa ghalani. Mazao kama mahindi, maharage yakihifadhiwa bila uangalifu yanaweza kuvunja moyo wa nia nzuri hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya maghala yetu kwa sasa siyo nzuri. Mengine ni ya watu binafsi (gharama na uaminifu wa wasimamizi wa mali za wakulima - ikiwa ni pamoja na wizi) upewe msukumo na usimamizi mzuri. Maghala ambayo hayako chini ya Serikali au Vyama vya Ushirika yapewe utaratibu wa kuyakodisha ili yasimamiwe na wenye mali wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka ya Bodi yaangaliwe upya ili yasijengewe hoja za kulalamikiwa wakati matatizo yanapojitokeza. Vyombo vya Sheria vitumike kila wakati ili kusiwepo na visingizio kwa Bodi ambazo zinaweza kukatisha tamaa Wanaushirika mambo yakienda kombo. Kila mara Bodi ziwe karibu sana na wadau na kuelezea kila wakati hali ya maendeleo ya mazao yao, hali ya masoko na maamuzi ya pamoja yatumike kila mara. Ingefaa tukaandaa kifungu maalum cha kufuatilia utekelezaji wa mfumo huu ili kila wakati wafuatilie maombi katika vyombo vya fedha na kufuatilia tatizo kwa kila zao ili marekebisho yawe yanafuatiliwa bila kuchelewa.

Naunga mkono hoja hii.

**MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE:** Kwanza kabisa nakupongeza kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa wakulima. Pili, naunga mkono hujo hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii itasaidia kuwawezesha wakulima hususan wa Mkoa wa Dodoma kupata mikopo ya kutosha kwenye mabenki na bei nzuri ya mazao yao, kwa kuwa hawana soko la uhakika la mazao yao kama vile karanga, ufuta, alizeti, mahindi na mtama.

Pia, Sheria hii itawaondolea wakulima adha ya kupeleka mazao yao sokoni na italeta ushindani wa soko la ndani na nje.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EDWARD NZIRIYE NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya Stakabadhi za Mazao yaliyohifadhiwa katika maghala kama dhamana ya mikopo toka benki na vyombo vingine vya fedha kupatia mikopo badala ya mali isiyohamishika, ni ukombozi mkubwa kwa wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wadogo. Naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuiwezesha Sekta yetu kuu kuanza sasa hatua ya kuingizwa katika biashara ya kisasa, kuirasimisha Sekta ambayo kwa kiasi kikubwa washiriki wake shughuli zao hazikuwa rasmi.

Napenda kushauri kwamba, kwa kuwa Stakabadhi husika zitafanana na *Bills of Lading* kwa kuwa *Negotiable Receipts,* ni vyema zikawekewa kinga ili zisiporwe na wasio wenye mazao halisi (Wakulima) na kujinufaisha badala ya wakulima wanaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo katika tafsiri pana kinajumuisha Sekta ndogo ya Uvuvi, ni kwa vipi sheria hii nzuri haitaji mahali popote matumizi ya Stakabadhi za mazao ya uvuvi yaliyohifadhiwa katika maghala ya wavuvi wadogo wadogo hasa mwambao wa maziwa yetu mbalimbali, Ziwa Tanzanyika ikiwa miongoni mwao?

Ni vyema Wizara ifanye rejea katika kutabu cha *Tackling Vulnerability* ukurasa wa 62 kilichosambazwa wakati wa Seminaya *MKUKUTA* ambao Mkoa wa Kigoma, hususan Jimbo lote la Kigoma Kusini, umeonyeshwa kama sehemu ya uvuvi, pamoja na Lindi na Mwanza. Kwa kuzingatia ukweli huo, ni vyema sheria ikabainisha maghala hayo bayana. Kwa kufanya hivyo, sheria itahamasisha uvuvi katika maziwa, mabwawa, mito na raslimali ambazo Mkoa wa Kigoma unazo kwa ziada na raslimali ambazo ni tegemeo la maelfu ya wavuvi wadowadogo. Pia kwa kufanya hivyo, sheria itahimiza uanzishwaji wa ufugaji wa samaki katika mabwawa binafsi hasa kwa aina ile ya samaki wasiopatikana mahali pengine popote duniani. Samaki kiasi cha jamii 56 wamethibitishwa na tafiti za *FAO* na Tafiti kuwapo katika mabwawa na Mito ya Malagarasi na Muyovosi - si pengine popote, ni Kigoma kwa sababu ni sehemu ya chakula na mazao pia.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutoa mawazo machache kuhusu Muswada ulio mbele yetu. Kwanza kabisa naunga mkono Muswada huu na kuwapongeza Waziri na Wataalam wake walioutayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kabisa kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuwakomboa wakulima kutoka kwenye umaskini uliokithiri na kutoa nuru katika kuboresha maisha ya wakulima wote. Pamoja na madhumuni haya mazuri, Taifa letu halitafikia malengo haya ya kuboresha maisha ya wananchi wetu kwa kuleta Muswada unaoelekea kutafuta njia ya mkato katika kutokomeza umaskini. Muswada huu unatia mashaka jinsi ya kutekelezeka. Utaratibu kama huu umejaribiwa katika nchi nyingi na katika Taasisi nyingi za Kimataifa lakini matokeoyake hapakuwa na mafanikio.

Kwa mfano, miaka ya 1970 na 1980 Shirika la *UNCTAD* na *ADB* walichunguza uwezo wa kuwasaidia wakulima wa mazao makuu ya biashara. Kwa Benki ya *ADB* utafiti ulifanywa kwa mazao ya kahawa na kakao, *The Export Commodity Diversification Fund: Cocoa and Coffee for Africa case,* kilichokubaliwa katika suala hili ilikuwa ni kuanzisha Mfuko wa muda kusudi kusaidia wakulima wa mazao haya mawili kuwasaidia kuondokana na utegemezi mkubwa katika mazao haya - *Commodity Diversification Strategy.* Leo nchi za Afrika wakulima wakubwa wa mazao haya waliofaidika na Mfuko huu ni Ghana na *Ivory Coast.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ingesaidia sana wakulima wetu kama itaweka utaratibu wa muda, *The Warehouse Receipts* wakati Taifa letu linaunda mpango wa kudumu wa kuwasaidia wakulima. Sheria hii ingelenga kabisa kuthamanisha mashamba ya wakulima wetu kwa mazao ya biashara na chakula. Muswada huu ungetazama na kutumia utaratibu wa kuhakikisha kuwa wakulima walio wengi mashamba yao yawe katika hali ya kilimo cha umwagiliaji maji kusudi waweze kuvuma

zaidi ya mara moja kwa mwaka. Hili litawezekana tu kama Serikali italeta mikakati kabambe ya kuvuna maji kwa matumizi ya umwagiliaji. Nchi hii ina mvua nyingi karibu kila Wilaya na kwa hiyo uchimbaji wa mabwawa uwe sehemu ya lengo la kuthaminisha mashamba ya wakulima.

Nchini Zimbabwe wakulima wadogo na wakubwa wanaweza kupata mikopo yoyote wanayohitaji kwa matumizi ya kilimo. Wakati wa kupeleka maombi ya mikopo Benki, sharti moja kubwa wanaloulizwa na Benki ni ni kama shamba la mkulima lina uwezo wa kupata maji ya kumwagilia katika kilimo cha zao lolote. Mara sharti hili likitimizwa, mkulima anaweza kukopeshwa kiwango chochote cha mkopo. Kwa nini Tanzania isione suala zima la kuthamanisha mashamba kama ni njia au mkakati muhimu wa kuwasaidia wakulima wetu kujikomboa kutoka kwenye umaskini unaoendelea kuwadidimiza zaidi? Nashauri tena kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuthamamisha *(valuation enhancement)* mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ha Stakabadhi za mazao ni lugha nyingine ya kuanzisha utaratibu wa kuwakopa wakulima. Suala la Maghala linakumbwa na matatizo mengi pamoja na teknolojia ya kuhifadhi mazao yabaki katika thamani isiyoweza kuwa suala la ubishi. Kimataifa suala la mazao yanayouzika katika masoko ya ulimwengu litatuwia vigumu kwa sisi Tanzania kuhimili mabadiliko ya bei. Pia, huenda tukakiuka taratibu za *WTO* - Shirika la Biashara Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu kwa masharti kuwa Sheria hii iwe katika mtizamo wa muda mfupi au muda wa mpito wakati Taifa likijiweka sawasawa na mipango au mikakati ya kudumu kuwasaidia wakulima wetu kutokomeza umaskini.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ingawaje nilichangia hoja hii muhimu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, pia nakuomba tena unipatie nafasi maalum ili niichangie tena hoja hii kwa niaba ya Jimbo langu. Naomba kuchangia hoja kwa maandishi ili endapo sitapata nafasi ya kuchangia tena hoja hii kwa kauli, mchango wangu kwa maandishi uwepo katika kumbukumbu za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkinga, napenda kusisitiza kwamba hoja hii ni muhimu sana na imeletwa kwa wakati muafaka. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ushirika na Masoko walioshiriki katika kuandaa Muswada huu muhimu wenye madhumuni wa kumuunganisha mkulima na mfanyabiashara mdogo kwa uhakika na manufaa zaidi katika mfumo rasmi wa soko huria na utandawazi kwa hiari yake mwenyewe. Hakika ni ukombozi kwao na mfumo wenye manufaa zaidi kuliko gharama ambazo watazipata chini ya utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Sika, wasiwasi ambao baadhi ya Wabunge, wameonyesha ama unatokana na hali ya kawaida ya kuwa na mashaka na utaratibu wowote mpya au kutokana na kutokuwa na uelewa mzuri kuhusu maudhui na faida ambazo zinatarajiwa

kutokana na mfumo huo. Uzoefu uliopatikana nchi nyingine na pia kwa mazao mawili katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu, ni vielelezo vya kutosha kuhusu manufaa yanayotazamiwa kutokana na matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika na vikundi kadhaa katika Jimbo langu la Uchaguzi la Mkinga, tayari limekuwa na shauku kubwa ya kutumia mfumo huo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkinga, kwa Mheshimiwa Balozi Clement Geogre Kahama (Mbunge), kwa ziara aliyoifanya Jimboni humo mwezi Oktoba mwaka jana. Mheshimiwa Waziri, alipata fursa ya kujionea maendeleo ya Chama cha Ushirika cha wafuga ng'ombe wa maziwa cha Tarafa ya Mawamba *(MADAFCO)*. Wanaushirika hao walitiwa moyo sana kwa ushauri na miongozo ya Mheshimiwa Waziri na pia ahadi yake ya kuwasaidia Wanaushirika hao kununua ghala hapo Maramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaushirika na wananchi kwa jumla Jimboni Mkinga wamehamasika katika masuala ya kujenga Ushirika na pia kutumia mfumo huo. Vijiji vya Bwiti, Maramba, Maroro, Mahandakini, Gombero, Mkinga, Mtimbwani na Duga ni miongoni mwa Vijiji vinavyozalisha korosho kwa wingi na kufaidika na mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mkinga limebahatika kuwa na mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na matunda, viungo vya vyakula ambayo yangeweza kufaidika sana na mfumo huu. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha kwa ngazi mbalimbali kuboresha huduma za ugani na umakini kwa jumla katika utekelezaji wa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa mara nyingine tena nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Hoja ya Muswada wa Sheria ya Stakabadhi ya Mazao kwenye Maghala yaani , *The Warehouse Receipt Act* ya mwaka 2005 ambayo mimi ninaiunga mkono na kwa mtiririko wa michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia toka jana hadi leo hii jioni inaelekea wote kwa ujumla wetu tunaunga mkono. Kwa hali hiyo basi, napenda kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tutakavyokumbuka kuwa kabla ya kuletwa kwa hoja hii hapa Bungeni, Wizara iliendesha Semina kwa Wabunge wote ambayo kwa kweli nia yake ilikuwa ni kutoa Mwanga juu ya dhana nzima ya stakabadhi za mazao maghalani na vile vile kupata maoni na ushauri mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Jambo ambalo tunataka kusema ni kwamba tunashukuru sana kwa mchango na mawazo yao yaliyotolewa katika Semina ile, imetusaidia sana katika kuwasilisha Muswada huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka, hata michango ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanachangia hoja mbalimbali hapa, imedhihirisha kwamba Semina ile ilisaidia sana. Kwa sababu baadhi yao wamekiri kabisa kwamba wakati Semina ile ilipokuwa inawasilishwa hapa, hawakuwa wameielewa vizuri na ndio maana hata *reaction* ya baadhi yao ilikuwa kidogo iko tofauti. Lakini nashukuru kusema kwamba karibu wote wamesema kwamba dhana nzima imeeleweka na wameona kwamba Muswada huu una manufaa kwa wakulima na wameunga mkono. Kwa hiyo tunapenda tuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajielekeza kufafanua na kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, pengine nizungumze moja tu la ujumla ambalo ni vizuri tukalielewa kwamba mpango huu wa stakabadhi za mazao ghalani, siyo mpango mbadala kwa mipango mingine yoyote ambayo inaendelea hivi sasa. Kwa sababu hii ni fursa mmojawapo katika kutekeleza shughuli nzima za ununuzi wa mazao na kwa hiyo, pengine tuondokane na dhana kwamba mpango huu unakuja kufuta au kusimamisha mipango mingine yoyote iliyopo. Vile vile, mpango huu ni wa hiari kabisa kwa mtu au chombo chochote kukitumia na Sheria hii imeletwa tu kwa ajili ya kuweka msingi kwa kutekeleza majukumu haya ili yaweze kwenda kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine, jambo linalojitokeza waziwazi ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wanauafiki mpango huu na hivi sisi inatupa moyo na kututia nguvu kwamba utekelezaji wake tutakuwa tukishirikiana wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika , sasa napenda nijielekeze moja kwa moja kwenye baadhi ya hoja zilizokuwa zimejitokeza kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge. Ilijitokeza hoja hapa juu ya masoko na bei ambayo kwa kweli ni hoja ya msingi sana na ilichangiwa na Waheshimiwa wengi kidogo. Nao ni kama wafuatao:-

Mheshimiwa Namkulala, Mheshimiwa Ndesamburo, Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Kilasi, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Hamisi Nguli na hapa mwishoni kwa namna fulani Mheshimiwa Kusila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa walipenda kujua kwamba ni jukumu la nani kuuza mazao yaliyohifadhiwa kwenye ghala. Sasa sisi tunasema kwamba, mazao yaliyohifadhiwa kwenye maghala na kupata stakabadhi yanakuwa bado ni mali ya mweka mali na ndiye mwenye jukumu la kuyauza. Iwapo itatokea kuwa mweka mali amekwishachukua mkopo na akashindwa kuulipa, Benki iliyotoa mkopo ina uwezo wa kumpa mwendesha maghala ruhusa ya kuuza mali iliyopo kwenye ghala ili kufidia fedha kwa mkopo pamoja na gharama za waendesha maghala.

Lakini vile vile, kutokana na suala hilo hilo la bei kwa gharama mbalimbali, limejitokeza suala la kushuka kwa bei mara kwa mara ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge niliowataja. Benki zinazotoa mikopo, hutazama mwendo wa bei

katika Soko la Dunia kabla hawajatoa mikopo. Hivyo, asilimia inayotolewa kwa mikopo huangaliwa kwa uangalifu mabadiliko ya bei, ili kumsaidia mkopaji asishindwe kulipa mkopo huo wakati atakapouza mazao yake. Hii ndio maana tunasema kwamba ile asilimia ni kutoka kati ya 60 mpaka 65. Kwa hiyo inaangaliwa hiyo *trend* ya bei itakavyokwenda.

Kwa hiyo, vyombo hivi vinavyotoa fedha, navyo vilevile vina utaratibu wake wa kuangalia hali halisi inavyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini limejitokeza suala la hoja ya uenezaji wa mfumo huu kwa mazao na maeneo mengine. Maana hapa hoja ilikuwa imeona tu kwamba tumeufanyia mpango huu katika mazao mawili,. Nataka tu nitangulie kusema kwamba mazao yale mawili ya kahawa na pamba, yalikuwa ni majaribio. Lakini dhamira na makusudio mazima ya mpango huu kwa kweli ni kujielekeza katika mazao yote. Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba mazao yaliyohifadhiwa kwenye maghala ni kwa ajili ya bei nzuri kwa kuyaongezea ubora ambao unaweza kuwa kivutio cha kupata wanunuzi wengi.

Kwa hiyo, korosho kwa mfano aliyoizungumzia ndugu Namkulala inaweza kuuzwa pia katika utaratibu huo. Lakini nataka tu niseme kwamba mfumo wa Stakabadhi za Mazao umeanzishwa nchini kwa ajili ya mazao yote ya kilimo. Mafanikio yaliyopatikana kwenye majaribio ya mfumo kwa mazao ya pamba na kahawa, yatakuwa ni changamoto kwa mfumo huo kuenea kwa awamu katika mazao mengine na katika maeneo mengine.

Kwa hiyo na yale mazao ambayo hayakutajwa yatajumuishwa katika mfumo huu na kama tutakavyoeleza hapo baadaye, suala la elimu ambalo limetajwa na Waheshimiwa Wabunge wengi litatiliwa mkazo ili kuweza kuhamasisha watu waweze kuelewa,na hatimaye waweze kuutumia mpango huu katika mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema, pengine ni pamoja hata na zao la samaki ambalo Mheshimiwa Balozi Mongella amelizungumzia sasa hivi kwa utaratibu wa hapo baadaye tutakapo kuwa tumejidhatiti vizuri, maghala kama hayo yanaweza yakatayarishiwa utaratibu yakaingia katika utaratibu huo. Kwa hiyo, hatua mbali mbali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi muhimu ya awali yatakayouruhusu mfumo huo kufanikiwa kutegemea na mazingira.

Lakini lilikuwepo pia wazo la kwamba, labda *SGR* mtumie mfumo huu. Tunasema kwamba wazo la *SGR* kutumia mfumo wa Stakabadhi za Mazao ni wazo nzuri, lakini *SGR* imeanzishwa kwa madhumuni yake. Mfumo ni wa hiari na haulengi kuondoa fursa za mifumo mingine iliyopo. Hii ni pamoja na *SGR,* hatuwezi tukasema kwamba sasa mfumo huu uwe ndio mbadala ili uweze ukafuta utaratibu wa *SGR*. Kama tulivyosema kwamba itakuwa inaangalia tu fursa nyingine kama zipo, zitaendelea kutumika. Lakini endapo mfumo huu utashamiri kutumika vizuri, watu wengine wakaamua kutozitumia fursa nyingine, basi zitakuwa zimejiondoa zenyewe kwa utaratibu huo. Lakini hatuwezi tukasema tu kwa ujumla wake kwamba, basi huu ndio uwe mfumo mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja ambayo imezungumziwa vilevile na wasemaji wengi kidogo kuhusu suala la umuhimu wa kupunguza gharama za uendeshaji wa mfumo wa Stakabadhi za Mazao. Wazungumzaji walikuwa wengi kidogo, wako 13 hivi. Nao ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Asha Magina, Mheshimiwa Ngwatura, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Dr. Kamala, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr.Aaron Chiduo, Mheshimiwa Magayane, Mheshimiwa Dr.Christant Mzindakaya, Mheshimiwa Hamisi Nguli na hapa jioni Mheshimiwa Dr. Wanyacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelezo ambayo tunatoa katika hili ni kwamba, utumiaji wa mfumo wowote wa kuuza mazao unaambatana na gharama mbalimbali zisizoepukika na vivyo hivyo utumiaji wa mfumo wa stakabadhi za mazao katika maghala unaambatana na gharama zake.

Utafiti uliofanywa katika maeneo ya majaribio ya mfumo huu, yameonyesha kwamba endapo wakulima au wazalishaji wataamua kutumia mfumo wa Stakabadhi za Mazao na kuuza kwa kuzingatia mwendo wa bei, gharama zinazoambatana na mfumo huu hazitakuwa ni kikwazo kwao, kwani walipata faida kuliko wale waliotumia mfumo mingine na mfano umetolewa asubuhi wakati tunawasilisha. Wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha Muswada huu hapa ametoa mfano ambao ulikuwa unaonyesha kwamba wale waliotumia mfumo huu wamepata faida kuliko wale ambao hawakuutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea pia kuhamasisha wakulima na wafanyabiashara wadogo kujiunga katika vikundi na Vyama vya Ushirika ili waweze kuuza mazao kwa wingi na hivyo kupunguza gharama za matumizi ya mfumo huu. Aidha, Serikali itaendeleza Sera zake za kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji wa mazao kama vile kufuta kodi za pembejeo, kutoa ruzuku kwa mbolea na kufuta kodi ambazo ni kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo mkubwa sana kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ilikuwa mpango huu uende katika maeneo mengi na uhusike na mazao yote. Hilo tumesema kwamba tumelizingatia tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja ambayo ilijitokeza ya juu ya uhalali wa Stakabadhi za Mazao kwamba uhalali wake utakuwaje? Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Leonard Derefa. Walikuwa na wasiwasi juu ya uhalali wa zile Stakabadhi, kwa kutoa mifano kwamba kama utengenezaji wa fedha tu unagushiwa; Je, Stakabadhi hizi ndio zitakuwa na ugumu gani kugushiwa na uhalali wake vilevile?

Maelezo ni kwamba, Stakabadhi zitakazotolewa chini ya mfumo huu zitatambulika kama nyaraka za fedha. Kwa mantiki hiyo, zitatengenezwa kwa utaalam wa hali ya juu kwa kutumia karatasi maalum kama zinazotumika kutengenezea nyaraka nyingine za fedha kama vile hundi za Benki. Kwa hiyo, ndio maana tunasema kwamba itakuwa *negotiable instrument.* Kwa hiyo itakuwa kama hundi ya Benki ili atakayegushi

aonekane kwamba amefanya kitu ambacho ni kinyume cha utaratibu. Aidha, elimu itaendelea kutolewa kuhusiana na mfumo huu likiwemo suala la kuelimisha jamii kuhusu thamani ya stakabadhi hizo na matumizi yake.

Pia, sheria inayopendekezwa ina vipengele vya kudhibiti vitendo vya kugushi Stakabadhi hizo na adhabu kali imependekezwa kwa wale watakaopatikana na kosa la kugushi Stakabadhi kama ambavyo mmeona kwenye Sheria hii. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasi wasi kwa sababu maandalizi yote yatakapokuwa yamekamilika, maandalizi ya nyaraka hizo yatatengenezwa kwa uangalifu mkubwa sana na zote zitapata uhalali unaostahili.

Hoja nyingine ambayo imejitokeza ni Bodi na majukumu yake kwa upande wa Serikali. Waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Ngwatura, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini; Mheshimiwa Kamala, Mbunge wa Nkenge na Mheshimiwa Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili Waheshimiwa Wabunge walionyesha wasiwasi kwamba sasa imeonekana kama ni mtindo kwamba kila tunapofikiria kuanzisha shughuli inayohusiana na mazao, basi inaundiwa Bodi yake. Hapa tunachosema ni kwamba, pamoja na kuwepo na Bodi ziliko sasa hivi, lakini suala hilo tunalolishughulikia chini ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo na mfumo huo kuhusu hatima ya kuwepo kwa Bodi. Hata hivyo, kuwepo kwa Bodi ya kusimamia mfumo huo ni lazima kwa kipindi cha mwanzo na Serikali itaghalimia uendeshaji wa Bodi hiyo. Hapa ninachotaka kusema kwamba, hii itakuwa ni Bodi maalum kwa ajili ya kusimamia mpango huu tu ambao kusema kweli, hii itakuwa inasimamia mazao ya aina yote kama tulivyokuwa tumeiema. Kwa hiyo haitakuwa ni Bodi ambayo inaangalia utaratibu wa mfumo wa zao moja.

Kwa hiyo, Bodi itakayoundwa ni moja tu na umuhimu wake ni kusimamia mfumo unaopendekezwa na Sheria hii. Chombo hicho kitakuwa huru na chenye mwelekeo wa kibiashara, shughuli ambayo Serikali kwa mujibu wa Sera za sasa imeamua kujitoa. Aidha, Bodi hiyo itakuwa na Wajumbe kutoka kwa wadau wa mfumo huu, kwa mfano Wawakilishi wa Vyama vya Ushirika, Wawakilishi wa Wakulima, Mwakilishi wa Mabenki, Mwakilishi wa Makampuni ya Bima na wa Wakilishi kutoka kwenye *operators* wenyewe. Hawa *Warehouse Operator* kusema kweli lazima wawakilishwe hapa maana yake kulikuwa na wasiwasi asubuhi kwamba sasa Bodi hii kama itakuwa inaendeshwa kiserikali Serikali hivi!

Tunachosema ni kwamba, Bodi hii itaendeshwa na wadau wote wanaohusika na mfumo mzima. Kwa hiyo watakuwepo watakaotoka kwenye Vyama vya Ushirika, wakulima wenyewe, hao *Warehouse Operators, Bankers* na wengine ili waweze wote wakaingiza utaalam pamoja na mahitaji yao mbalimbali katika hatua mbalimbali. Kwa hiyo, haitakuwa Bodi ya Serikali kama walivyokuwa wamejaribu kuonyesha wasiwasi baadhi ya Wajumbe katika uchangiaji. Kwa hiyo, Bodi imepewa mamlaka ya kuita mashahidi na kutoa vyanzo pindi itakavyokuwa inashughulikia masuala ya kiutendaji

katika mfumo huu na sio mamlaka ya kimahakama. Mahakama hiyo ni ya kawaida katika Bodi mbalimbali ambazo zinatumika hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi itakuwa ni chombo cha utoaji leseni za kuendesha maghala katika mfumo huu. Aidha, vigezo vilivyowekwa ni kwa ajili ya kuwezesha mfumo huu uweze kutekelezwa bila kumuathiri mkulima mdogo ambaye ndio mlengwa katika mfumo huu. Masharti yaliyowekwa ni kwa ajili ya kupata waendeshaji maghala wenye sifa zinazotakiwa na maghala yenye viwango vya ubora unaostahili. Kwa hili nilivyokuwa naeleza, ile *composition* ya Bodi maana yake ilikuwa ni hiyo, kwamba kutakuwa hakuna wasiwasi wa namna ya kutekeleza yale majukumu ya mfumo mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda nijielekeze katika hoja za Wabunge ambazo zilijielekeza kwenye vifungu mbalimbali vya Muswada wa Sheria. Ipo hoja hapa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kifungu 33 (1); anasema, hakijaeleza umuhimu wa thamani ya mazao kuonekana kwenye stakabadhi. Maelezo yake kwamba ni hii itajumuishwa kwenye kanuni chini ya kifungu cha 33 (1) (d), kwa hiyo tutakapokuwa tunaanda kanuni hili suala litajitokeza na ufafanuzi wake utatolewa.

Lakini Mheshimiwa Beatus Magayane kwenye vifungu pale alihoji kifungu Na.44 (2) (b) kwamba, hakiweki umuhimu wa kuwasiliana na *depositor* kabla mwendesha ghala hajauza mazao. Maelezo yake ni kwamba kifungu hiki kitatumika endapo tu *depositor* atashindwa kulipa ili mazao hayo yatolewe ghalani. Hii ina maana atakuwa na taarifa tayari. Ufafanuzi zaidi pia nao utatolewa kwenye kanuni ambazo zitaandaliwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini pia iko hoja katika kifungu cha 17 kuhusu ku-*renew* leseni ifanyike baada ya miaka miwili ili kupunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ilikuwa kwamba ili kupunguza gharama, leseni pengine ingetolewa kila baada ya miaka miwili, na maelezo ni kwamba Sheria na Sera za usimamizi wa fedha zinahitaji leseni ziwe zinakuwa *renewed* kila baada ya mwaka mmoja. Ili kuhakikisha kuwa masharti ya leseni bado yanatekelezwa, hata hivyo Serikali imerekebisha kile kifungu cha Na. 9(b) kama mtakavyoona kwenye *Schedule Amendments* zilizotolewa jioni hii ili kuondoa ile dhana ya leseni kutumika kama chanzo cha mapato. Kwa hiyo, utoaji wa leseni hakitakuwa mojawapo kama chanzo cha mapato ya Bodi katika kutafuta mapato yake. Hii ipo kwenye *amendments* kama nilivyokuwa nimesema.

Halafu hoja nyingine katika sehemu ya tano ilisema kwamba haionyeshi vifungu vitakavyosaidia katika kuzingatia ubora. Suala la ubora ni kitu muhimu ambacho kinapaswa kionekane kwenye Stakabadhi za maghala. Hivyo, kimezingatiwa. Aidha, kwenye kanuni suala hili litafafanuliwa vizuri zaidi kwa sababu kule ndio kwenye maelezo ya utekelezaji zaidi. Chini ya kifungu Na.7 Mtendaji Mkuu achaguliwe kwa utaratibu wa kutumia *Search Committee* na hoja hii nadhani alikuwa ameitoa Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga. Tumesema kwamba kifungu kinatoa maelekezo ya jumla kuwa Mtendaji Mkuu wa Bodi atateuliwa na Waziri kutokana na mapendekezo ya majina matatu yatakayokuwa yametolewa na Bodi, na suala hili kusema kweli ni la utaratibu tu. Kwa hiyo *Search Committee* sio lazima kuingizwa kwenye Sheria yenyewe, lakini katika utaratibu wa utekelezaji kama mamlaka ya uteuzi ni Waziri, basi wale

waandaji wa utaratibu mpaka kumfikia Waziri ateue, kwa vyovyote vile wanaweza wakatumia utaratibu huo na kwa hiyo si lazima uingie kwenye Sheria kuu.

Mheshimiwa Mzindakaya alitoa hoja katika Ibara ya 54 (1) kwamba nani atasema kwamba *charge* hizi ndizo halali? Hili lilikuwa suala la msingi sana. Maelezo ninayoweza kutoa hapa ni kwamba, utaratibu wa namna ya kukubaliana kuhusu *charges* utafafanuliwa kwenye kanuni pia. Kwa sababu si kila kitu lazima kiwekwe hapa, kwa hiyo tumesema kwamba itafafanuliwa kwenye Kanuni, na hata hivyo itategemeana na bei zitakazokuwa kwenye soko. Lakini pengine kwa sababu bado nipo katika eneo hili ambalo Mheshimiwa Mzindakaya alikuwa amelichangia, tungependa tumshukuru kwanza kwa lile angalizo juu ya utumiaji wa maghala na kukosekana kwa maghala Vijijini.

Lakini mahususi ameelezea maghala ya Mkoa wa Rukwa ambayo yalikuwa yamejengwa kwa msaada wa wenzetu Wajerumani kupitia Shirika la *GTZ* na kwa maelekezo ambayo Serikali ilikuwa imetoa kwamba maghala haya hayakupaswa yauzwe, lakini ameeleza kwamba kuna ukaidi wa namna fulani ulifanywa. Sisi tunasema kwamba suala hili tutalifuatilia na kusema kweli tungependa tu ushirikiano wake ili kuhakikisha maghala yale ambayo yalikuwa yamedhaminiwa yatumike na wanakijiji, yanarudishwa mikononi mwa wanakijiji tungeomba atupe ufafanuzi wake wa kina juu ya namna gani fedha hizo zilivyotolewa na nani alizipokea.

Kwa hiyo, katika hilo, Serikali itafuatilia na tunadhani itakuwa imejenga hata hoja yetu hii ya kuhakikisha kwamba tuna maghala ya kutosha na imara ya kuweza kutumika kule Vijijini. Kifungu cha 28 ambayo ni hoja ya Mheshimiwa Ibrahim Marwa kwamba hakionyeshi sifa za *inspectors;* sifa za *inspectors* zinataonyeshwa kwenye kanuni na marekebisho yamependekezwa katika *Schedule of Amendments* ili kuwezesha sifa hizo ziwekwe kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ufupi na kwa ujumla hizi ndio hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo niliona nizitolee maelezo. Lakini kusema kweli ni nyingi sana ambazo pengine kuzimaliza zote si rahisi. Kwa sababu mengi yalikuwa kama ni ya ushauri ambayo tutauzingatia katika utekelezaji na yale ambayo yalikuwa yanahitaji tujielekeze moja kwa moja kwayo kama tulivyosema, yapo mengine kwenye Sheria, kwa mfano wale waliosisitiza kwamba mazao yanaonekana ni mawili tu, tumesema kwamba yale yote yamehusishwa kwenye Sheria na tutayatekeleza.

Lakini la mwisho la jumla ambalo watu wengi ambao walikuwa wamechangia, wamezungumzia suala la elimu ambalo najua Mheshimiwa Waziri ataliongelea pia na hasa wale waliokuwa wanazungumzia habari ya Elimu ya Ushirika na Elimu ya Biashara. Nataka niseme tu kwamba kazi hiyo kama Wizara au kama Serikali, ilishaanza kuitekeleza toka muda mrefu sana. Tumeshaanzisha taratibu mbalimbali za mafunzo ya Elimu ya Ushirika shirikishi na kama mtakavyokumbuka, hivi karibuni Chuo chetu cha Ushirika sasa ni Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara. Kwa hiyo, suala la kusisitiza stadi za biashara, kwa vyovyote vile itakuwa ni pamoja na hizi taratibu zote

ambazo tunakuwa tunazieleza hapa kwa mifumo hii itakayokuwa inaanzishwa iwe ni hiyo *ya Warehouse Receipts*, mambo ya Bima, mambo ya Banking yote yataingia humo.

Kwa hiyo mimi ningependa tu niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wabunge kwamba katika suala la elimu, unapozungumzia elimu kwa ujumla wake itakuwa ni kuelimisha mfumo huu utakavyofanya kazi. Lakini vile vile kuelimisha juu ya stadi nzima za biashara ambazo zitaweza kuwasaidia wananchi kuelewa na hatimaye kuwa wasimamizi wazuri katika utekelezaji wa majukumu ya Sheria na yale ambayo yatakuwa ya manufaa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine na nataka nirudie kusema tena kwamba ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kwa mara nyingine tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine ili nihitimishe hoja yangu niliyoitoa hapa Bungeni jana jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Hezekiah Chibulunje, Mbunge wa Jimbo la Chilonwa kwa kunisaidia kujibu hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja yangu leo mchana na jana. *(Makofi)*

Vilevile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Stanley Kolimba, Philemon Ndesamburo na Herbert Mntangi ambao pia wamesaidia kueleza na kufafanua masuala mbalimbali kuhusu dhana nzima na faida za kutumia mfuko unaopendekezwa wa stakabadhi za mazao kwenye maghala. *(Makofi)*

Napenda nichukue nafasi hii vile vile, kumshukuru Mheshimiwa Dr. Mzindakaya na Waheshimiwa wengine kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Asante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara, kwa jinsi walivyotupatia ushirikiano mzuri katika shughuli mbalimbali za Wizara ikiwa ni pamoja na michango yao katika Muswada huu ambao uko mbele yetu. Kama nilivyosema katika hotuba yangu ya kuwasilisha Muswada, maoni yote ya Kamati yamezingatiwa kwenye Muswada huu. Kwa ujumla Kamati imetupa hamasa kubwa katika utekelezaji wa majukumu yetu Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Waziri wa Kivuli wa Wizara yangu Mheshimiwa Aisha Magina. Napenda kumhakikishia kwamba hoja zake alizozitoa tutazizingatia katika utendaji wa kazi zetu. Ingawa Mheshimiwa Magina hakusema kama anaunga mkono Muswada huu, lakini hoja zake zote zinaonyesha wazi kuwa anakubaliana na maudhui ya Muswada huu. *(Makofi)*

Hivyo ninaamini kuwa anaunga mkono mia kwa mia, namshukuru pia kwa umakini wake. Napenda vilevile, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika mjadala wa Muswada huu ama kwa kuzungumza Bungeni au kwa maandishi. Napenda kuwatambua kwa kutaja majina yao, lakini kabla ya hapo napenda kuwahakikishia kwamba hoja zao zote na ushauri wao na mapendekezo waliyoyatoa yatazingatiwa na hakuna hata moja ambayo itapuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:- Ni wengi kidogo, lakini naomba uniruhusu niwataje. Kwanza ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, ambaye aliongea kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na kwa niaba yake; Mheshimiwa Aisha Magina, Mbunge wa Viti Maalum na Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini; Mheshimiwa Irenus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki; Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mbunge wa Ludewa; Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini; Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge; Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza; Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga; Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali; Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mbunge wa Gairo; Mheshimiwa Beatus Magayane, Mbunge wa Buyungu; Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela; Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu; Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Vijijini; Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini; Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mbunge wa Singida Mjini; Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mheshimiwa Singo, Mbunge wa Same Magharibi; Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge (Viti Maalum); Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, Mbunge wa Serengeti na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko na Mbunge wa Chilonwa, *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa maandishi ni kama wafuatao:- Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini; Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa; Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga; Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi na Mheshimiwa Edward Ndeki, Mbunge wa Kigoma Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo katika baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yafuatayo, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwanza ni elimu, umuhimu wa elimu kwa wadau wa mfumo huu; pili, ni huduma za Bima; tatu, ni miundo mbinu ya maghala na nne, ni huduma za kibenki. Ningependa kuanza na hoja kuhusu elimu kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii inahusu umuhimu wa elimu kwa wadau wote, kama walivyoeleza Waheshimiwa Wabunge na utaalam unaotakiwa kwa uendesha maghala na katika hili Wizara inaitambua umuhimu wake.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni wengi, lakini kama nilivyosema, naomba pia niwataje. Ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Ngwatura, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Stanley Haule Kolimba, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Kilasi, Mheshimiwa Dr. Chiduo, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Karamagi na Mheshimiwa Kusila.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya kuwasilisha Muswada huu jana, na kama Waheshimiwa Wabunge walivyoeleza, kuna umuhimu wa kueneza elimu ya mfumo huu kwa kuwa ni utaratibu mpya ili uweze kueleweka kwa wadau wote. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kutoa mafunzo kwa wadau wote wakiwemo wakulima, vikundi vya wakulima, Vyama vya Ushirika, Taasisi za fedha, wamiliki na waendesha maghala kuhusu uendeshaji na manufaa ya mfumo huu. Mafunzo haya yatazingatia mapendekezo na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa elimu kuhusu mfumo huu imeanza kutolewa na imetolewa kwa muda wa miaka minne kwa wakulima, imetolewa kwa viongozi wa Vyama vya Ushirika na vikundi vya wakulima kuanzia kufanya Mikutano katika warsha na katika kutoa vipeperushi mbalimbali, vinajieleza chimbuko la mfumo, faida zake na taratibu zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kuomba mikopo.

Aidha, mafunzo yametolewa na uongozi wa mradi na programu za kuendesha masoko ya mazao ya kilimo, kwa kushirikiana na Bodi za mazao na Kampuni binafsi ya *Audit Control Expertise.* Mafunzo hayo yanalenga kupanua uelewa wa wadau katika maeneo yaliyopendekezwa kama vile umuhimu wa ubora wa mazao, sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya mifuko hiyo na mbinu za kuepuka hasara mbalimbali zinazoweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, elimu kwa waendesha maghala na mabenki imetolewa vilevile na inaendelea kutolewa na Taasisi za kitaalam ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo ya mafunzo yaani *Training Guide Lines* ambayo imeainisha aina ya mafunzo katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja hii pia kuwa kuhusu waendesha maghala kuwa na ujuzi na kanuni za uboharia na ugavi, Serikali inawahakikishia

Waheshimiwa Wabunge kuwa suala hilo linazingatiwa katika kifungu cha 18(1) ambacho kinatoa vigezo ambavyo vinatakiwa kuzingatiwa kabla mwendesha maghala kupata leseni. Hoja ya pili iliyotolewa ilikuwa ni hoja kuhusu huduma za Bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilihojiwa kama kuna Mashirika ya Bima ambayo yako tayari katika mfumo wa Stakabadhi za Mazao kwenye maghala na kama yana uwezo wa kufidia pale inapohitajika. Aidha, kulikuwa na hoja ya kuanzisha *Price Stabilazation Fund* iliyosisitizwa sana na Mheshimiwa Dr. Kamala na leo mchana na Mheshimiwa Kusila. Waheshimiwa wengine waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimwa Iwvatta, Mheshimiwa Kamala, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Kilasi, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na Mheshimiwa Leonard Derefa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa watoa Bima katika mfumo huu ni kukinga mali iliyoko ghalani juu ya upotevu. Hii ni muhimu ili kumthibitishia mkopaji, yaani mabenki kuwa mali hiyo ipo, na hata ikitokea upotevu Benki na mkulima mwenye mali watafidiwa kikamilifu, yaani *Compensated Appropriately.* Kwa hiyo, Shirika la Bima litakaloshiriki katika mfumo huu, lazima liwe na uwezo wa kulipa. Kwa vile huu ni mfumo wa hiari na washiriki kuingia mikataba maalum, ni jukumu la Bodi tutakayoiunda kuhakikisha kuwa washiriki wa mfumo huu wana uwezo wa kusimamia na kutekeleza majukumu yao kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kulipa fidia pale inapohitajika.

Kwa kipindi hiki cha soko huru, kuna Mashirika mengi ya Bima Dr. Kamala alihoji kama Mashirika haya yapo, nataka kumhakikishia kwamba katika kipindi hiki cha soko huru kuna Mashirika mengi ya Bima na yale yenye sifa ambayo yatakuwa na yale ambayo hayana sifa yanajijua yenyewe. Aidha, Mkoani Kilimanjaro kwa mfano mfumo huu umepata mafanikio makubwa kutoka kwa Kampuni ya Bima ya *Jubilee* yaani *Jubilee Insurance* ambayo imeweza kutoa punguzo la gharama za Bima kwa Benki ya Kilimanjaro *Comparative Bank* kutokana na kutokuwepo upotevu wa mazao yako ghalani. Aidha, Benki ya *CRDB* wana utaratibu wao wa ndani wa kuhakikisha washiriki wote kwenye Mfuko huu wanakuwa na Bima zinazopunguza athari zinazoweza kutokea.

Katika mradi wa uendeshaji wa mfumo wa masoko ya mazao ya kilimo, tayari mazungumzo yanafanyika na Kampuni ya Bima, yaani *Alexander Forbes,* Kampuni kubwa kutoka Afrika Kusini ambayo inafanya kazi katika Afrika Mashariki ili kuweza kutoa huduma ya Bima ya mazao ghalani. Baada ya sheria kukamilika tunaamini wadau wengi zaidi watajitokeza ili kushiriki katika mfumo huu. Kampuni ya Bima inaweza pia kujiongezea uwezo wa kutoa fidia kwa *reinsurance*. Kwa utaratibu huu Kampuni ya Bima nayo inakuwa na kinga ya kipekee ya kuepuka kushindwa kulipia stahili zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwepo wazo kuwa ili kupunguza *risks*, Mfuko wa *Stabilization Fund* uanzishwe. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba rai hii ilikuwa kwa muda mrefu katika maofisi ya Serikali na tunaendelea kuangalia uwezekano wa kuanzisha. Lakini wote kama mnavyofahamu, *Stabilization Fund* unahitaji mapesa mengi na si nchi nyingi sana zina mifuko ya namna hii, hata zile

ambazo zilikuwa na mifumo ya namna hii wameachana na utaratibu huu, lakini sisi tunaendelea kuona kama uwezekano huo upo.

Lakini kwa sasa kuna utaratibu mbadala ambao unaonyesha mafanikio ndani ya mfumo wa Stakabadhi za Maghala ambao ni Bima au kinga ya bei, yaani *price insurance* na *price hedging* ambao tumeanza kuitumia tangu mwaka jana pamoja na ushirikiano na *CRDB*. Mbinu hii hutumika kukinga maporomoko ya bei ya ghafla kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ningetaka kuitolea maelezo ya ziada ni hoja ya miundombinu ya maghala. Katika eneo hili hoja zilizojitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na kwamba uhakiki wa maghala ni gharama na huchukua fedha nyingi na upatikanaji wa vibali vya kuendesha maghala unaweza ukachukua muda mrefu.

Pia, kwamba maghala kuwa katika ngazi mbalimbali na hivyo kuongeza gharama mfano wa maghala ya Kahawa, Mbinga Mjini, Kiwandani na Makombako, wajenzi wa maghala wanaweza kujenga sehemu zenye miundombinu mizuri, ujenzi wa maghala uende sambamba na masoko, Serikali iingie katika kujenga maghala ya mfano na aina ya maghala inayotakiwa kwa ubora yajengwe hadi Vijijini. Maghala yaliyopo ambayo sio imara na mengine yamejengwa kwa matope yanaweza yasifae.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni wafuatao:- Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa na Mheshimiwa Leonard Derefa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa maelezo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama uhakika haufanyiki kwa makini, ni kweli gharama zitakazotokana na utumiaji wa maghala yasiyohakikiwa vizuri zinaweza kuwa kubwa zaidi ya zile zitakazokuwa na uhakika na ubora wa maghala. Maghala yasiyofaa tutahakikisha kwamba hayatumiwi kwa sababu lengo kubwa la mfumo huu ni usalama na ubora wa bidhaa zinazohifadhiwa kwenye maghala. Katika kipindi cha majaribio, maghala yaliyokubalika na Taasisi za Fedha ni yale yaliyopo kwenye viwanda vya kusindika mazao kama vile viwanda vya kukoboa kahawa vya Mbozi, Moshi na Mbinga na Kiwanda cha Kuchambua Pamba kilichopo Moshi.

Hata hivyo, uuzaji wa mazao katika ngazi yoyote ya maghala ni kutokana na utaratibu wa masoko uliopo hata kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huu tunaouzungumzia. Gharama za kuhifadhi mazao kwenye ghala hujumuishwa katika gharama za kusindika kwa mfano Sh.160/= kwa kilo ya pamba nyuzi ililipwa kama gharama za kuchambua na kuhifadhi pamba mbegu katika ghala la *ginnery* ya Moshi. Aidha, Kiwanda cha Kukoboa Kahawa cha Mbozi kilitozwa Sh.42/= kwa kilo na kile cha

Moshi kilitozwa Sh. 46/= kwa kilo kama gharama za kukoboa na kuhifadhi kahawa kwenye ghala kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba maghala yanatakiwa yajengwe sehemu ambazo zina miundombinu kama barabara ili mazao yaweze kufikishwa na kuchuliwa ghalani wakati wowote. Vigezo muhimu vinavyozingatiwa katika kuweka madaraja ya maghala mojawapo ni kuwepo kwa miundombinu. Hata hivyo, ujenzi wa maghala utategemea uwingi wa mazao katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *program* mbalimbali kama ile ya Uboreshaji wa Mifumo ya Masoko ya Mazao ya Kilimo umeshaanza jukumu la ujenzi wa maghala kwa kuziwezesha Halmashauri za Wilaya mbalimbali katika nchi yetu. Serikali pia itahamasisha ujenzi wa maghala ya ubia kati ya Vyama vya Ushirika, Halmashauri na Taasisi nyingine.

Pamoja na kuendelea kuhamasisha Sekta binafsi, mkazo zaidi utakuwa kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika. Kwa sababu kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, ni kutokana na gharama zake kuwa ndogo kuliko yale ya watu binafsi na wote tunaelewa tunaotoka katika sehemu ambazo kuna Vyama vya Ushirika kwamba Chama cha Ushirika na maghala yake ni ya wanachama wenyewe na hawatozwi gharama zaidi kwa kuyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, alituhimiza kwamba tuhakikishe kwamba kuna maghala ya samaki Nansio Ukererewe na sisi tunakubaliana naye kwa sababu ndio zao kubwa walilonalo. Kama Mheshimiwa Naibu Spika alivyosema, wale wenye mipango mbalimbali ya kuwasaidia wakulima tutahakikisha kwamba jambo hili wanalifanyia kazi. Kwa kuanzia *definition* ya samaki imeonyeshwa chini ya *definition* ya *goods* katika Muswada huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Getrude Mongella awe na uhakika kwamba hoja yake tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo ningetaka kuzungumzia ni ile hoja ya huduma za Kibenki. Hoja hii ilihusu ushirika wa Benki nyingi kutoa huduma za Kibenki kufika hadi Vijijini kwa riba nafuu. Waheshimiwa Wabunge wengi walihoji kama ukiondoa zile Benki ambazo tumefikia nazo katika kipindi cha majaribio za *CRDB*, *Kilimanjaro Cooperative* na *Exim*, kama kweli Benki nyingine zinayo hamasa kuingia katika mtindo huu. Waliochangia hoja hii ni Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Eliachim Simpasa na Mheshimiwa Ibrahimu Marwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya jana, katika kipindi cha majaribio, ni Benki tatu, Benki za *CRDB, Exim* na *Kilimanjaro Cooperative Bank* zilizoshiriki kikamilifu. Aidha, mazungumzo yanayofanyika sasa na Benki za *Standard Chartered,* Benki ya *Stanbic, National Bank of Commerce, NMB* na Benki ya Posta na zote zimeonyesha kwa dhati mtazamo wa kushiriki pindi kitakapokuwepo chombo cha sheria cha kusimamia matumizi ya mfumo huu.

Kwa hiyo, wasiwasi waliokuwanao Waheshimiwa Wabunge haupo. Ningetaka kuongeza kwamba kwa sasa hivi, wale wanaofuatilia biashara ya Mabenki hasa katika nchi yetu ya Tanzania biashara kubwa ya Mabenki na wanakopata faida yao kubwa ni biashara ya mazao. Kwa hiyo, hakuna Benki ambayo hawawezi kusema hawatashiriki kwa sababu ndiko chakula chao kinakotoka. Kwa vile mfumo huu unalenga kuwanufaisha wakulima ambao wengi wao wapo Vijijini, ipo haja ya kuchambua kwa makini ufikishwaji wa huduma hii kwa wale waliopo Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki yanayo utaratibu; kama wao hawana mtandao Vijijini, kutumia mabenki mengine ambayo yana mtandao huo Vijijini pamoja na kuimarisha Benki za Wananchi, yaani *Community* na *Cooperatives Bank* zilizopo na nyingine zitakazoanza baadaye. Aidha, ili kuwafikia wakulima Vijijini, Benki ziko tayari kutumia Vyama vya Akiba na Mikopo yaani *SACCOS* kuwa kama Wakala wao katika zoezi hili zima. *(Makofi)*

Hivyo sasa, Benki ya *CRDB* tayari imeshaanza kutekeleza utaratibu huu wa kutumia *SACCOS, SACCAS*, Benki za Mikoa na kadhalika. Taasisi nyingine za Fedha, mfumo mzuri ni *SACCOS* ya Kibaigwa iliyoko Dodoma. Pale Benki zote za Biashara zinatumia *SACCOS*. Kuwepo kwa sheria kutatoa imani kwa Asasi za fedha na hivyo kuongeza ushiriki na ushindani ndani ya Mfuko huu.

Hali hii itaongeza ushindani na kupelekea utoaji huduma bora zenye ufanisi na riba nafuu. Mfuko huu wa kutumia waendesha maghala hupunguza gharama za kusimamia mkopo hadi kufikia asilimia 12 kama nilivyoeleza ikilinganishwa na zile zinazotolewa nje ya Mfuko huu ambazo ni riba ya asilimia 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa mara nyingine kukushukuru sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia maoni na mapendekezo mazuri ya kuboresha utekelezaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao yaliyowekwa kwenye Maghala wa Mwaka 2005**
***(The WarehouseReceipts Bill, 2005)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla Katibu hajaendelea, kama mnavyouona Muswada huu ni mrefu sana. Kuna Ibara mpaka ya 79.

Kwa hiyo, Katibu atasoma kwa sehemu na yeyote mwenye hoja yoyote kwenye sehemu yoyote inayohusu Ibara yoyote chini ya sehemu hiyo, basi asimame aweze kutoa hoja yake.

Sehemu ya 1
Sehemu ya 2
Sehemu ya 3
Sehemu ya 4

*(Sehemu zilizotajwa hapo juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 5

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa na lile tatizo la kwamba Serikali katika suala hili zima imekuwa katika maeneo yale ya wakulima ambao wamekuwa na ahadi ya *STABEX*. Sasa kuna vitu ambavyo vilikwishaahidiwa, navyo vinafanana na hivi.

Sasa katika kifungu hiki ambacho kinahusiana na hii 31; Je, Waziri anasema nini hasa kuona kwamba sisi kule tunao wakulima ambao waliahidiwa tena Waziri wa Kilimo naye aliahidi kwa kushirikiana na Wizara zote hizi mbili kwa suala zima lile la barabara ili maghala haya yaweze kuimarika? Utapelekaje kwenye maghala hayo wakati barabara hizi ni mbovu? Sasa kuna hela ambazo zilikwishatolewa kwenye Bajeti iliyopita, sasa maelezo hayafanani. Hebu nipate maelezo! *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuandaa mipango ya kutengeneza barabara chini ya *STABEX* bado inaendelea. Lakini nafurahi kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kiasi cha Shilingi milioni 939 zimetengwa kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma na nyingi zitatumika katika eneo lililoahidiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuniona. Mimi naongeza kidogo tu kwenye Ibara ya 38(b), ningependa kufuta maneno: *"The Resident magistrate"*, badala yake kuweka *"an affidavit sworn before a commissioner of Warehouse."*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Maana hiyo ni sheria, anapendekeza kifutwe hicho kifungu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la Mheshimiwa Mkono ni kuondoa maneno: *"The Resident Magistrate"* na Serikali inakubaliana naye kwa sababu kilivyoandikwa ni finyu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawasumbua sana wananchi katika maeneo mengi ya nchi yetu ambapo hawa Mahakimu Wakazi hawapo na kwa vile Sheria ya A*uction and that state declaration* inatoa tafsiri pana ya neno alilotumia Mheshimiwa Mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Commissioner for Ox* inajumuisha pia Mahakimu wa ngazi mbalimbali na Mawakili wa Serikali na Mawakili wa kujitegemea na wengine. Kwa hiyo namshukuru sana katika pendekezo lake hilo. Serikali inalikubali. *(Makofi)*

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 6
Sehemu ya 7

*(Sehemu ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Sehemu ya 8

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya 9

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao yaliyowekwa kwenye Maghala wa Mwaka 2005**
***(The Warehouse Receipts Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada uitwao, *The Warehouse Receipts Act 2005*, pamoja na marekebisho yake kifungu kwa kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Warehouse Receipts, Act 2005* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tumefika mwisho wa shughuli za leo. Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12. 52 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 21 Aprili, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*